ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaybah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 26 Juni, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2010/11.

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2010/11. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohamed Ali Salim: (Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya upande wa upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2010/11. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 9

Raslimali za SMZ Dar-As-Salaam na Mwanza

Mhe. Said Ali Mbarouk: (Kny: Mhe. Juma Duni Haji) - Aliuliza:-

Ni rasilimali kiasi gani ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekeza katika Jiji la Dar-as-Salaam na Mwanza; miji ambayo ina wakaazi wengi na mzunguko mkubwa wa biashara, ili kuongeza vianzo vya mapato yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kuwekeza katika Miji ya Dar-es-Salaam na Mwanza katika maeneo ya Biashara ya Bima, ambapo shirika hilo hivi sasa limewekeza kiasi ya milioni 810.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, miji ambayo ameitaja Mhe. Waziri ni miji ambayo ina watu wengi sana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli kama Serikali ya Mapinduzi ingeweza kuekeza vizuri, basi hakika tungeweza kupata mapato mengi ambayo yangewezesha hazina ya Zanzibar kutononoka kidogo.

Je, kwa nini serikali haijawa na sera madhubuti ya kuona kwamba fursa za kuekeza katika mabenki, biashara ya Shirika la Meli na biashara ya jumla katika miji hiyo haijaekezwa. Huoni kuwa tunakosa fursa nzuri ya kukuza uchumi wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba ni kweli kwamba serikali yetu ingeweza kufungua milango zaidi katika upande wa Tanzania Bara, hasa kwa vile miji hiyo niliyoitaja ni mikubwa.

Kwa upande wa PBZ, alizungumza upande wa benki. Upande wa benki tayari mipango iko njiani ya wenzetu PBZ kujaribu kuekeza Dar es Salaam. Wana mpango hata wa kwenda Arusha na Mwanza. Lakini kwanza wanajaribu kuona vipi wanaweza kuingia Dar es Salaam kwa lile soko lilivyokuwa kubwa na kupata ushindani hasa katika biashara zao.

Kwa hivyo, ni kweli nakubaliana na wewe kwamba iko haja. Hata upande wa Shirika la Meli nakumbuka tulikuwa na matawi yetu kule, lakini baada ya muda yalikufa wakati shirika lenyewe nalo lilipokuwa na matatizo. Kwa kweli *investment* inayofanywa, mfano wa Shirika la Bima katika hiyo miji niliyoitaja sio kidogo. Mhe. Spika, naweza kusema kwa mwaka jana tu wameweza kukusanya shilingi bilioni 6,379,418,000 kwa mtiririko ufuatao.

Dar es Salaam wameweza kukusanya shilingi bilioni 4,555,000,000. Mwanza wameweza kukusanya shilingi milioni 798,960,000. Arusha wameweza kukusanya shilingi milioni 611,000,000 na Mbeya wameweza kukusanya shilingi milioni 413,242,000. Jumla kama nilivyosema ni shilingi bilioni 6,379,418,000. Kwa hivyo, hiyo mikoa minne tu unaona *volume* ya biashara na faida tunazopata. Kwa hivyo, nakubaliana na yeye ni kweli kwamba iko haja ya kutanua zaidi wigo wetu kwa kupata mapato.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba ruhusa yako ya kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri ametujibukuwa rasilimali ambazo zimewekwa katika mji wa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na akaongezea na Mbeya ni rasilimali inayohusiana na vyombo vya kifedha.

(a) Pia Mhe. Spika, nakumbuka kwamba tuna rasilimali ya mambo ya kilimo na mifugo Makurunge. Mbona Mhe. Waziri hakutujibu?
(b) Vipi hatima ya rasilimali hiyo ilioko Bagamoyo Makurunge?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, mradi wa kuendeleza ufugaji Makurunge ni mradi wa kihistoria kwetu. Hapo zamani kulikuwa na dhamira nzuri tu na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuekeza pale Makurunge kupata nyama kwa kitoweo kuleta hapa.

Mhe. Spika, lakini kwa bahati mbaya mradi ule kutokana na matatizo mengi sana, kwa kweli haukufanikiwa lengo lake na hatimaye ulisambaratika. Hivi sasa serikali kwa eneo lile lililobaki ina mipango ya kuliekeza kwa kupitia vijana wetu katika mradi wa kilimo mbali mbali kupitia vijana wa JKU. Miradi hiyo iko njiani, lakini namuomba labda Mhe. Spika, tumpe ruhusa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira aje kujaribu ku *propound* zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Waziri, naomba kutoa maelezo zaidi kwa Mhe. Haji Mkema Haji. Ni kweli alivyosema Mhe. Waziri, lakini pamoja na hayo, nafikiri suala hili tulilizungumza sana. Hivi sasa serikali au wizara yetu tunawasiliana na wenzetu kule Bara kuhusu shamba hili la Makurunge na tumefikia pahala pazuri. Titizo lilikuwa ni suala la hati miliki. Kwa sababu serikali kwa serikali, wanasema wenyewe wataalamu kwamba haiwezekani serikali ikawapa hati miliki serikali.

Kwa hivyo, sasa hivi uwamuzi tuliofikia ni kwamba wizara yetu tumekubaliana na wenzetu Bara kwamba eneo lile sasa tutalikabidhi kwa Chuo chetu cha Kilimo, ambacho ndio hasa muafaka. Maana yake Chuo chetu cha Kilimo cha Kizimbani kinashughulika na mambo hayo ya kilimo, kwa hiyo tumeona ni jamo la busara ikiwa tutawapa wao suala hili, kwa mantiki kwamba wao sasa hivi wanaweza kupewa hati miliki. Mara tu baada ya kupewa hati miliki dhamira yetu tushirikiana na serikali kuu kuliamrisha serikali kuu kama vile ambavyo ilivyokuwa zamani.

Kwa hivyo, tunangojea mara tu tukipewa hati miliki ambayo sasa hivi tumo katika mpango wa kuwasiliana na wenzetu kuweza kuipata hati miliki.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, nilikuwa nimeshakata tamaa, lakini nakushukuru. Mhe. Spika, Shirika la Bima ni chombo ambacho ni cha biashara na mfanyabiashara yeyote ili mizigo yake na biashara yake iende vizuri basi hutegemea kuwekeza katika Bima.

Lakini katika nchi yetu ya Tanzania kuna mikusanyiko mingi, ukiacha haya maeneo ya miji aliyoitaja Mhe. Waziri, kwa mfano Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya. Lakini pia tuna miji mizuri ya biashara kama Mtwara, Arusha, Dodoma na Tanga. Mimi suala langu liko hapa Mhe. Spika, kwa kuwa Mtwara palikuwa na biashara kubwa sana kati ya Zanzibar na Mtwara au Mtwara na Dar es Salaam kwa usafiri wa vyombo vyetu vya meli au majahazi.

Hivi Mhe. Waziri ana mpango gani kwa makusudi kwa upande huu kuhakikisha kwamba huduma hiyo inafika ili wafanyabiashara wawe salama na huduma hiyo kwa ajili ya usalama wa vitu vyao.

Mhe. Waziri wa Nchi(AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba kweli kuna miji mingine ambayo ina upeo mzuri wa biashara kama alivyoitaja mwenyewe Mtwara, Arusha. Arusha tayari Shirika la Bima wapo. Alitaja Dodoma na hata Tanga.

Mhe. Spika, ni lengo hasa Bima kwenda kote huko. Lakini suala la msingi naomba Mhe. Spika, afahamu Mhe. Ali Suleiman kwamba biashara yoyote ni ushindani. Kwanza unaangalia wapi liko soko na ushindani. Hasa hilo nilosema wapi lipo soko na ushindani uliopo. Sasa kama Mtwara kuna soko kuwazidi labda Mwanza au Arusha, basi ni imani yangu basi Shirika la Bima wangeanza huko. Lakini wamegundua kwamba soko liko Mwanza zaidi, Arudha, Mbeya na Dar es Salaam yenyewe. Sasa huko kidogo kidogo naamini tutafika huko.

Lakini Mhe. Spika, wacha kwanza tu *concentrate* kwenye hii miji minne ambapo uzito wake wa biashara ni mzuri na kuna mafanikio makubwa tu katika biashara hii ya BIMA. Kwa hivyo, lengo letu ni kujitanua zaidi kadiri ya ushindani na soko linavyopatikana. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 90

Ukosefu wa Madaktari na Wauguzi Hospitali ya Fuoni Kibondeni

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny: Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu) - Aliuliza:-

Huduma za afya kwenye Kituo cha Afya Fuoni Kibondeni zinakwazwa na ukosefu wa wataalamu wa fani ya udaktari na uuguzi.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni nini sababu ya kukosekana wataalamu hao katika kituo hicho?

(b) Kwa kuzingatia kuwa afya bora kwa kila mwanachi ndio sera ya Serikali, Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kukosekana kwa madaktari na wauguzi wa kutosha katika Hospitali ya Kibondeni kunawakosesha wananchi wa Fuoni Uwandani, Fuoni Kibondeni, Fuoni Kitongani na Kichaka Punda pamoja na maeneo jirani huduma ya Afya bora?

(c) Je, Mhe. Waziri ni lini wewe mwenyewe au Naibu wako mtapata nafasi ya kuwatembelea wafanyakazi wa Hospitali hiyo pamoja na wananchi wa maeneo hayo kwa lengo la kuwasalimia na kujua matatizo yao?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 90 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kituo cha Afya Kibondeni ni kituo cha daraja la kwanza yaani (1 st line) kinachohudumia jumla ya wakaazi 6,192 kutoka maeneo ya Fuoni Uwandani, Kibondeni, Kitogani na Fuoni Kichaka Punda.

Kwa sasa kituo hicho kina wafanyakazi (5) wanaotoa huduma za afya, wakiwemo mganga msaidizi 1 wauguzi 2 na *Ordaly* 2. Pia wafanyakazi wa Kituo cha Afya Fuoni huwa wanatoa huduma za uzazi wa mpango na kutoa chanjo kituoni hapo wiki mara moja kwa njia ya *Outreach*. Idadi ya wafanyakazi waliopo inatosheleza kutoa huduma kwa hivi sasa.

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa ni jukumu la Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Afya kutembelea hospitali na vituo vyote vya afya hapa nchini, kikiwemo Kituo cha Afya Fuoni Kibondeni. Tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo kwa Unguja na Pemba na kwa mujibu wa ratiba za kazi zetu zilivyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Hivi sasa vituo vingi vya afya vya mashamba hasa Mfenesini vina upungufu wa wafanyakazi. Utaona *nurse* alioko pale ndio afagie, achemshe sindano na mambo mengine.

Je, haoni kwamba katika mapengo hayo wangejazwa ma- *orderly* ili wakaweza kusaidia kazi hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, upungufu wa wafanyakazi katika kada mbali mbali kwenye vituo vyetu na hospitali zetu tunaufahamu na juhudi ya kufanya ili kuyaziba mapengo hayo tunajitahidi kuchukua. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe awe mstaamilivu kidogo, jitihada tunazichukua muda sio mrefu hili suala litaweza kutatuka katika hospitali zetu. Ahsante.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, mimi napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nilikuwa na taarifa kwamba muuguzi mmoja alikuwa na likizo bila malipo kwa muda mrefu pale. Lakini sijui kama huyo amerejea au bado hajarejea kazini na kulikuwa kuna sababu zipi za kuchukua likizo bila malipo kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni kweli muuguzi mmoja aliyeko pale analikizo bila malipo. Sababu za kuchukua likizo bila malipo Mhe. Spika, mara nyingi hutokana na mtu dharura zake binafsi. Inategemea mwenyewe shida aliyokuwa nayo ndio inayompa achukuwe likizo bila malipo.

Kwa hivi sasa mimi sina uhakika ni sababu gani aliyochukulia, lakini bila shaka yeye mwenyewe anaifahamu shida hiyo ndio akaona achukuwe likizo bila malipo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi, alisema kuwa Fuoni Kibondeni wafanyakazi wanatosha. Lakini hoja ya mjumbe inalalamika kwamba kuna huduma ya kusuasua.

Hivi unataka kutuambia Mhe. Naibu Waziri kwamba waliopo ni wavivu au wana sababu gani, kwa sababu anasema wapo wa kutosha. Kama ni wavivu si vyema akawapeleka wengine ili huduma ikapatikana kwa ukamilifu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, mleta hoja alileta swali lake kuhusu wafanyakazi kuwa kidogo ndio maana pana huduma ya kusuasua. Lakini wafanyakazi wanatosha. Sasa suala la kusuasua huduma, sisi hii taarifa hatuna, itabidi tuifuatilie. Lakini tunavyoelewa sisi, wafanyakazi wakiwemo wa kutosha, vitendea kazi vikiwa vipo vya kutosha na huduma zote pale zipo zinapatikana, basi huwa hakuna sababu ya kusuasua. Labda angekuwepo mwenyewe aliyetoa hoja angesema kuwa hii kusuasua aliyokusudia ni ya namna gani.

Lakini sisi tunaamini kuwa pale Fuoni Kibondeni shughuli zote zinakwenda vizuri, kwa sababu huduma ziliopo zinatosheleza kwa kituo kile, ahsante Mhe. Spika.

Nam. 73

Utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika Ilani ya Uchaguzi ya 2005 – 2010 Chama cha Mapinduzi kilionyesha malengo yake ya utekelezaji katika nyanja mbali mbali ikiwemo sekta ya Mawasiliano ya barabara.

Ni barabara ngapi zilizoahidiwa kujengwa zimejengwa katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa ilani hiyo kwa kiwango cha lami?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 73 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kilitoa malezo katika sekta ya Mawasiliano kwa kujenga jumla ya km. 252 zenye kujumuisha jumla ya barabara 19.

Katika utekelezaji wa Ilani hiyo Jumla ya barabara 10 zllijengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami na barabara 9 hivi sasa ujenzi wake unaendelea, na wakandarasi wapo katika maeneo kazi yaani *site*. Aidha, barabara kadhaa zilifanyiwa matengenezo makubwa na nyingine kujengwa kwa kifusi. Licha ya kujengwa kwa barabara hizo na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005-2010, Serikali pia ili zijenga barabara nyengine ambazo hizikuwemo katika Ilani kutokana na barabara hizo kuwa katika hali mbaya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba ilani ya CCM iliahidi kujenga barabara 19 zenye urefu wa km.252. Lakini hadi hii leo ni barabara 10 tu ndio ambazo zimemalizika katika kiwango cha lami na barabara 9 zinaendelea na ujenzi.

(a) Je, katika barabara hizo 9 ni pamoja na ile barabara ya Bumbwini ambayo hata kazi haijaanza?
(b) Kama kuna barabara ambazo hazitomalizika, anakusudia kuniambia kwamba ilani ile ilikuwa haitekelezeki?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane naye kwamba katika miongoni mwa barabara ambazo hazikukamilika ni pamoja na barabara ya Mfenesini Bumbwini.

Pia kuna barabara ya Amani Dunga, pamoja na barabara ya Kengeja Mtambile, Mwambe Kenya Chambani, Mzingani Wambaa, Chanjamjawiri Pujini, Mtambile Kangani, Chanjamjawiri Tundauwa, pamoja na barabara ya Mgagadu Kiwani ambapo Mhe. Hija mwenyewe ndio Jimboni kwake.

Kuhusu kukamilika Mhe. Spika, lengo letu ni kuzikamilisha barabara hizi, lakini pale ambapo itakuwa hazikukamilika basi zitakuwa zinaendelea, kwa sababu bado ziko katika mpango ambao umepangwa sahihi. Kwa hvyo, tunategemea kwamba ilani hiyo itakuwa imetekelezeka vizuri kwa asilimia 90.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika kutaja barabara 9 ambazo bado hazijatengenezwa na ambapo ilani ya CCM inaeleza kuwa ni kutengeneza barabara nyingi tu kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Spika, barabara ya Mtambwe ambayo haijapitiwa tokea Mapinduzi au kabla ya Mapinduzi mpaka leo haikutajwa, na kule kuna watu na mahitaji ya barabara kila mtu anaelewa. Nimejitahidi na yeye mwenyewe mpaka kumkaguza kuona hali ilivyo, angalau kupitisha kiparapara tu watu waweze kupita, wachilia mbali hicho kifusi mpaka leo hakujafanywa lolote.

Je, katika ilani hii ya CCM ilisema isipokuwa barabara ziliopo katika Jimbo la Mtambwe mpaka ikafika hadi leo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tulifanya ziara jimboni kwake na kuona hali ya barabara. Mhe. Spika, ni kwamba barabara ya Mtambwe nayo imo katika kujengwa,

lakini haimo katika hizi barabara 9, hii imo katika barabara zitakazojengwa na MCC.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kabla sijauliza napenda sana kuipongeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kujenga barabara nyingi, nzuri na ikiwemo ile ya Pwani Mchangani ambayo siku hizi yako mashindano ya msererekо wa magari kwa ule uzuri wake. Pia zaidi ya mchezo huo na mingine inaandaliwa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa ahadi ya Mhe. Rais alipokuwa anaomba mwaka 2005/2010, aliagiza kwamba barabara ya Kijini ishughulikiwe ili ipitike. Lakini mpaka leo hakuna dalili. Hivi Mhe. Naibu Waziri unataka kutuambia kauli ya Rais haina nguvu na kama ina nguvu kwa nini huoneshi dalili kwamba angalau kuipiga *grader* au kifusi ili ikaweza kupitika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama unavyoelewa kwamba barabara zinazotaka kujengwa ni nyingi katika nchi yetu, na miongoni mwa barabara hizo ni pamoja na barabara ya Kijini.

Mhe. Ame Mati Wadi atakuwa shahidi tulikuwa pamoja wakati Mhe. Rais alipotembelea pale kufungua Skuli ya Kinuni na akatuagiza hili. Lakini kutokana na kazi ambazo tumepanga, basi haijafikia awamu tuliyopanga kwenye barabara hii. Lakini tunategemea kwamba barabara itajengwa kama zinavyojengwa nyengine.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea nafikiri tutaweza kusikiliza kama wajumbe sita miongoni mwa walioomba, kama wapo zaidi labda wanane na baadaye tumwite Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho.

Kwa hivyo, ninawaomba tupunguze kurudia, kwa sababu maelezo ya wajumbe na ingawa kuna mambo yanaekewa msisitizo, lakini maelezo ya wajumbe yakurejea sana kiasi cha kusema labda tumemaliza yale ya kuchangia mapya kuliko ambayo tayari yameshachangiwa. Kwa maana hiyo, napenda kuchukua

fursa hii tena kusisitiza kwamba Waheshimiwa Wajumbe tupunguze kurejea, ili tupate nafasi ya kuwaita wajumbe wengi zaidi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kwa kuwa umesema tusirudie na vile jana jioni sikuwahi kuyasikia, kwa hiyo naomba unistahamilie kwa yale nitakayochangia na nitajitahidi kwa ufupi kiasi ya dakika tatu mpaka tano.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kushirikiana na kuweza kutekeleza yale mambo wananchi wanayahitaji. *(Makofi)*

Vile vile nampongeza tena Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa kufanikisha suala la umeme kutoka Tanga kwenda Pemba. Pia nampongeza kwa mara nyengine kwa kuchukua jitihada za juu zaidi kama tulivyoahidiwa kule Pemba, kwamba umeme utaletwa na wananchi wa Pemba watakuwa na umeme milele daima.

Kwa kweli wananchi wa Kisiwa cha Pemba tulikuwa kama tumo kwenye kaburi, kutokana na kukosa kwa umeme kwa muda mrefu. Kwa hivyo, nawaomba wananchi wa Pemba waipokee hidaya hii aliyotutunukia Mwenyezi Mungu, ambayo wenzetu walijitahidi kuitafuta kwa hali na mali mpaka kutufikia kule Pemba. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha au kuwaomba wananchi wa Pemba, wautumie umeme kwa ajili ya kutafuta miradi ya maendeleo kwa lengo la kuwekeza na kujitafutia maisha yao. Kwa hivyo, wasitumie nafasi kuonesha *video* na kuangalia michezo mbali mbali ikiwemo mpira wa miguu kwa mashindano ya timu za Ulaya, kama vile timu ya *Liverpool. (Makofi)*

Kwa hiyo, wanaomba wananchi wa Pemba wachukue jitihada za kuwekeza, ili walete maendeleo kisiwani Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo jengine nataka kumuuliza Mhe. Waziri ni kitu gani kinachosababisha kuchopoka nyaya mara kwa mara kisiwani Pemba, hasa sehemu za vijijini katika *transformer* na kusababisha umeme kuwaka mwekundu mfano kama kaa la moto katika kijiji hasa cha Kukuu Kangani.

Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kuhusu ule umeme uliokatwa na nguzo kung'olewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kangani/Mtambile, umeme huu utarejeshwa lini katika kijiji cha Mtakakaa/Mtambile?

Mhe. Spika, suala la mwisho ambalo linawaumiza wananchi wengi na hasa sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi linatuumiza vichwa. Kwa hivyo, nimuulize pamoja na kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atupe ufafanuzi zaidi kuhusu suala la mafuta na gesi asilia limefikia hatua gani, kwa sababu mpaka hivi sasa limetuweka njia panda sisi wajumbe wako.

Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri atupe ukweli hasa kuhusiana na suala hili au zile kelele tulizokuwa tukipiga hapa Barazani zilikuwa za bure. Kwa kweli mpaka hivi sasa tunao wasi wasi mkubwa sana, hivyo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atoe kauli zake kama vile alivyokuwa akisema kwamba hatowasaliti Wazanzibari mpaka kufikia hatua hii. Vile vile anao uchungu wa Wazanzibari, wananchi pamoja na vizazi vijavyo. (*Makofi*) Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Assaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, niwapongeze Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kufika kwa wakati kuendelea na shughuli ingawaje leo ni siku ya Jumamosi.

Mhe. Spika, niungane na wenzangu, lakini nianzie na pongezi zangu za dhati kabisa kuwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wakiongozwa na Katibu Mkuu wao. *(Makofi)*

Mafanikio yanayozungumzwa leo pamoja na sifa nyingi za Mhe. Waziri ni baada ya kazi nzuri iliyofanywa na wao. Kwa hivyo, leo Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi Mhe. Mansoor Yussuf Himid Maftah (*original* mwana wa kindakindaki *ASP*), ndio maana amefika hapa, kwa sababu wanazo sifa zao hao. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, niende kwenye suala la maji kama yanavyotajwa ni uhai, umuhimu wa maji unaeleweka. Lakini hivi sasa nitazungumza ni vipi ndani ya Jimbo langu la Wete yanapatikana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba kwa kupitia kwako Mhe. Spika kama anavyoombwa, kwa sababu ni msikivu, mahiri, lakini ni jasiri, yaani anajiamini.

Kwa maana hiyo, namuomba sana kwani ninavyo vijiji vyangu pamoja na mitaa, kama vile Selemu, Kipangani cha Juu na Kipangani cha Chini, Mkwajuni hapa ni Wete. Vile vile kuna Ujinga ni kijiji na Kipange kwa Shehia ya Pandani, wananchi wangu kwa kweli wanasumbuka sana na huduma hii ya maji.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda, basi nitajitahidi. Sasa nizungumzie kuhusu Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Kwa kweli hii ni

haiba kubwa Mwenyezi Mungu ametujaalia na mji wetu kuingia kwenye Urithi wa Dunia.

Siku chache zijazo kuna Mkutano Mkubwa wa Kanda ya Afrika ya Mashariki, ambao utafanyika hapa. Lakini hali ya mji huu bado haijaridhisha na wala haipendezi, yaani uchafu bado Mji Mkongwe umekithiri.

Tatizo liko baina ya Mamlaka na Baraza la Manispaa. Nadhani kwa hii dharura inayotukabili Mhe. Waziri aunganishe nguvu za Mamlaka na Manispaa kwa ajili ya wageni, bila ya shaka watakapofika watatembezwa kwenye mji huu na kuepusha kupata aibu, kwa sababu hali ni mbaya sana.

Mhe. Spika, kuhusu suala la nishati na madini kuna mambo ambayo yamepangwa, kwa ajili ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa hiyo, imechagua machache kushirikiana kikamilifu juu ya suala la nishati na Jumuia ya Afrika ya Mashariki ni vyema.

Namuomba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wazidishi umakini wao, wakielewa wazi kwamba bado tunalo suala la mambo yaliomo ndani ya muungano, ambayo yamekwama na sasa kuna suala la Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, tukikwama mara mbili basi ni mtihani mzito kwetu.

Kwa hivyo, naomba sana wakashirikiane na kuzungumza kwa yale yanayozungumzika. Lakini wenzetu hapo Bara suala la ardhi walisema hapana na wala sio dhambi, hivyo kwa upande wetu basi wanayoyahisi haya hayana maslahi na Zanzibar yetu waseme hapana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna utekelezaji wa *program* ya mafuta na gesi kwa masuala ya mafunzo. Kwa kweli hili ni jambo zuri na Mhe. Waziri aendelee na shughuli hii na aongeze nguvu kwa vijana wetu waendelee kusoma. Lakini kuna jambo moja ambalo nataka niseme Mhe. Spika, tunapata tabu sana, kuna kile chombo kinachotumika kupimia viwango vya haya mafuta, kwa sababu tunawaagiza wenzetu hawa waje na hapa tunapoteza baadhi ya mambo.

Suala jengine ni ujenzi wa njia hii tunayoisubiri kwa hamu kubwa ya umeme kutoka Ras Kilomoni hadi Fumba. Mhe. Spika, jambo hili limeshazungumzwa sana, kwa hivyo naomba hapa tujipange kwa sababu hali si nzuri na sote tunashuhudia tunayotendewa nadhani sio bure lipo jambo, kwa hivyo tusijekupigwa mara mbili. Kwa kweli Mhe. Waziri ninamuamini sana na hili alisikie na wala lisijekutufikisha mahapa baya sana. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sana nizungumzie kuhusu suala la mipango miji. Hapa napenda kusisitiza kwamba miji yetu wahusika waangalie sana

geography ya visiwa vyetu, matumizi ya ardhi tunavyokwenda nayo, kwa hiyo, lazima tufanye liwezekanalo na tuhakikishe kwamba kile kinachofaa ndicho kinachowekwa mahala panapofaa.

Miji ipimwe, ramani zisomwe na zifuatiliwe, kwa sababu ujenzi wetu umekuwa ovyo mno na wala hapatambuliki wapi pa kuchezea na wapi pa kuweka jaa, wapi pa kujenga nyumba na sehemu gani ya kulima. Kwa kweli hali hii kwa jinsi ya visiwa hivi vilivyo hatuwezi kwenda namna kama hiyo na hata kama tungekuwa na ardhi kubwa kiasi gani hatuwezi kuharibu kama inavyoharibiwa leo.

Mhe. Spika, kuna mwenzangu mmoja jana alisema lazima itafutwe *formula*, mimi nasema *formula* tunayo nadhani wenyewe bado tunasuasua juu ya hili. Nasema hivyo, na wala si kwa furaha ni kwa machungu sana baada ya kumsikia Mhe. Waziri Kiongozi wetu amemuandikia barua Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri Mkuu amesema kwamba Zanzibar si nchi, wenyewe tuliponyanyuka kwa ajili ya kuitetea alisema wala sijateleza na kusema anarudia tena, yaani alisema hivyo hivyo. Sasa leo tunamuandikia yeye barua kwamba mafuta ni yetu wenyewe na tunaomba ruhusa kwake mbona kizungumkuti.

Mhe. Spika, hivi suala hili limo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kama Katiba basi na gesi imo ndani ya Katiba na kule kwa wenzetu Songosongo *gas* na *gas* hii kwa mujibu wa Katiba ni ya Muungano. Naamini kwamba Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi hata hesabu ya kipi kinazaliwa mpaka leo hajui, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar haijui, kilichouzwa sisi hatujui, lakini baada yake inaingizwa kwenye *Grid* ya Taifa na kuuziwa tena kwa bei hii tunayopiga kelele hapa. *(Makofi)*

Hivyo, sisi lipi linalotufanya tusiweze kujiamini juu ya hili, wanajiamini wao kwa sababu gesi inatoka Songosongo ni kwao. Kwa hivyo, na sisi lazima tujiamini kama mafuta yatatoka Wambaa, Fundo, Gando au Mtambwe, almradi ni ardhi ya Zanzibar hii iwe baharini au nchi kavu, hayo ni yetu na itabaki Katiba kama ilivyo na wala hatuivunji. Mhe. Spika, kama ni halali gesi inavyofanywa kwa nini iwe haramu kwa mafuta. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru kwa hayo machache na naunga mkono hoja kwa asilimia zote. *(Makofi)*Ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii iliyowasilishwa jana ya Mhe. Waziri

wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2010/2011.

Nimpongeze Mhe. Waziri Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wao wote kwa kuleta hotuba fupi, lakini imefahamika na imeeleza nyanja nyingi *(Makofi)*.

Kwa hivyo, niwapongeze kwa utendaji wao wa kazi na kama kungekuwa na mashindano ya kuweka *marks* katika wizara basi nadhani wizara hii ingechukua *marks* nyingi sana. Lakini bahati mbaya huwa hapana *marks* na kila mtu anafanyakazi kwa mujibu wa uwezo wake. Hivyo, nawapongeza sana na ninaomba washikamane katika kutekeleza majukumu ya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitakuwa na *points* nne tu na nyingi ni kusisitiza nianzie ukurasa wa 43 kuhusu matengenezo ya dharura yaliyofanyika wakati wa kurejesha huduma za umeme katika Kisiwa cha Unguja kutoka Fumba na Ras Kilomoni.

Mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi miaka miwili iliyopita na kuna tatizo ambalo tunaliona dogo, lakini baadaye litakuwa kubwa. Kwa kweli juzi liliulizwa swali hapa kwamba Ras Kilimoni kituo kile cha kuleta umeme huku kinaathirika kwa chumvi kwa sababu kipo katibu na bahati, tuliambiwa utaratibu wa kujengwa upo na eneo limeshapatikana. Lakini hivi sasa ni mwaka wa tatu maneno ni hayo hayo.

Mhe. Spika, naiomba wizara suala hili tusilidhararu, kwa sababu kama hatukuziba ufa, basi tutajenga ukuta. Kwa kweli kile kituo kinaathirika kila mwaka na hutumia fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo. Kutokana na hali hiyo, ninashauri kama eneo lipo basi zingeomba fedha serikalini tukakirudisha nyuma kwa ajili ya kuondosha kazi ya kila mwaka kutengeneza na huu ni ushauri kwa wizara. *(Makofi)*

Hoja yangu ya pili kwenye ukurasa wa 46 kuhusu usimamiaji wa ardhi na eka. Mhe. Spika, niipongeze wizara kwa kutanabahi, mimi naona wamechelewa, lakini kwa kuwa wamezinduka hivi sasa basi sina budi kuwapongeza.

Kwa kuwa eka zilitolewa na Rais wetu wa mwanzo wa Zanzibar marehemu Mzee Abeid Amani Karume mwaka 1964, kwa lengo la kusaidia wananchi wengi katika nchi yetu, kwa ajili ya kulima pamoja na kufanya mambo mengi ya maendeleo kwenye eka hizo. Katika miaka ya hivi karibuni malengo hayo pamoja na dhamira imebadilika, sasa eka watu wanaziuza kwa kuchimba mchanga pamoja na kujenga nyumba. Lakini jambo la kusikitisha imekuwa hadithi ya bata kuna mtu alifuga bata akawa anataga yai la dhahabu, akaona kwa kuwa bata anayo mayai ya dhahabu mengi kwa nini kusibiri moja moja,

matokeo yake alimchinja kwa lengo la kupata mayai mengi kwa bahati hakuyakuta.

Mhe. Spika, hivi sasa umezuka mtindo kilichobakia inauzwa na minazi mtu kusubiri miezi mitatu kwa ajili ya kuangusha nazi na kuuza anaona anachelewa, sasa inakatwa minazi na kipande cha mnazi kinauzwa shilingi 6,000/- kwa lengo la kupasua mbao. Kwa kweli hili ni tatizo ambalo wenzetu wameliona na tayari wameshaanza kukagua hizi eka.

Kwa hivyo, swali langu lipo hapa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anipe jibu. Kwa mfano, zimekaguliwa eka na kugundulika kuna matatizo, je jambo gani la kuendelea wale waliofanya matatizo watanyang'anywa ama waliokuwa wameshauza watapewa nyengine? Mhe. Spika, naomba nipate jibu kwa ajili ya kufahamu mimi pamoja na wenzangu, kwa sababu dhamira zilizokusudiwa na Rais wetu wa mwanzo sasa zimetenguka watu wanafanya wanavyotaka na sheria zipo.

Nikiendelea na mchango wangu niende kwenye ukurasa wa 59 kuhusu upimaji wa mipaka ya mikoa na wilaya. Mhe. Spika, nishukuru sana kwa sababu hili tatizo ni la muda mrefu hasa baina ya Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi. Sasa kama limeonekana naomba hatua za haraka zichukuliwe, ili kuondosha matatizo yaliyopo. Lakini naamini kwamba sio Mkoa wa Mjini na Magharibi tu, nadhani matatizo hayo mikoa mingi yapo.

Vile vile chini ya hapo kifungu 110 kinazungumzia kuhusu udhibiti wa ujenzi kwa mijini na vijijini. Mhe. Spika, hapa pia kumezuka tatizo, hivi sasa ule utaratibu wote unaopangwa watu wanauvunja.

Kwa mfano, hapa imeelezwa kwamba watasimamia *ZIPA* pamoja na vitengo vyengine, kuhakikisha kanuni na sheria zilizopo zinafuatwa, ili watu wajenge kwa mujibu wa mpangilio. Nadhani ukipita kwenye mji wetu huu hivi sasa kuna mambo mengi ya ajabu yanatokezea.

Mhe. Spika, hivi juzi kwenye Baraza hili liliulizwa swali hapa *ZIPA* Amani pamejengwa maduka yanayofika manane nje ya ukuta wa *ZIPA*, Mhe. Waziri alijibu kwamba pale pamekubalika, kwa sababu hawamo ndani ya *ZIPA*. Lakini tuliacha nafasi ile kwa makusudi kwa ajili ya sehemu ya akiba na pakitokezea tatizo basi watu waweze kujihami, sasa leo pamejengwa maduka na tunaambiwa ni halali.

Kwa hivyo, ninashauri kwa kamati yenye kusimamia utaratibu wa ujenzi mijini na vijijini, basi waangalie kanuni pamoja na sheria kweli inakubalika kwa haya yanayofanywa hivi sasa. Kwa mfano, kujenga maduka kwenye eneo la *ZIPA*,

ambalo tumetenga kwa ajili ya wenzetu wanaotaka kuweka vitaga uchumi waje pale kwa lengo la kuwekeza, lakini tunajenga maduka.

Kwa maana hiyo, kuna mambo ambayo si mazuri kuyafanya na wala si hapo tu, isipokuwa yapo maeneo mengi na huo ni mfano mmoja ambao nimeutoa, ili tuweze kufahamu hayo.

Sasa nizungumzie kuhusu mradi wa maji kwa majimbo matatu, ambayo ni Mfenesini, Bumbwini na Kitope. Mhe. Spika, naipongeza serikali pamoja na wenzetu wa *ACRAA* kwa kutusaidia kuweka mradi huu ambao utaondosha kilio cha majimbo matatu katika suala zima la maji.

Ninashauri kwamba pale Mfenesini ndipo palipochimbwa visima vyote vitatu katika mradi huo. Lakini tulikuwa na tangi letu Michungwamili ambalo ni lazamani, kwa hivyo naomba na hili litengenezwe kwa lengo la kusaidia huu mradi, siku ya kupumzika mradi wetu wa *ACRAA* tukatumia mradi wetu wa zamani, kuna msemo unaosema “usiache mbachao kwa msala upitao”. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atusaidie ili kuweza kutumia na ule mradi wetu wa zamani.

Sehemu yangu ya mwisho katika mchango wangu nizungumzie kuhusu Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Kwanza niwapongeze Wakurugenzi pamoja na wataalamu wake wote wanaosimamia Mji Mkongwe.

Kwa kweli Mji wetu wa Uthiri wa Kimataifa tumepata sifa kwamba dunia nzima unatambulika, pia nimeona malengo yao waliyoweka kuwa bado tusitoke kwenye sifa hizo na mimi ninawashukuru kwa hayo.

Vile vile mji wetu unavutia wageni kwa mambo mengi na nitatoa mfano kwa mambo manne tu. Kwanza mji wetu unayo Ngome Kongwe ambayo ngome ile imejengwa kwa kitaalamu sana kwenye karne za muda mrefu nyuma, yaani imejengwa kwa jiwe, chokaa na dongo, ambapo hivi sasa ukimpa mtu tofali na saruji ajenge kama ile basi itamshinda, sasa ile ni moja ya kivutio cha wageni wetu.

Jambo la pili tunalo Soko la Watumwa katika Kanisa la Minara Miwili, pale ukienda unaelezwa kwamba watumwa walikuwa wakiuzwa na kununuliwa Afrika ya Mashariki nzima na mpaka leo kumbukumbu zile, kwa hiyo na kile ni kivutio.

Jengine ni nyumba zetu zilizojengwa katika mji ule, utakuta nyumba ya ghorofa hivi sasa unaweka jamvi ukimaliza jamvi ghorofa ya kwanza unafunga zege na kuendelea hivyo hivyo. Lakini zile za zamani walikuwa wakijengea

jiwe na kila wanapotoka hatua moja kwenda nyengine hawana zege isipokuwa ni botiri na kuweka dari na baadaye kupandisha juu, yaani ni utaalamu mkubwa sana.

Kwa kweli hivi sasa mtu akiamua ajenge nyumba ya ghorofa na kutumia boriti basi watu wengi watashindwa. Kwa hiyo, hiki ni kivutio ambacho kinachowafanya wenzetu waje.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni zuri zaidi kuhusu ile michoro ya milango. Kwa kweli milango mikubwa ya nje wameisanifu kwa ujuzi mkubwa sana, wakati hivi sasa ukimpa mtu kazi ile anaweza kuchukua mlango mmoja muda wa mwezi mzima kwa ajili ya kuutengeneza na kushindwa. Lakini wenzetu walikuwa wakitumia utaalamu na Mwenyezi Mungu aliwasaidia na mpaka leo historia ile ipo.

Jambo jengine ambalo limevutia katika mji wetu kumetengenezwa bustani moja nzuri sana ambayo inaleta haiba ya mji ule. Mhe. Spika, nimeona kwenye kitabu katika kujiandaa kuienzi bustani ile unajengwa ukuta kutokana na bandari yetu kuondoka ule mvungu imeonekana utaathiri mji kwa bandari ya tuta.

Sasa wameweka mradi kujenga ukuta wa kuzuia mji wetu usiathirike. Kwa hivyo, wanapongeza sana naomba waendelee, ili na sisi tusitoke kwenye Urithi wa Mji wa Kimataifa.

Mwisho kabisa nizungumzie kuhusu usambazaji wa mradi wa umeme kwenye ukurasa wa 78. Mhe. Spika, hapa nipongeze katika shehia zangu zote saba za Jimbo la Mfenesini tulikuwa tumeshapata umeme, lakini kuna kasoro kwenye Shehia moja ya Mbuzini katika vitongoji viwili kitongoji cha kwanza wanaita Mkanyageni na ya pili Mbuzini kuelekea Kitundu.

Nashukuru katika bajeti hii tumeonewa jicho la huruma na tumewekwa kwenye mradi wa kutia umeme sehemu zilizobakia. Mhe. Spika, nashauri tusaidiwe, ili na wenzetu waliomo kwenye shehia hizi na wao wagomboke, kwa sababu hivi sasa nyumba za ghorafa zinajengwa Mbuzini, yaani kuna ghorofa tayari imeshajengwa na watu wameshahamia, lakini kwa bahati mbaya wanawasha karabai na hayo ni mambo ya kizamani.

Vile vile wenzetu wa Halmashauri wamejenga hospitali pale yenye uwezo wa kulaza watu kiasi ya kumi na umeme haupo. Sasa na wao kuja kuwasha karabai itakuwa si vizuri, kwani hivi sasa hata vibua havivuliwi kwa karabai, watu wanachukua taa za *steam* wanawacha na kuvua vibua.

Kwa hivyo, naomba na eneo hili tufanyiwe haraka na kama kuna tatizo lolote basi tushirikiane kwa ajili ya kulitatua, ili wenzetu hawa wa vitongoji viwili vya Mkanyangeni na Mbuzini kuelekea Kitundu wapate umeme.

Mhe. Spika, mwisho kwa kumalizia nishukuru serikali kwa kuweza kutafuta mbadala wa nishati ya umeme na wala sio kutegemea tena Kidatu. Katika kitabu kwenye ukurasa wa 78 wameelezwa kwamba hivi sasa wao mpango wa kuzalisha umeme kwa njia ya upepo pamoja na mawimbi ya bahari. Utafiti huo unaendelea na naomba wajitahidi na Mwenyezi Mungu atatusaidia, ili tupate umeme wetu wa kujitegemea wenyewe.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja *(Makofi)*. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria katika kikao cha Baraza, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu.

Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011.

Kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianzie mchango wangu kwenye ukurasa 15 na 16 kuhusu mradi wa *TASAF*. Mhe. Spika, katika jimbo langu nilipata mradi huu na kwa bahati nzuri nimeshikiriana vizuri na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi katika kuhakikisha kwamba Mradi wa Kisiwa cha Maji Chaani Kubwa unafanikiwa.

Kwa kweli mradi huu tumekwenda nao vizuri, lakini namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba bado kuna haja ya kufanya juhudi za makusudi zichukuliwe, kwa sababu mradi huu wa muda mrefu tumeanza kuchimba kisima kwa hatua ya awali, kwa bahati mbaya kisima kile kimeonekana maji yake ni kidogo kwa hiyo tuliacha. Sasa tumeanza kuchimba kisima sehemu nyengine lakini mashine zimeharibika na hilo liko kwenye uwezo wa Mwenyezi Mungu na wala sio letu.

Hata hivyo, naomba juhudi zichukuliwe kuona kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati, hasa tukizingatia kwamba wananchi wamekuwa wakilalamika na kuona labda ule mradi unaendeshwa taratibu mno, ili kuona karibu ya uchaguzi ndio ukamilike. Kwa hivyo, suala hili kuna haja ya kulifanya kwa haraka, ili

kuondoa ile dhana ya watu ambao pengine kwa makusudi wahapendi lifanikiwe.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza wizara kama nilivyotangulia kusema kwamba, katika jimbo langu karibu shehia zote zimepata maji, tukiondoa Shehia ya Bandamaji. Kwa hivyo, nataka nimkumbushe Mhe. Waziri tulifanya ziara ya pamoja katika Skuli ya Bandamaji na aliwaahidi wananchi wa Bandamaji kwamba atatuchimbia kisima pale. Lakini bado wananchi wa pale wanadai hilo kwa Mhe. Waziri, kwa hivyo nataka kumkumbusha kwamba kuna deni hilo la kisima bado wananchi wanalidai.

Mhe. Spika, jengine ni mradi wa umeme vile vile naomba nipongeze sana Wizara pamoja na watendaji wote wa *ZESCO* kwa jinsi ambavyo wamejitahidi sana kuona kwamba mradi huu wa umeme na hasa hii *phase four* umeenea katika jimbo letu.

Mhe. Spika, naomba tu Mhe. Waziri pamoja na watendaji kwamba tayari tumeshafika katika afisi zao. Ndugu Hijja pale pamoja na Mkurugenzi na tumeeleza kwamba tuna vijiji vyetu vya Kidimni yaani shehiya ya Kinyasini, Ketwa shehia ya Chaani Masingini, Kirama ambayo iko shehia ya Moga lakini pia Shehia ya Chaani kubwa Jua Kuu hizi ni sehemu ambazo bado hazijafikiwa na huduma hiyo ya umeme na tumekuwa na tatizo katika kipindi hiki, hasa ukizingatia kwamba hivi sasa kuna hili kombe la Dunia wananchi wa maeneo hayo wanapata shida, mwengine tumepeleka TV lakini pia tulinunua janareta kwa sababu ya ukosefu wa umeme ili wenzetu waweze kuona haya mashindano ya Kombo la Dunia.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka nilizungumze na ningeomba sana wenzetu wa vyombo vya habari hili walitolee maelezo kama ambavyo nalieleza, mradi wa umeme na maji katika jimbo la Chaani ni mradi ambao umeteelezwa kwa nguvu kubwa sana na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Pale ambapo palilazimika sisi kama viongozi wa jimbo Mhe. Mbunge na Muwakilishi kuweza kusaidia maeneo ambayo yalikosekana baadhi ya vifaa tulijitahidi kuona kwamba vifaa hivi vinapatikana.

Sasa ninachotaka kukisema hapa ni kwamba kuna baadhi ya viongozi wamepita kwenye majimbo na kusema kwamba mradi huu umetekelezwa na baadhi ya viongozi bila ya kumtaja Mhe. Muwakilishi katika utekelezaji huu, kwa hivyo hii nataka nifute kauli hizi zinazowaptosha wananchi. Sisi kama viongozi wako wa Baraza lako tukfu na tunapenda tuishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na Rais wa Zanzibar Dk. Amani Karume kwamba

imekuwa sikivu na ikitufanyia kila ambacho tukikitaka katika serikali, sasa pale ambapo tunasimamia miradi akitokea mtu akiwapotosha maana yake ni kwamba hapotoshi viongozi waliopo madarakani tu lakini pia anapotosha viongozi wa Idara pamoja na Rais kwa jumla kwa sababu yale mambo hayatekelezi yeye kama anavyodai, sasa hili nilikuwa nataka wananchi walielewe na walisikie na kama kuna maelezo yoyote basi mimi niko tayari kujibu hoja kutokana na hilo.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka kulizungumza nataka na mimi nichukuwe nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Rais wa Zanzibar kutokana na miradi miwili mikubwa ya umeme, mradi wa kutoka Tanga/Pemba na ule mradi ambao wa Ras Kiromoni hadi Fumba. Juhudi za serikali tumeziona kwa hivyo naomba niwapongeze lakini pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwapongeza wenzetru wa Norway kwa jinsi ya msaada wao mkubwa ambao wameufanya katika nchi yetu na kuwa wao ni wadau katika maendeleoya nchi yetu.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ningeomba sana wizara hii kama kauli yao walivyoitoa kauli mbiu wakati Mhe. Waziri alipokuwa akitoa bajeti ya mwaka jana lakini alielezea kwamba kuna mradi ule wa kuuza nyumba za vijijini, mradi ule wa kuuza nyumba vijijini. Mradi ule wa kuuza nyumba vijijini ni mradi mmoja ambao mzuri na umetoa mwelekeo kwa wananchi wa maeneo wanayokaa. Sasa ningeomba sana ile nafasi iliyotolewa na Mhe. Waziri kwamba mtu ambae anaishi katika nyumba ile apewe umuhimu wa kwanza kuuziwa nyumba ile, kumekuwa na malalamiko baadhi ya maeneo kwamba kuna baadhi ya watu ambao walikuwa tayari wako katika nyumba aidha ni zile za vijiji au serikali tu kwamba yeye anaishi humo lakini baadae anatokea mtu mjanja anachukua nafasi ya kutaka kuchukua nyumba ile na kumtoa yule ambae aliyekuwemo, kitu ambacho kitatufanya wananchi wetu waone kwamba serikali yetu hawaifanyii haki.

Sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri najua ni msikivu ataliona hilo pale ambapo kuna mahitaji ya maelezo yoyote kutokana na hili nililolizungumza basi niko tayari kushirikiana nae kuona kwamba haki inapatikana. Kama alivyosema Mhe. Ali Hassan Mwinyi kwamba haki na wajibu ni watoto pacha kwa hivyo lazima masuala haya tuyazingatie.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda wako nataka nirudie kusema tu kwamba mimi binafsi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii fupi ya kuchangia Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, kwa sababu

ya maandiko mazuri ya kitabu yalivyo na kwa sababu tumeona utekelezaji kama alivyoeleza katika kipindi cha mwaka 2009/2010 na malengo yanayofuatilia kama kilivyowekwa na Idara ya Mipango na Fedha katika ukurasa wa sitini na nne mimi naona yote atasababisha nisizungumze chochote, labda ni kutaka ufafanuzi wa mambo madogo tu.

Lakini kabla ya hapo hapana budi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa dibaji yake aliyoitia katika kitabu chake kuhusu namna alivyoipa hazi hii kura ya maoni itakayofanywa atarehe 31/07/2010. Tunajua kuwa kura hii ilipitishwa tokea kwenye muwafaka kwa madhumuni ya kuwa wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi ni kutaka mabadiliko ya uendeshaji wa serikali katika nchi hii.

Lakini ikaja kuwa wananchi lazima waulizwe kuwa suala hili limo katika ridhaa yao au laa, kwa kuona Mhe. Waziri katia mkazo suala hili kwamba lifanikiwe mimi nipo pamoja na wewe na sisi Waheshimiwa tuliomo humu kwa sababu tumelipitisha kwa kauli moja tuwe ni wajumbe kwa wenzetu kuona lile lengo tulilokusudia limefanikiwa na *inshaalla l*ikifika baada ya uchaguzi Mkuu 2010 tuwe na serikali imara ya umoja wa kitaifa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka ufafanuzi tu baadhi ya mambo ni kuwa siku moja au siku mbili tofauti Mhe. Naibu Waziri alikwenda kule Pemba katika jimbo langu kuangalia matatizo ya maji kama nilivyokuwa nikilalamika hapa, siku moja alikwenda Bahanasa akangalia tangi ambalo limejengwa bahati mbaya likaanguka, alifika eneo la Kisiwani kuangalia matatizo ya maji yalivyo kama nilivyokuwa nikilalamika, nashukuru aliniahidi kwamba atafanya kazi nzuri na matatizo yale yataondoka. Lakini katika kutazama hiki kitabu ukurasa wa kumi na nne kifungu namba kumi na saba katika miradi mitatu ambayo haikutekelezwa mmoja ni huu mradi wa kuanzisha mradi wa maji mpya katika kijiji hiki cha Kisiwani.

Kwa hivyo nilitaka maelezo tu kuwa kazi hii imefeli kwa sababu fedha hazijaingizwa tu au kuna sababu zozote nyengine hasa kwa kuwa katika sehemu hii watu wana shida kubwa sana ya maji, pale baada ya kuanguka lile tangi maji yanapatikana kwa shida na kule ndio maji hakuna hasa. Kwa kuwa alikwenda na kuniahidi nikitaka kupata maelezo zaidi hilo ni moja.

Mhe. Spika, hili jengine ni lalamiko tunapokuwa hapa huwa tunapeleka maombi yetu kwa Mhe. Waziri na Mhe. Waziri huwa anatuahidi vizuri tu na analoliamua yeye mwenyewe hapa hapana budi akifika kule hutekelezwa hilo nashukuru sana, hata juzi tu aliniahidi katika matatizo ya maji niliyonayo Mtambwe Kaskazini atanisaidia vijiji viwili na nashukuru vijiji vile yaani Nyali

na Mpakanjia mpaka hivi sasa tunapata maji vizuri na wananchi wanapunguza kuteremka milima mikubwa kufuatia maji usiku wa manane.

Lakini kuna mambo mengine tunapiga kelele kwa sababu ya umeme na hutoa maagizo mazuri tu kwa njia ya simu na sisi huwa tunasikia na kushuhudia, sasa tunapofika Pemba yale mambo huwa yanabadilika kwa hivyo inakuwa sisi tukipata kauli kotoka hapa kule tunawaeleza wananchi wetu kuwa tulifika na tumeahidiwa hivi na hivi. Lakini jambo lolote la umeme likipelekwa kule Pemba utekelezaji wake huwa ni tofauti na vile tulivyoondokea mfano.

Mhe. Waziri kama anakumbuka siku moja tulikuwepo hapo na akapiga simu kuwa nakuomba mumpelekee Mhe.Salim Abdalla Hamad umeme Machengwe lakini tokea siku hiyo hatukupata chochote mpaka hivi sasa watu kwa kujikusanya na kuchanga changa kusaidiana wamepata nguzo kumi katika nguzo kumi na nne za kununua wenyewe, wamekwenda katika shirika mpaka hivi sasa hawajafanyiwa chochote walichoambiwa shirikianeni na Mbunge na Mwakilshi wafanye hii kazi.

Sasa sisi tumechaguliwa na jimbo zima na kuna vijiji kadhaa havijapata hii huduma, unafikiri vijiji vingine vikisikia kwamba Mwakilishi na Mbunge wanafanya kitu kadhaa wakati kuna vijiji vingine havijafanyiwa na gharama zao ni kubwa hatuziwezi, hiyo itakuwa ni fitina kwa makusudi kwa sababu wananchi wangu wa Machengwe wameshajitahidi kununua zile nguzo kumi na walivyonambia kila nguzo ni shilingi laki moja na thalathini. Namuomba Mhe. Spika, anipe uhakika wa hizi nguzo zilizobakia pamoja na vifaa vyengine vinapatikana na wale wananchi waondokane na shida ile ya kutokuwa na umeme.

Mhe. Spika, juzi hapa tulipokuwa tukichangia katika Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ uongozi wa Mkoa wa Kaskazini uliandika kuwa kwa kushirikiana na wizara husika, wameeneza maji na umeme katika vijiji vyote vilioko katika Mtwambwe Kusini na mimi nilisimama sikukubaliana nayo taarifa ile lakini kwa sababu imeandikwa na kwa kuwa kuna mashirikiano nahofia ikawa taarifa ile ikaonekana kuwa ni ya kweli.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aone kuwa taarifa hii haikuwa kama ilivyoelezwa na ilivyo sahihi ni hivi, taarifa ilisema kuwa kijiji cha Mkanjuni kuna umeme na maji pale pana maji tu umeme hapana, taarifa ilisema kuwa kijijiji cha Minazini na Mitambuni kuna umeme na maji, kule hakuna umeme wala maji. Taarifa ilisema kuwa kijiji cha Kivumuni kina umeme na maji kule kuna maji tu hakuna umeme, na taarifa ilisema kuwa kijiji cha Makoongeni kuna umeme na maji pale pana umeme tu hapana maji.

Mhe. Spika, ichukuliwe hii ndio taarifa rasmi ili tutakapowatetea wananchi na kwa sababu katika ukurasa wa ishirini na nne umeelezwa kuwa mambo haya yataendelea kusambazwa kwa zile sehemu zilizobakia, ionekane kwamba taarifa hii ndio rasmi isije ikaonekana kwamba hawa watu wameshapata wakakoseshwa haki yao. Pamoja na hayo nimejitahidi sana kuomba angalau tufikishiwe maji pale Makongeni na wakati mtandao wa maji umeshafika Kivumoni ni sehemu ya kuunganisha tu ndogo, Kwale pana skuli, Kwale pana Kituo cha Afya ni kijiji kikubwa na hivi sasa mpaka kumeshajengwa nyumba kubwa ya daktari, kwa hivyo naomba kwa maslahi ya wananchi wa pale kutokana na hizo taasisi nilizozitaja nisaidiwe pale Makoongeni kwanza papatikane maji kwa haraka halafu tena tutategemea uwezo wa serikali tuweze kuendelea katika hizo sehemu nyengine.

Mhe. Spika, kwa kuendelea Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ina kazi kubwa na moja niliyozungumza hapa ni kufanya uhakiki wa eka tatu tatu ninapozungumza ni kwamba eka hizi tatu ziligaiwa kwa nia njema kabisa na Rais wa awamu ya kwanza Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi ili wananchi wafaidike, wakati ule idadi ya watu ilikuwa hata laki nne haifiki kwa hivyo ardhi yetu hii hii ambayo imeshapungua sasa hivi kwa sababu kadhaa ilikuwa na watu kidogo kuliko hivi sasa, ambayo idadi haipungui milioni moja laki mbili na kidogo.

Sasa hivi kuna mashamba hayashughulikiwi kuna mashamba watu wanarithiana kama yao, kuna na mashamba masheha wanakodisha kama yao, mimi ningeliomba uhakiki huu wa mashamba uendelee lakini pia serikali itilie maanani ongezeko la watu ardhi ndogo tuliyokuwa nayo kwa yale ambayo hayamo katika umiliki wa watu kwa hivi sasa, serikali kama kuna njia ya kuangalia kwa namna tunavyoongezeka itafute njia bora ya matumizi kwa maslahi yetu sote. Kuliko kuwapa watu eka tatu waliokuwa hawazitumii na wakati tumeshaongezeka na kilimo ndio uti wa mgongo wetu , ikawa badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma kwa sababu ya hizi eka tatu. Sasa kama kutakuwa na mpango mwengine maalum wa kiserikali wa kutumia hizi eka tatu tukafaidika sote ingelikuwa bora kwa zile ambazo hazimo katika kukabidhi watu.

Mhe. Spika, jengine ninaloomba kuzungumza ni kuwa kuna mradi huu wa Mtambwe Kaskazini wa maji na nashukuru Mhe. Waziri japokuwa hakuutembelea anaujua vizuri sana, kutokana na kuwa na watu wengi vijiji tofauti vimetapanyika alisema haiwezekani kupeleka kwa mara moja lakini tutakwenda hatua kwa hatua. Sasa vile vijiji viwili kama alivyozungumza mwanzo viko tayari ningekuomba tuende hiyo hatua kwa hatua kwa vile vijiji vilivyobakia. Kwa hivyo ombi langu kutokana na ule mtandao ulivyo

ingelikuwa ni zamu ya kila pahala na baadae kuendelea na kwengine, tusikwamishe lakini iwe endelevu.

Halafu la mwisho Mhe. Spika, ninaloomba kuzungumza ni kuwa mimi narudia tena nimestuka sana na nimeshavunjika moyo na navunjika moyo kweli kweli kwa sababu mimi nilifikiria kuwa hili ni Baraza la Wawakilishi mswada utakapotoka Baraza la Mapinduzi ukapita hapa ukapitishwa kwa kauli moja huwa tena hakuna kikwazo. Tukitaka tusitake kwa idadi ya watu ilivyo hatuna ardhi ya kilimo ya kuweza kutusaidia, wala hakuna njia ya kupata umeme wa kuweza kutegemea isipokuwa kama Mwenyezi Mungu atatujaalia tutapata mafuta yetu wenyewe.

Kazi tuliyofanya ni kubwa na tukaipitisha hapa tena kwa kauli moja mimi nilifikiria kuwa serikali iliyobakia ni kuelekeza tu serikali ya Muungano kuwa Baraza la Wawakilishi wamepitisha suala hili na hili kwa hivyo serikali ya muungano iliondoe moja kwa moja lakini ukisema kuna kuomba na ukisema kuna kitu kuomba maana yake ni kwamba kile kitu sio haki yetu, kwa hivyo *statement* imepelekwa kwa Waziri Mkuu lakini kiutendaji inaturudisha nyuma kweli kweli. Tukija tukifeli hapa Mhe. Spika, ni ufukara wa milele.

Kwa hivyo ushauri wangu patafutwe kila namna lakini kwa vyovyote ilivyo suala hili kwa sababu liliingizwa kwenye orodha ya Muungano kinyemela, hata wanasiasa wakongwe walioko bara walisaidia kufafanua hilo tuone kuwa halina mzozo kwenda kule lijadiliwe halafu tena tupewe jibu, hasa niliogopa juzi Mheshimiwa mmoja alipokuwa akitoa majumuisho kule kuzungumza kwamba katika mambo ambayo tutajadili katika bunge ni ugawaji wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia nilishtuka sana, kumbe wenzetu hawako hasa kuwa sisi tumeshapitisha.

Kwa hivyo tumefika pahala pazuri ila tuongeze gia nzito kuona kuwa haturudi nyuma na wala hili sio suala la kubembeleza kwa wenzetu hii ni rasilimali yetu, kwa sababu wao wameshaanza hawakutushauri tuone na sisi kwa vyovyote itakavyokuwa rasilimali hii tusiichezee Mhe. Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kupata nafasi hii kuzungumza machache katika bajeti hii. Mwanzo ningependa kuchukua nafasi kumshukuru sana Waziri kwa hotuba yake hii nzuri, hotuba ambayo imeeleza kinaga ubaga nini yamefanyika katika Wizara lakini vile vile ni yenye matumaini kwa mambo ya baadae.

Mhe. Spika, basi nianze kwa Mamlaka ya Maji napenda nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji hasa Mkurugenzi wa maji, nilikuwa na matatizo sana katika jimbo langu wananchi wa sehemu ya jimbo la Chambani walikosa

maji kwa kipindi kikubwa sana, kutokana na uharibifu wa hii pampu ya maji. Lakini kwa mashirikiano makubwa sana na Mkurugenzi ingawa alikuwa ni msaidizi wake kwa wakati ule kwa sababu Mkurugenzi alikuwa hayupo alikwenda hija, lakini nashukuru sana nilipata mashirikiano makubwa sana kutoka kwa mtu ambae alikuwa akimkaimu pamoja na Ndugu Mshindo wa Pemba na tatizo lile likaondoka kwa muda mdogo sana, tokea siku hiyo wananchi wanashukuru sana kwa upatikanaji wa maji.

Tatizo lililokuwepo katika shehia ya Chambani ni *pressure* ya maji ambalo hili nimekuwa nikiliripoti sana kwamba yanapofunguliwa maji sehemu moja ya shehia kwa sababu ya umbile ya ile sehemu ni kwamba kuna minyanyuko, sehemu moja inakuwa haipati maji sehemu ya kijiji cha Tumbini ni matumaini yangu kuwa suala hilo kwa kuwa nimekuwa nikilisema sana na bado wananchi wanaliripoti basi Wizara itachukua hatua ili kuliondosha tatizo hili.

Mhe. Spika, katika shehia ya Ukutini kulikuwa na tatizo moja kubwa sana la kisima ambacho kilikuwa kimekauka kabisa namshukuru sana Mkurugenzi kwa namna ambavyo tulishirikiana na kikapatikana kisima chengine, hatukuzungumza mimi na yeye kwenye afisi yake tu lakini tuliwahi kuyazungumza masuala haya kupitia kwenye kamati ambazo tulikuwa tunatembelea afisini kwake na kikapatikana kisima. Ingawa baadae kulizuka mzozo kidogo lakini maji yanapatikana, mzozo wenyewe ulikuwa ni namna ambavyo kimepatikana kisima.

Mkurugenzi wakati tukitembelea na kamati atakumbuka nilimuuliza suala kwamba kisima hiki ambacho kitachimbwa Ukutini kitagharimiwa na nani, Mkurugenzi akanambia kitagharimiwa na mamlaka yenyewe lakini wakati kisima kinachimbwa mara nilipokwenda jimboni nikaambiwa Mwakilishi, Mbunge hapa ameshatoa milioni moja na wewe tunataka milioni moja ya kisima mimi nikasema mchango wangu ni kukifanya hiki kisima kichimbwe na serikali kwa kauli ambayo tumekwisha kuzungumza ndani ya Baraza na ndani ya kamati pamoja na Mkurugenzi, lakini ikiwa Mbunge katoa milioni hii basi ibakie katika *account* kikiharibika au matengenezo madogo madogo yatafanyika.

Nilichokuwa nikitaka kusema tu hapa ni namna ambavyo wananchi kama alivyosema Mheshimiwa hapa wanavyoyapokea vibaya haya masuala ya maendeleo katika majimbo, mara nyingine wanafikiria kwamba Wawakilishi na Wabunge watakuja hapa watoe pesa mifukoni mwao ndio maendeleo yatapatikana, wanasahau kwamba kuna majukumu ambayo wametupa na tumeyaona ndani ya katiba na tukaapa na katiba ya kwamba tutawatetea wananchi ili serikali tuiharakishe na tuisaidie tuikosoe na tuiseme panapohitaji kusema ili serikali itoe maendeleo.

Nadhani kifungu cha katiba kinasema hivyo hivyo kwamba serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio yenye wajibu wa kuwafanyia watu maendeleo katika nchi hii, kwa hivyo ninachotaka niseme tu wananchi yanapotokea mambo yakawa tumeshayapigania na yakatokea katika majimbo isionekane kwamba kila kitakachofanyika katika jimbo kinahitaji mchango wa fedha, lakini mchango na msukumo wa maneno ambayo tunakuwa tunayazungumza na serikali kwa sababu inapanga bajeti na tunaipitisha basi ndio *source* kubwa lakini hatukarai mashirikiano na wananchi ni jambo ambalo vile vile tunalihimiza.

Mhe. Spika, labda tatizo ambalo bado nimebakia nalo ni sehemu ya Jambangome na siku zote naizungumzia hiyo, Jambangome ni sehemu ambayo ina mnyanyuko mkubwa, nimeona katika kitabu kuna huu mradi wa usambazaji wa maji safi wa mazingira ambao katika kijiji cha Mizingani ambacho kiko Chambani kimebahatika, lazima hapa nishukuru lakini vile vile Mizingani iko karibu sana na jambangome na kwa kweli ni mnyanyuko ulio mkubwa na Mzingani.Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri aiangalie shemu hii ya Mizingani na Jambangome ili ifaidike na mradi huu.

Mhe. Spika, tuna tatizo kubwa bado tena kubwa sana la maji katika kijiji cha Kuyuni na Ngezi sehemu hii sio maji tu lakini hata umeme na umeme takribani katika jimbo langu nishukuru kwamba umefika sehemu nyingi sana, lakini inanisikitisha kwamba Ngezi na Kuyuni ni barabara kuu sasa ukifika pahala barabara kuu hapana umeme lakini vijijini upo mpaka Makaani, lakini pale barabara ile tu kwa sababu panapita magari lakini hakuna maji wala umeme suala hili linasikitisha sana, tumelizungumza kwa muda mkubwa sana. Naiomba tena Wizara itupie macho katika sehemu hii ili tuone kwamba basi napo panakumbukwa na tatizo hili liondoke.

Mhe. Spika, sasa nizungumze kwenye Idara ya Majenzi, Idara ya Nyumba pamoja na maendeleo ya makaazi na Idara ya Upimaji suala ambalo hapa nilitaka nilikumbushe kwa sababu nimelizungumza sana ni kwamba serikali ilifanya juhudi kubwa sana ya kugawa viwanja vya makaazi, viwanja vizuri na vikubwa na umeme watu wamepelekewa na mara nyengine zamani kabla simu za mkononi hazijaingia walikuwa simu wanapelekewa. Lakini tatizo la barabara zinazopita katika viwanja vile ni kubwa mno, mimi nimekuwa nikijiuliza suala hili limekuwa la Wizara hii ni suala la Mawasiliano au suala la Halmashauri ya Wilaya, ilimradi maana yake kama umeshona suruali ya suti lakini haikutimia ukweli unakuwa bado hujawa mahiri na ndio matatizo tuliyokuwa nayo humo vijijini.

Mhe. Spika, ukienda Mpendae nyumba nzuri zimejengwa safi kabisa ukenda kwa Mhe. Suleiman Othman Nyanga unapita lakini kuingia na gari ukasema

unakwenda kwa Mhe. Suleiman Othman Nyanga basi lazima kwanza utakata shokomzoba zote za magari, hii ni kusema kwamba ili makaazi haya yawe mazuri na lengo ambalo limepangwa lipatikane vizuri basi suala la kupitisha njia katika mwahala ambamo viwanja hivi vimekatwa na watu wanajenga liwe la kipaumbele kabisa. Sasa hili ni tatizo na sio kwamba hamna barabara hamna njia za kupitia lakini kuna mabwawa sasa ya maji machafu. Unaona mahala ambapo pamekatwa viwanja vizuri ndio penye makaazi mazuri lakini huwezi kupita kuna mabwawa kuna matope kiasi ambacho huwezi ku-*communicate* nyumba nyengine na nyumba nyengine. Hili ni tatizo na Mheshimiwa lazima wizara zinazohusika au kama ni Halmashauri lazima suala hili lichukuliwe kuwa la msingi na lirekebishwe haraka sana iwezekanavyo.

Mhe. Spika, katika hifadhi ya Mji Mkongwe tunashukuru sana kupata Forodhani mpya zamani ilikuwa ni Foro iliyokuwa haiko sawa sawa, lakini leo imekuwa ni nzuri. Tatizo linalojitokeza pale ni kwamba tunawauliza hawa wauzaji zamani tulikuwa tunakuja hapa mtu na shilingi 1000 au 2000 anakula chimsi anashiba, lakini leo hata ile badiya mtu hununui kwa nini? Wanasema tunapandisha bei kwa sababu ya malipo mengi ambayotunakuwa tunalipa hapa. Sijui ni kiasi gani lakini nilitaka niseme hilo kwa sababu ni jambo zulimefanywa na jambo hili lifanywe ili likusudie kuwasaidia watu kuliko kulenga kwamba kuna wazungu watakuja au kuna wageni watakuja Forodhani ni vyema kama kuna malipo makubwa ambayo wanapewa hawa wanaotoa huduma pale basi yapunguzwe ili watu waweze kwenda pale na kufaidika na huduma ile.

Sambamba na sehemu ile, Mhe. Spika, Pemba tuna miji karibu mine na hapa tunayo Mikoa haingekuwa busara ya kwamba watu wote wa Zanzibar watoke Pemba, watoke Makunduchi tuje Forodhani pale na watu wote waliokuwepo huko nao wanapenda wapate huduma nzuri. Hebu niiyombe Wizara basi katika kupanga kwake mambo ya viwanja basi itenge sehemu zilizo muhimu sana za burdani kwa watu angalau hakuna jambo la kufanya ili ikifika jioni watu wanakwenda na watoto wao pahala wanakwenda kupumzika na kurejea sehemu hizi za miji.

Zamani Mhe. Spika, ilikuwa ukienda miji unaona kwamba kuna sehemu angalau ikifika jioni unakwenda wapi kupumzika siku hizi hakuna tena mambo ya snema. Lakini bado kuna haja ya watu kujumuika pamoja angalau kusalimiana. Hakuna jengine la kufanya isipokuwa ni mwahala kama humo mwa mikusanyiko. Mhe. Spika niliomba sana badala ya Forodhani kuwa ndio sehemu pekee ambayo inatajikana basi ndani ya miji humu muwe na sehemu kama zile ambapo watu hawa ambao wanajitolewa kupata riski na wengine wanataka angalau kujitafunia tafunia jioni basi wapate mahala mwa kwenda na kupumzika.

Leo ukenda Chakechake usiku nadhani hata wanaotoka hapa wanaokwenda kule kwa kazi unazunguka kila pahala labda uje kituo cha mafuta hapa kuna akina mama wanauza ngizi na mikate. Mwahala kama mle kungekuwa kumetengwa ikawa wanajua wanakusanyika jioni na mwahala muzuri basi kwa kweli ingekuwa ni sehemu moja katika mambo yanayowafurahisha watu katika maisha yao.

Mhe. Spika, tatizo la Mamlaka ya Mji Mkongwe. Ni t atizo ambalo sisi wengine tunaliona kwamba tunauhuisha Mji Mkongwe kupata misaada lakini tunauhesabu kama ndio sehemu yetu ya mji hatuna pahala pengine pa kuwaonesha watu ndio mji. Kwa hivyo kama tuna *preserve* Mji Mkongwe uwe ni mji wa kihistoria basi ni lazima mji huu usafi wake uzidishwe sana. Hakuna mtu atakayekuja kutizama historia katika mji ambao hauko katika hali nzuri. Majengo hujui wakati gani litaanguka likuangukie, kuna lile limewekewa mwega, kuna lile sijui limefungwa.

Mhe. Spika, juhusi zifanywe uwe ni mji ulio safi. Mwahala mwengine tunakwenda katika miji wanashindana kwa usafi wa mji. Kama mji huo ni wa kihistoria ya Kimataifa lazima *forcus* uwe ni kuuweka safi mji huo. Kuhakikisha kwamba majumba hata kama tunataka yabakie hayo hayo *structure* zake lakini yawe yanapata matengenezo na kuhakikisha baada ya kipindi yanapigwa rangi na kuona kwamba watu wa pale wanahamasishwa kuweka usafi. Katika hali ya sasa hivi bado kuna haja ya kujirekebisha zaidi ili kuuweka mji wetu katika hali iliyo safi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni suala la umeme na mimi nichukue nafasi sana kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Karume kwa jitihada yake ya kuona kwamba sasa Pemba kuna umeme wa uhakika. Tunaseme sisi ni ukombozi mkubwa pamoja na jitihada za watu za kufuta umasikini umeme ulirejesha watu nyuma. Mara nyengine nakumbuka Shekhe Ali Hassan Mwinyi wakati ule aliwahi kusema Ikulu Dar-es-Salaam na alitwambia sisi Wapemba *specific* akasema "Ndugu zangu Wapemba nawaomba mrejee mkafanye maendeleo kwa sababu ng'ombe akivunjika guu hukimbilia zizini"

Hadithi hii aliyoitoa ulikuwa ni ujembe ambao wengine tulikuwa tukimtazama *live* alikuwa anahimiza watu kurejea katika makaazi na kufanya *investment* tatizo la wakati ule sababu ilikuwa ni umeme tu. Kwa hivyo mimi napenda nizungumze na wenzangu sasa wale ambao wamekwenda Dar-es-Salaam, wamekwenda Mwanza na sehemu mbali mbali, wamefanya *investment* nyingi sana ili kuisaidia jamii ya pale ambapo wanatoka sasa hivi jitihada zao wagawe basi nyenzo zao. Waje pale wafanye *investment* ili ile sehemu nayo iyonekane ni sehemu ya kukalika, ni sehemu ya kufikiwa na watu na sehemu ya kutajika.

Vyenginevyo tukiachia tu kwamba umeme umekuja kutoka Tanga lakini hautumiwi kwa kweli itakuwa ni mapungufu makubwa ya kimaendeleo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumwambia Mhe. Waziri kwamba gharama hizi za umeme ambazo tumeziona ni kubwa na itakapokuwa distribution ya Pemba wataachiwa watu umeme ule utabakia pale pale ulipofikia tu hautosambaa na hautotumiwa. Mamlaka ya kusambaza umeme sasa hivi yawe ni mikononi mwa wizara na watu wabebeshwe ule mzigo wa kulipia kwa ajili ya matumizi yao tu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. Naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii iliyopo mezani kwako.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza niyapongeze mawizara yote kwa muda wa kipindi hiki cha miaka mitano tuliyomaliza na kwa kuwa mwanzo nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Kutekeleza ahadi za serikali kwa hivyo niliwahi kutembelea wizara nyingi na nikaona juhudi zao jinsi wanavyofanya.

Mhe. Spika, kwa kweli la ukweli husemwa Wizara ya Biashara imejitahidi vya kutosha kuboresha mambo ya biashara kwani kila aina biashara ipo Unguja isipokuwa bei tu ndio juu kidogo. Suala la biashara kupeleka nje sasa hivi kutoka Zanzibar kwenda Bara imekuwa hakuna kulipa uchuru kwa hivyo ni manufaa katika Wizara hiyo.

Ukija Wizara ya Wanawake na Watoto Wizara ya Utawala Bora mambo mazuri tu, ukija Wizara ya Mhe. Waziri Kiongozi katika ulinzi Alhamdulillah tumefika hatua nzuri na ukija katika mambo ya maafa hakuna aliyekuwa hakupata msaada wa maafa, wachache wote wamepata na waliokuwa hawakupata wanarekebishiwa. Nije katika wizara niliyopangiwa sasa hivi Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, nazipongeza wizara hizi kwa kuwa nimezitembelea kwa kina na kuona juhudi zao za kazi wanazofanya ukija Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ukija bandarini mambo yanakwenda vizuri tumepata mpaka vifaa vipya.

Ukija ujenzi wa njia barabara hata juzi tumepata magari ya vifusi vya kutosha kwa hivyo wanajitahidi vya kutosha na kutandika barabara. Uwanja wa ndege sasa hivi ndege zinatua kwa muruwa kwa barabara zilivyojengwa na ukuta ulivyozungushwa. Ukija Mamlaka ya maji tunaona wenyewe kwa macho yetu makampuni ya CONOICE , ACRA jinsi inavyotandika mabomba ya maji na juhudi za watendaji wao.

Mhe. Spika nawashukuru watendaji wote wa Mawizara haya kwa juhudi kubwa walizochukua kwa kipindi hichi cha miaka mitano. Kukamilisha ahadi za Chama cha Mapinduzi na kutekeleza ilani ya Chama hicho.

Mhe. Spika, nije katika mchango ukurasa wa 6 kifungu cha 12 uendeshaji wa kazi za utumishi. Imezungumzwa hapa wafanyakazi 44 wamestaafu kazi baada ya kufikia umri. Wafanyakazi watano (5) wamestaafu kwa hiari na wawili kufikia muda (2). Kwa hivyo hawapungui wafanyakazi kama 60 ambao wamestaafu lakini walioajiriwa hatukuona hapa. Ninachoomba hapa wakistaafu 60 basi walioajiriwa basi wawe robo au japo nusu ya robo. Kama hawa wastaafu sio wastaafu hewa basi na walioajiriwa waonekane ni wangapi.

Mhe. Spika, nije katika mfanyakazi mmoja amefukubwa kazi kwa ukosefu wa nidhamu mwaka 2009/2010. Kwa kweli baadhi ya watendaji wetu kwenye Idara au Vitengo mbali mbali wengine huwa wanafanyakazi kwa kudeka na wanakuwa hawana nidhamu ya kazi. Kwa hivyo ikiwepo dawa hii ya kuwa aliyekuwa mzembe hawajibiki kusimamishwa kazi hii itakuwa changamoto kwa wafanyakazi wetu kufanyakazi kwa uwadilifu na kwa nguvu zao zote. Kwa hivyo hii Wizara naipongeza kwa juhudi yao iliyochukua. Lakini atakapokuja anifahamishe kwa kipindi cha miaka mitano wangapi walikuwa wazembe na walikuwa wakosefu wa nidhamu wameachishwa kazi, isiwe huyu mmoja tu katika Idara zake ambazo zipo chungumzima.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 9 kifungu cha 14, mafunzo kwa wafanyakazi. Wizara imefanikiwa kuwapeleka masomo ya muda mrefu wafanyakazi wasiopungua 57 na wengine 18 wa muda mfupi. Ninachotaka kusema hawa wafanyakazi wanapelekwa kusoma kwa fedha za wananchi kwa hivyo zaidi ya wafanyakazi 70 wamepelekwa masomoni na kurudi wafanyakazi hawa waajiriwe kwa maslahi ya wananchi. Leo kuwa mfanyakazi huyu anarudi anakwenda kufanya kazi zake binafsi au anaajiriwa sehemu zake nyengine mbali na serikali kwa kweli hapa itakuwa tumeipoteza fedha za umma.

Ninachotaka kusema wadhibitiwe wafanyakazi hao wakati wametumia fedha ya umma basi warejeshe fedha ya watu au watafutiwe kitu cha dhamana ili fedha hii isipotee kiholeta. Maake haiwezekani tunasomesha wanafunzi zaidi ya 70 halafu tunakuja kuwapata watatu au 10 hii inatia ufukara nchi yetu.
Nije katika ukurasa wa 11 kifungu cha 17 Mamlaka ya Maji. Hii kwa kweli imejitahidi vya kutosha, kuwepo kwa maji safi ndio chombo cha kupunguza umasikini. Maji yanasaidia katika uboresho mbali mbali na utendaji wa kazi mbali mbali kama ilivyoelezwa humu. Watu wenye miradi yao ya kulima, kupiga matofali, miradi mbali mbali inafanikisha. Hili nitaomba uwe muangalizi sana kwa sababu kunaleta upungufu kwa mama zetu wanahangaika

kutafuta maji. Akina mama wazuri lakini wanaharibika nywele zao wanakuwa vipara kwa utafutaji wa maji ya kuokota visimani au katika sehemu mbali zilizokuwa hazihusiki. Ningeomba hapa wapaangalie sana watu wa maji kwa kuwa maji tunayo basi wayafungue na wayasambaze kwa mujibu wa utaratibu.

Mapungufu ya maji tunaambiwa kuwa visiwa vya Unguja vinaelea kwa maji. Kwa hivyo kwa kuwa kuna maelezo hayo ningeomba wataalamu wetu wa maji waangalie sana kuboresha vitengo vyao ili maji yetu yawe ya kutosha, angalau kupungua ule mgao wa maji.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 31 kifungu cha 56 Idara ya Nishati na madini. Niwapongeze kwa kutoa kibali kwa *deport* mbali mbali za Unguja ambazo ni Mtoni, Bumbwini kwa juhudi yao kubwa wanayochukua huyu Mkurugenzi wa Nishati kwa kuwapokea wawekezaji hao na kuwekeza vitega uchumi vyao ili kuongeza mapato ya Serikali. Tulitembelea katika Kamati yetu na tukaiyona juhudi yao wanavyofanya Ni jambo la maana sana kufanikisha masuala haya.

Mhe. Spika, Nishati ya Umeme wa jua taaluma itolewa zaidi kwa wananchi, vyombo vya redio, televisheni na kadhalika. Kwa kuwa nishati hii ikitolewa taaluma zaidi itapunguza uharibifu wa miti yetu. Kuna utumiaji wa gesi kuna utumiaji wa nyenzo mbali mbali za umeme ili kupunguza uharibifu wa msitu wetu. Ningeomba hapa wawe makini sana na kuliharakisha suala hili ili lifanikiwe kwa wananchi wetu.

Shirika la Umeme ukurasa wa 35 kifungu cha 64. Mhe. Spika, juu ya kupata mitihani ya kuzimika umeme isiwe tena zinakuja bei zilizokuwa sio kwa bili za kawaida. Baada ya kukosa umeme kwa kipindi kirefu muda wa miezi mitatu tulikuwa tuna mitihani mikubwa, taasisi zetu nyingi zilikosa kufanya kazi, watu binafsi ajira zao nyingi walizikosa. Ninachokiomba baada ya kurejea umeme watendaji wa Idara ya Umeme wawe waangalifu sana katika kufanya mahesabu ya unit wanazotumia wananchi, kusiwe na ubabaifu au ongezeko ambali lililokuwa halina mpango katika bei za kulipia umeme.

Hili uliangalie sana kwani baadhi ya wananchi wanalalamika bili hawazifahamu, zimeingizwa bili ambazo sizo walizokuwa wakitumia mwanzo. Kwa hivyo ningewaomba wafanye marekebisho hayo ili pasitokee usumbufu kwa wananchi wetu. Mita za TUKUZA kama inavyotangazwa kwa kila siku kuwa kuna mpango wa kuweka mita za TUKUZA katika miji yetu. Ninachomuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kwa sababu tumeshazungumza muda mrefu kuhusu kuweka mita za TUKUZA ili kuwapunguzia kero wananchi, utakuta katika maeneo yangu bado mita za TUKUZA hazijawekwa, hususan maeneo ya Sebleni na Kilimahewa. Ningemuomba katika usambazaji huu akaliangalia katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, vile vile namuomba Mhe. Waziri na kumkumbusha tena tulipokuwa katika Kamati Pemba alizungumza kuna makero mbali mbali ya viongozi wake wa Kamati yake yatatuliwe. Kwa hivyo namshukuru Mkurugenzi wa maji kazi hiyo tayari keshaiyanza katika shehia yangu ya sebleni kuifanyia ufumbuzi ile iliyokuwa kero kubwa la maji katika eneo lile kuyatafutia ufumbuzi na yale maeneo mengine atayafanyia ukarabati kabla Julai 10. Nashukuru watendaji wake wameshaanza kazi hiyo sawa sawa na watendaji wa Shirika la Umeme.

Katika maeneo yangu ya Jimbo la Amani kuna baadhi ya sehemu nyingi nguzo zake mbovu, kwa ushahidi tosha juzi amekuja mratibu mmoja kwa kuangalia nguzo mbovu kutoka Wizara ya Umeme kwa hivyo nategemea na suala hili nalo watalifanyia kazi kabla ya kipindi hicho kilichokuwa kimepangwa. Nawapongeza watendaji hawa wa Shirika la Umeme na Maji kwa kutaka kulifanya suala hilo kabla wakati wa mbele haujafikia.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na kuwapongeza watendaji wote wa Wizara zote kwa kipindi hichi cha miaka mitano jinsi ya utendaji wao walivyofanya katika mawizara yao hususan Wizara hizi zilizokuwa katika Kamati yangu kwa kufanya kazi vizuri na ushahidi nimeyaona kwa macho yangu. Kwa hivyo namuomba Waziri wa Fedha anayehusika na bajeti awape bajeti yao mapema ili kupata kumaliza shughuli zao na kutekeleza majukumu yote waliyokabishiwa kwa wananchi wetu.
Ahsante Mhe. Spika mimi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Amani naiyunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa tukiwa wazima. Lakini pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mchangiaji wa bajeti hii.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na watendaji wake wote Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wakurugenzi wake pamoja na wafanyakazi wake wote kwa kuandaa hotuba hii ambayo imeandikwa kwa ufasaha na utaalamu mkubwa.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kutoa pongezi maalum nimwendee Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Amani Karume kwa kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 100. Nimpongeze tena kwa kuleta maendeleo katika nchi yetu hasa katika sekta muhimu.

Mhe. Spika, zamani ilikuwa kama unataka kwenda Nungwi basi uwage nyumbani kwako jinsi ilivyokuwa barabara hakuna, useme nyumbani leo nakwenda Nungwi kutwa lakini sasa hivi kama utakwenda Nungwi jinsi barabara iliyokuwa kama kapet na kama utapata dereva mzuri unaweza ukasinzia ndani ya gari ukashtukia unaamshwa kuwa umeshafika Nugwi. Haya yote ndio maendeleo ambao wanayatarajia wananchi.

Mhe. Spika, ujenzi wa nyumba za maendeleo, labda niseme kwamba nyumba hizi za maendeleo zimeanza kujengwa kama sikosei tokea mwaka 1966 mimi sijazaliwa, zimekuja kumalizwa sasa hivi. Nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa.

Pia nije katika sekta ya nishati, hasa kwa kupeleka umeme Pemba. Sisi wanakamati tulikuwa tukenda Pemba tulikuwa tunaulizia leo mgao wapi, lakini sasa hivi Alhamdulillah sasa hivi umeme Pemba upo na ukenda unachagua hoteli unayotaka huulizi kama hoteli hii inajenereta au haina. Haya yote Mhe. Spika, ni maendeleo namuomba Ishallah Rais atakayekuja basi aige nyayo za Mhe. Rais wa Zanzibar Dokta Amani Abeid Karume.

Mhe. Spika, nilikuwa nina mengi sana ya kuchangia lakini kwa vile umenipa dakika tano na kwa kuokoa muda nitazungumza machache.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 5 nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa kutafuta eneo la kujenga jengo jipya la Wizara hii. Sote ni mashahidi pale ilipo Wizara kwa kweli hapatoshi, kama utapita basi msongamano wa magari mengi, foleni na hata mle ndani basi lile jengo limechoka sana. Lakini zaidi na la kupendeza lile eneo lililopatikana pale ni kugeuza matumizi baada ya matumizi yaliyokuwa zamani na sasa kuwa matumizi ya jengo la wizara hii, nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, ningependa nimshauri Mhe. Waziri alisema kwamba atajenga katika Fedha za Serikali na kwa kupitia wahisani. Labda nimuombe kwamba tusitegemee sana wahisani kwa sababu wahisani kama tunavyojua hawaaminiki, ukitegemea cha mtu inategemea kaamka vipi. Nilitegemea hapa Mhe. Waziri labda atwambie bajeti hii labda ametenga kiasi gani ya kuanza jengo hili. Naamini kwamba tunaweza na mifano ipo.

Mhe. Spika, wenzetu wa Wizara ya Elimu wameanza kujenga jengo lao pamoja na kuwa wametegemea wahisani lakini wamehamia hivyo hivyo pale chini na wapo. Wizara ya Wanawake na Watoto wameanza kujenga na wao wenyewe wamo. Unapojenga jengo na wewe mwenyewe ukiwepo unakuwa unahamasika kujitahidi kujenga lile jengo kuliko unapokuwa mbali, unasahau hasa kama unadhamana ya kujenga. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie hili japo tujenge

kwa awamu pengine mwaka huu tutenge bajeti kidogo, tujenge nusu, mwaka mwengine tutenge bajeti nusu, tujitahidi kujenga awamu kwa awamu.

Mhe. Spika, nije katika idara ya Mamlaka ya Maji inaonekana kwamba Idara yetu hi ya Mamlaka ya Maji bado haijakusanya mapato ipasavyo. Kuna wananchi wengi wanatumia maji lakini hawalipi. Idara hii naomba iangalie ifanye kazi pia watambue pia kuna wananchi ambao kuwa wanatumia maji bila ya malipo na kwa israfu (mengi zaidi) kwa mfano wanaofanya biashara ya matofali unaweza ukapita kwenye biashara ya matofali ukayakuta maja yamefunguliwa yanamwagika tu pengine masaa mawili au matatu. Pia wale wanaotumia mahodhi, mahodhi yanajazwa maji mpaka yanamwagika. Lakini kuna wananchi wengine hawatumii maji mengi. Kwa hiyo naomba Idara hii iwe inatumia kodi kwa kitaalamu labda pengine aweke TUKUZA mtu alipe kutokana na utumiaji wa maji.

Mhe. Spika, naomba niunge mkono asilimia 120 ya hotuba hii. Ahsante.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipati nafasi japo kuwa ndogo kuweza kutoa mchango wangu katika suala hili la Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mimi nitaanza moja kwa moja kwenye Mahkama za Ardhi, tunajua kwamba kazi kubwa ya Wizara hii ni kupokea kesi na kuzisikiliza na baadaye kuzitolea maamuzi. Lakini kutoka katika kitabu cha Waziri inaonesha kwamba idadi ya kesi ambazo zimetolewa si chini ya 171 lakini na zilizopata maamuzi kusikilizwa ni kesi 19, katika kesi hizi zilizobakia ni 152. Ambayo hii tunaona ni idadi kubwa ya kesi zilizobakia. Labda nimuulize tu Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizochangia kwa kesi hizi kuchelewa, labda tuseme ni kwa sababu ya uwezo wa hawa wanaoendesha kesi au tuseme kwa sababu nyengine kwamba hawa wanaoitwa katika kesi hizi huwa hawafiki Mahakamani. Kama kuna idadi kubwa ya kesi zinabakia tunasema mwenendo huu wa kesi umezorota sana na unaweza ukatia dosari katika wizara yake. Kwa hivyo, ninachomuomba Mhe. Waziri aweze kulifuatilia suala hili kwa jitihada kubwa.

Mhe. Spika, la pili katika kesi hizi 171 bado hatukupewa ufafanuzi mzuri kwamba kesi hizi zingeelezewa kwamba kila wilaya ni kesi ngapi ambazo zinahitajiwa kuelezewa, hivyo hazikuelezwa. Mhe. Spika, hii ni jumla jumla baina ya kesi za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika suala jengine ambalo nasema suala la Mradi wa Umeme ambao umepelekwa Pemba. Mimi niseme kwa upande wangu natoa shukurani zangu za dhati au pongezi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada yake kubwa kuhakikisha kwamba katika

awamu yake hii nafasi yake ameitumilia kwa kuwapelekea wananchi wa Pemba umeme. Hiyo ni jitihada kubwa sana nasema nampongeza kwa suala hilo.

Mhe. Spika, pia napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa jitihada yao kubwa ya kuhakikisha kufuatilia suala zima la umeme Pemba. Kwa hakika hili limesaidia kutatua matatizo mengi katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, pia napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Norway kwa kufuatilia na kufanya jitihada ya kuhakikisha kwamba umeme umepatikana kwa muda mfupi sana. Hilo ni jambo la kupongezwa. Pia sisi wananchi wa Pemba tutakuwa tumefaidika sana katika suala la umeme kwa mfano katika masuala ya viwanda vitaweza kutusaidia, mambo ya magereji moto humo umeme unatumika kwa hiyo wananchi watafaidika. Kwa hivyo, mimi nafikiri suala hili litaweza kupunguza umasikini ambao tunao kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, pia nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba pamoja na matatizo ya umeme ambao tumeunganisha lakini kuna suala la magenereta, magenereta haya yapo. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri suala la magenereta ayahuwishe ayaweke tayari ili kesi ikitokezea tuweze kuyatumia magenereta hayo.

Mhe. Spika, pia limezungumzwa suala la umeme mbadala. Mimi nataka niseme katika suala hili ni muhimu na namshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta watafiti kutoka nchi mbali mbali kwa kulisimamia hili suala. Suala hili tumelizungumza kwa muda mrefu kwamba tunahitaji umeme mbadala na kwa jitihada zake waziri na wakuu wote wa maidara na wizara kwa jumla wamelitilia mkazo na wameweza kutusaidia kuwa watu wako tayari kutusaidia. Hilo ni suala muhimu na tunawapa pongezi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la umeme uliopita wa *Phase IV*. Umeme huu tunashukuru kwamba na mimi katika jimbo langu nimefaidika kwa kupata maeneo mbali mbali. Mwaka 2007 na 2008 niliweza kubahatika nikapata maeneo ya Kipange, Msuka, Kipangani pamoja na Tondooni katika kipindi kile. Kwa hivyo, namshukuru Mhe. Waziri katika katika ahadi zake umeme huu tumeweza kuupata. Pia nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba kuna maeneo mengi ambayo bado umeme haujaweza kufika kwa mfano, katika kijiji cha Misufini, Makangale, Dodea na wananchi wa pale ambao ni watu wa mwanzo kufanya *installation* lakini na wao walipata bahati nzuri walikuwa ni watu wa mwanzo waliotegemea kupata umeme, na miti yao mingi ilikatwa kwa kutegemea kupata umeme, lakini mpaka hii leo umeme

hawajapata. Mhe. Spika, nimeshamuona Afisa Mdhamini mara mbili na wenyewe pia walikwenda wakaonana nae lakini bado hilo halijatekelezwa. Mhe. Spika, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hili suala aliangalie.

Mhe. Spika, katika suala ambalo lililokuwa ni muhimu ingawa itakuwa upande mmoja ni wako wewe na upande wa pili kwa Wizara ya Afya lakini kuna hospitali ya gharama kubwa ambayo tumeijenga Mkia Ng'ombe. Mhe. Spika, hospitali hii mpaka leo imekosa umeme na kutokana na pale bandari kuu masafa yake ni makubwa sana. Kwa hivyo, shauri lililotoka ni kwamba tuweze kupata *solar* ambayo hii itaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, jambo jengine nataka nimwambie Mhe. Waziri pale Konde pana transofoma moja ambayo transfoma hii *load* yake imekuwa kubwa sana. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri hili suala alipitie kwa sababu kila siku linaleta matatizo makubwa. Tumekwisharipoti mara nyingi lakini bado hatua hazijachukuliwa.

Mhe. Spika, sasa nije katika suala la mamlaka ya maji, mimi nataka niseme kwamba nimshukuru Mhe. Waziri kwamba ni watu ambao tulioifadika mara nyingi, katika kipindi changu hiki cha miaka 5 nimefaidika na maji, umeme na naendelea kufaidika na barabara ambayo iko katika mji wa Konde. Hizi ni shukurani kwa Mhe. Rais na shukurani kwa Mhe. Waziri na watendaji wake wote. Kwa hivyo, ninalomuomba Mhe. Waziri ni kwamba tangi la Konde ni bovu muda mrefu linavuja na linahitaji kufanyia matengenezo.

Pia nataka nimwambie Mhe. Waziri katika suala la mtandao wa maji kutoka Konde kuelekea Msuka hapa pana matatizo makubwa sana. Mtandao huu umeshindikana kupeleka maji kwa urahisi kila siku kunakuwa na malalamiko ya wananchi kwamba maji hayaendi sawa sawa. Pia kuna baadhi ya vijiji maji hayo hayawafikii kwa mfano sehemu ya Kivumoni, sehemu ya Bungi na baadhi ya sehemu maji hayafiki sawa sawa.

Vile vile nilikuwa nataka nimpe Mhe. Waziri ushauri kwamba pale katika eneo la Konde kisima kile ambacho kilichokuwa pale Mwembematrekta tunacho kisima ambacho tungeweza kukitumilia na kikaweza kuwasaidia watu wote ambao maji hawapati sawa sawa. Mhe. Spika, niliwahi kulipeleka suala hili tukaomba *machine* tukaambiwa *machine* iliyokuwepo ni kongwe, nikawaambia mimi *machine* kongwe siitaki tupatiwe *machine* mpya. Mhe. Spika, nimepata habari kwamba *machine* hii iko tayari, kama suala hili ni kweli ningemuomba Mhe. Waziri hili suala alifuatilie kwa umakini sana ili wananchi wangu waweze kufaidika na maji.

Mhe. Spika, niendelee katika suala jengine la mafuta na gesi asilia. Mhe. Spika, hili suala linaonesha kidogo lina utata, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie sana kwa sababu sasa hivi katika katiba yetu ya Zanzibar suala la mafuta na gesi asilia limo katika Katiba ya Zanzibar, suala hili hili pia liko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Spika, wao wanaona kama huu ni mtego mkubwa sana kwamba Wazanzibari watashindwa kuweza kulifuta suala hili katika katiba yao, kwa sababu liko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, sisi tumejiandaa kuhakikisha kwamba mafuta ni rasilimali yetu wenyewe na tunasema tuichimbe wenyewe bila ya wao kuwa ni *partners* wa suala hili. Kwa hivyo, kama suala hili tumekubaliana hapa katika Baraza la Wawakilishi na sera tukazitengeneza hapa katika Baraza ziko tayari na vile vile wanafunzi wetu wameshakwenda nje kwa ajili ya kusoma. Mhe. Spika, ikiwa bado sisi tunasema tunapeleka maombi yetu kwa Waziri Mkuu kwenye suala hili, huwa lile suala bado lina utata.

Mhe. Spika, kwa sababu unapompelekea mtu barua kwa kumuomba anahiari kukubali au kutokubali. Hili mimi ningekuomba Mhe. Waziri tupate ufafanuzi wa kutosha ili tuone hili suala likoje. Mhe. Spika, mimi ninaloliomba katika Baraza hili tukufu ni kwamba tuendelee kulizungumza hili suala na kulifanyia kazi na kama kuna kitu katika katiba kipindi kinachokuja cha Agosti au Septemba tuweze kuliondosha mafuta na gesi asilia tunasema iondoshwe. Mhe. Spika, mambo yote tunayosema tunataka kuyafanya katika mambo ya mafuta tuyafanye ili tuweze kujitegemea wenyewe na kutoa maamuzi katika suala hili, tusingojee mtu akatutolea maamuzi. Hili ndio jambo la muhimu.

Mhe. Spika, pia ningekuomba katika suala la maji, unajua tuna sekta hii ya KMKM ambao hawa mara nyingi wanalalamika kwamba wanapopita kwa masuala ya mambo ambayo yanawatokezea mara kwa mara maafa ya ndani ya nchi yanayotokezea kwa mfano moto hawa wanahitaji maji, na maji inasemekana kwamba kuna maeneo mengi hayawezi kupatikana. Ningelimuomba Mhe. Waziri kwa suala hili aweze kulifuatilia katika yale maeneo na kama unavyoujua mji wetu wa Unguja ulivyojengeka, haukujengeka kwa kupitisha magari ya kuweza kufika maeneo ambayo maafa yakitokezea. Mhe. Spika, pamoja na hayo iko haja ya kuhakikisha kwamba maeneo ya hawa watu kuweza kuchukua maji waweze kuyapata kwa urahisi zaidi.

Mhe. Spika, nastahi muda wako kwa hivyo mimi sina zaidi ila naunga mkono hoja hii mia juu ya mia na nashukuru alhamdulilahi rabilaalamina. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, vile vile nikazungumza machache tu kwa niaba ya serikali. Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wake wote na wafanyakazi wake wote wa wizara hii. Mhe. Spika, jitihada yao hakuna asiyeiona na waswahili wanasema "mwenye macho haambiwi tizama".

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwanza nilikuwa naomba sana hasa watendaji wa Idara ya Maji tunashukuru sana kwa kusikia kwamba huu mradi mkubwa wa Mkoa wa Mjini Magharibi tunategemea pengine labda mwezi unaokuja huenda ukawa umefikia tamati yake, na tunaamini kwamba baada ya hapo yale matengenezo madogo madogo ya kuunganisha laini za ndani zitakuwa chini ya mamlaka yao. Hili kwa kweli nalishukuru sana kwa sababu bado katika jengo langu la Kwamtipura tatizo la maji bado ni kubwa sana.

Kwa hivyo, naamini kwamba kwa kuwa tulikuwa tuna tatizo la miundombinu hilo mimi ninalifahamu kwa sababu ndio tunaogelea humu, lakini nilikuwa naomba sana baada ya kukamilika mradi huu sasa tukae kwa karibu ili kuhakikisha kwamba maeneo yote ndani ya Jimbo la Kwamtipura kama yalivyo majimbo mengine tuwe tunapata maji ya kutosha.

Mhe. Spika, nikiendelea tena na mchango wangu naomba sana kuna bomba ambalo lililotokea Welezo. Mhe. Spika, bomba la Welezo lile la saruji, bomba lile ndio linalopeleka maji mpaka yanayoelekea Mji Mkongwe. Kwa hivyo, bomba hilo sasa hivi limekuwa na *crack* nyingi hasa ndani ya Jimbo la Kwamtipura. Kwa hivyo, inawezekana pengine huu usumbufu wa maji wakati mwengine unatokana na zile *crack* ambazo zinazotokea katika bomba lile.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana kwamba wajaribu wawe wanafanya *survey* ya mara kwa mara. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya watu basi hata zile kuta zao za nyumba zimefika mpaka kwenye lile bomba lenyewe la maji. Kwa kweli hili ni tatizo na tatizo kubwa kwa sababu siku ambayo bomba lile litakatika ndani ya nyumba ya mtu basi huyu mtu itabidi lazima tukatafute kidau kwa ajili ya kumuokoa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba wajaribu kulifuatilia na bomba lile limeanza kutoka Saateni limekuja zake kupitia katika Shehia ya Shauri Moyo mpaka Shehia ya Kwamtipura kuelekea Welezo. Mhe. Spika, hili nilikuwa naomba sana wajaribu kulipitia ili zile *crack* ndogo ndogo waweze kuzifanyia marekebisho.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mkema alizungumza kuhusu suala la uvamizi katika eneo la kambi ya Unguja Ukuu. Hili Mhe. Spika, tunalichukua na Mhe. Waziri Kiongozi alikwisha kutupa agizo tushirikiane na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwenda kuliangalia eneo lile na kuweza kutoa ushauri unaofaa.

Mhe. Spika, si busara sana wananchi wakajenga karibu na kambi za jeshi, yaliyotokea Mbagala kiasi kama miezi sita mpaka mwaka mmoja uliopita kama mtu si wapale Mbangala basi akihadithiwa hawezi kujua ile ladha au tatizo la yale mabomu yalivyokuwa yanaripuka. Mabomu yalikuwa yanaripuka watu wanakwenda mbio utafikiria siku ya kiama.

Kwa hivyo, tulikuwa tunaomba sana hawa watu wanaojenga karibu na kambi za jeshi waachane na mtindo huu kwa sababu ukiacha matatizo ya kuingilia masuala ya mazoezi na ulinzi wa kijeshi, lakini pia usalama wa maisha yao pamoja na familia zao. Mhe. Spika, hili tunaahidi Mhe. Mkema tutampa mashirikiano tutakwenda kuliangalia hili eneo ili kuweza kutoa ushauri unaofaa, na pia tutaangalia kama kuna watu ambao wamo mule hawajajenga wanataka kujenga basi mimi nafikiri tutashirikiana na Mhe. Waziri waangalie katika viwanja hivyo vitakavyotoka basi watuachie kule kwenye kambi ya jeshi tuweze kuwapa viwanja katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, nikiendelea nataka nizungumze kidogo suala la mafuta. Unajua mara nyingi wajumbe wanapozungumza suala la mafuta wanalaumu sana kitendo cha Mhe. Waziri Kiongozi kupeleka barua kwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kulindoa suala hili la mafuta. Mhe. Spika, hapa tuko katika chombo cha kutunga sheria, hapa hatuko katika vibaraza vya kahawa au baraza za mazungumzo, hiki ni chombo cha kutunga sheria.

Mhe. Spika, suala la mafuta limo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hiyo wao ndio lazima walitoe kupitia kwenye katiba yao. Mheshimiwa pale kazungumza Katiba ya Zanzibar inazungumzia mafuta, Katiba ya Zanzibar hamna kifungu hata kimoja kinachozungumzia suala la mafuta na gesi, wale kule wakishalitoa sisi tutaliingiza. Mhe. Spika, lakini hakuna utaratibu mwengine bila ya serikali mbili kuweza kushauriana katika suala hili ni kwamba Zanzibar tumeshafanya maamuzi. Tumeshawaambia wenzetu sisi maamuzi yetu kutokana na sababu kadha wa kadha suala hili haliwezi tena kuwa la Muungano.

Mhe. Spika, katika kitu ambacho sasa hivi tunatakiwa tuwe makini serikalini katika suala la kufunga mikataba, tunasikia wenzetu huko Bara siku zote huyu sijui EPA huyu sijui hivi. Kwa mfano leo watu wameshafunga mikataba hewa tunaambiwa mikataba sijui inafungwa hotelini ina maana inawezekana kwamba

katika visima vya Zanzibar watu wakaja wakafunga mikataba sisi tutawabana vipi.

Mhe. Spika, Kamati ya PAC haina uwezo wa kwenda kumkamata mtu yeyote kwa hiyo hili nilikuwa naomba utukubalie kwamba kule tumekwenda katika utaratibu wa kawaida. Kule Bungeni lazima apelekewe Waziri Mkuu kwani yeye ndiye kiongozi wa shughuli za Bunge na ndio maana hapo Waziri Kiongozi akampelekea Waziri Mkuu ambaye yeye sasa ndio atalipeleka pale ili Bunge likapige kura kwa ajili ya kuliondoa. Mhe. Spika, nina amini suala hili litaweza kuondoka.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umefikia pazuri dakika saba zimekwisha sentensi moja ya kufungia hotuba hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa kumaliza baada ya hayo machache sasa mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaiunga mkono hotuba hii lakini kuna jambo nilikuwa nataka kulisema nitakuja kulizungumza katika hotuba nyengine. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nawaomba radhi baadhi ya waheshimiwa wangu ambao wamekosa nafasi ningependa sana ningewaita wote wakaweza kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi lakini haikuwezekana hivi kichwa kinaniuma jinsi nilivyokuwa *under suspense* kuona kwamba nimudu angalau kila mmoja kuweza kuzungumza, lakini sikumudu hivyo kwa sababu tulipanga kwamba tumalize shughuli hii kipindi hiki cha asubuhi. Kwa hivyo, namuomba radhi Mhe. Rashid Seif Suleiman pamoja na Mhe. Moh'd Ali Salim (Mulla) wao sikumudu kuwapa nafasi. Nadhani wataandaa utaratibu mwengine wa kuweza kumuarifu Mhe. Waziri nini wanataka kusema. Kwa hivyo, sasa namuomba Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi naye achangie katika hoja hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, na mimi naomba niungane na wachangiaji wengine 26 na mimi niwe wa 27 katika kuchangia bajeti hii. Lakini kabla ya hapo namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uwezo niko hapa leo. Mhe. Spika, bajeti hii ilichangiwa na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu akiwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kumalizia na Mhe. Hamza Hassan Juma na hatimae mimi na baadae Mhe. Waziri mwenyewe atakuja kumalizia jahazi hili.

Mhe. Spika, kwa upande wa umeme napenda kutoa shukurani zangu za dhati kabisa katika mwaka huu wa fedha jumla ya vijiji 48 kwa Unguja na Pemba vitapatiwa umeme, vijiji hivyo kwa hivi sasa hamna. Kwa upande wa Unguja ni vijiji 22 na kwa Pemba kutakuwa na vijiji 48. Natoa shukurani zangu za dhati

kabisa kwa Mhe. Waziri na wizara nzima kwa ujumla miongoni mwa vijiji ambavyo vitakuwemo kwa upande wa Unguja lazima jimbo langu na mimi niliseme kutakuwa na kijiji cha Dongongwe, Ghana na Kiboje Muembe shauri mimi ndipo nilipozaliwa lakini bahati mbaya umeme hakuna, lakini nafarajika kwa mwaka huu vijiji hivyo umeme utakuwepo.

Mhe. Spika, mchango wangu utakwenda huku nikisaidia moja moja yale mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyataja. Mhe. Spika, Mhe. Ramadhani Nyonje Pandu yeye kama Mwenyekiti alitoa pongezi zake na kutoa maelekezo ya hapa na pale lakini pia Mhe. Hamad Masoud Hamad moja ya jambo ambalo amelizungumza ni suala la mafundi ambao kwa muda mrefu walikuwepo katika ule mradi wa umeme vijijini.

Mhe. Spika, imani yangu kwamba kama ajira itakuwepo basi mafundi wale ambao walishiriki katika mradi ule wa umeme vijijini watapewa nafasi ya kwanza katika kuwaajiri. Ni kweli Shirika la Umeme lina matatizo ya mafundi na kwa hiyo haja ya kuwa na wafanyakazi wa ziada ipo, kwa hiyo haja hiyo ikitokea wale mafundi watapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali alizungumzia suala lake la maji tunamfahamu sana Mhe. Ali kwamba bado tatizo linaendelea. Mhe. Spika, wewe mwenyewe binafsi na kamati yako ambayo napenda niipongeze sana ningekuwa nawajua majina ningewataja wamekuwa wafuatiliaji sana katika suala zima la maji katika eneo hilo. Kwa hivyo, haya maeneo ya Muungano ambayo bado yana tatizo imani yangu kwamba mradi wetu wa maji wa Mjini Magharibi ambao utamalizikwa mwezi ujao ukikamilika basi eneo hili tatizo la maji nalo litaweza kupungua.

Mhe. Spika, mchango mwengine napenda nimshukuru sana rafiki yangu Mhe. Ali Moh'd Bakari huyu alikuwa ni mwakilishi wa mwanzo hasa katika kipindi kile ambacho hali ya kisiasa kadri pande mbili za chama zilikuwa ngumu yeye alikuwa ni mwakilishi wa mwanzo mimi kunichukua jimboni kwake hasa katika suala zima la umeme. Wakati fulani Mhe. Spika, wawakilishi wana sifa moja ina uzuri wake na ubaya wake, unaweza ukalia maiti si wako tulikuwa tukifanya kazi kwa pamoja ndani ya jimbo lake. Napenda sana nimpe shukurani zangu za dhati kabisa kwa ushirikiano wake ambao uliniwezesha kufanya kazi Pemba bila ya wasi wasi, bila ya hofu pamoja na wawakilishi wengine wote.

Mhe. Spika, katika hili napenda sana niwashukuru wananchi wa Pemba kwa ujumla kwani wengi walikuwa wana hofu sana kufanya kazi Pemba. Mhe. Spika, wakati fulani niko kule baadhi ya wanachama wa chama changu waliniuliza kwa sababu nilikuwa nikifuatana na CUF waliniuliza wewe unawafahamu wale, nikawaambia ninawafahamu ni nani wale nikawaambia ni

CUF. Nikawaambia mngenihoji kama mngenikuta niko katika matawi ya chama cha CUF nahutubia ni suala jengine lakini unaponikuta nakwenda majimboni kwenye suala la miradi hili halikuwa likinipa wasi wasi.

Mhe. Spika, ndio maana niliweza kufanya kazi zangu kule kama Mhe. Waziri alivyokuwa akiniagiza mara kwa mara bila ya hofu. Mhe. Spika, mpaka leo nikenda kule Pemba basi nikirudi huwa na zawadi ya mafenesi, ndizi, viazi na kila kitu. Hii ni kuonesha vipi nilikuwa kufanikiwa kufanya kazi kule.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yeye alichangia suala la tatizo la maji kule Kinduni. Napenda kuwafahamisha kwamba tuna mpango wa kuchimba kisima maeneo ya Mahonda ambayo yatatoa huduma za maji pale Mahonda na kule Kinduni na maeneo ya jirani. Kwa hivyo, kazi hiyo imeshapangwa na kwa kushirikiana na yeye itakwenda kufanywa ili kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Spika, jambo jengine pale maeneo ya Kiwengwa alisema kuna kisima wananchi wamekosa maji sasa hivi kwa sababu kuna hoteli ambayo imekatiwa umeme. Ni kweli tatizo hilo lipo ni kwamba wananchi wale walikuwa wakipata maji kupitia kwenye laini ambayo ilikuwa inakwenda kwenye hoteli wakati wale wanapopata maji kwenda kwenye hoteli yao. Mhe. Spika, hoteli hiyo imefilisika kidogo wamekatiwa umeme, hata hivyo tumezungumza na Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji kuangalia ni uwezekano gani kwenda kuangalia pale ili tuweze kurudisha huduma ile ya umeme kwa eneo lile tu ili wananchi hao waweze kupata huduma ya maji ili tusiwaadhibu.

Mhe. Spika, pia alitaka kujua tulikubaliana kwamba nyumba nyingi hasa za vijijini na pengine hizi za mjini zilizokuwa za Serikali basi ziuzwe, lakini alipata fununu kwamba zoezi hili limesitishwa. Mhe. Spika, napenda nimfahamishe Mhe. Mwakilishi na wananchi wengine kwamba zoezi hili halijasimamishwa na linaendelea na maeneo mengi kabisa watu ambao wanaokaa ndani ya zile nyumba wameshaleta maombi yao na wengine tayari wamekwishauziwa. Kwa hivyo, kama kuna dhana hiyo dhana hiyo haipo nyumba hizo zinaendelea kuuzwa na kama yeye kuna wananchi wake ambao wamo ndani ya nyumba hizo basi waendelee na utaratibu wa kupitia mikoani na hatimae kwa Idara ya Nyumba.

Mhe. Spika, suala la kupeleka umeme vijijini hili litaendelea na lazima tukubali kwamba sasa hivi ndio kazi iliyobaki kupeleka umeme vijijini. Pamoja na jitihada zimefanyika kupeleka umeme huu lakini kuna vijiji vyengine kazi hiyo itakuwa inaendelea hatua kwa hatua kikiwemo kijiji hicho cha Matetema ambacho Mhe. Mwakilishi alikitaja ikiwa pia ni ahadi ya Mhe. Waziri ambaye alikwenda wakati huo.

Mhe. Spika, karibu wawakilishi wote wamekuwa wakifanya kazi vizuri katika majimbo yao, wanachangia nguzo, wakati mwengine wanachangia waya. Lakini alisema jitihada ziendelee wawakilishi wakitoa nguzo 10 basi shirika nalo litoe nguzo 10. Mhe. Spika, nasema jambo hili sio baya lakini vizuri ni kwamba wakakaa pamoja ili kwenda kufanya tathmini ya ku-*survey* na kupima pamoja na kujua ni vitu gani vinavyohitajika, mita ngapi za waya na vitu vyengine ili kujua tathmini nzima na kuona vipi mradi ule katika eneo lile utaweza kutekelezwa hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, swahibu yangu Mhe. Abdalla Juma Abdalla nataka nimpongeze kwa michango yake, lakini aliweza kuzungumzia suala hili la umeme mbadala wengi wamesema je, kuna siku ndugu zetu wakinuna wakaamua kukata umeme itakuwaje. Mhe. Spika, napenda nimthibitishie Mhe. Mwakilishi na wajumbe wote wa Baraza kwa kweli katika suala zima hili la kutafuta umeme mbadala wizara imejidhatiti vya kutosha na kwa sasa hivi kupitia mradi wetu ule wa umeme wa mawimbi ya bahari tayari Shirika la Umeme limeshalipa kwa Idara ya Mazingira jumla ya shilingi milioni kumi na tano kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huu.

Kazi hiyo wameahidi itakamilika baada ya miezi miwili ikiwa tayari wiki mbili zimeshapita, hii ni kuonesha ni kwa kiwango gani tumejiandaa na wenzetu wa Israil wako tayari fedha zipo na mradi huu unatarajiwa uanze na *mega walt 10 mega walt 40* na hatimae kwenda pole pole hadi kufikia *mega walt 40*. Nafikiri tukiwa na kutoka kwenye mradi mwengine nadhani sasa tutawapelekea hata Tanga umeme badala ya umeme kutoka Tanga kuja Pemba utatoka Pemba kwenda Tanga. Pia kuna Kampuni nyengine ya Kichina ilikuja hivi karibuni wao ni kwa ajili ya *wind power*. Kwa hivyo, tunajitahidi ili hayo yasitokee na pindipo yakitokea basi tuwe tayari tumejidhatiti.

Mhe. Spika, pia hofu yako ya pale ambapo ukitoa salam huitikiwi, nenda na mimi niko tayari twende, salam nitatoa mimi nafikiri zitaitikiwa ili kuwapa moyo wananchi wale wasiwe na hofu. Hatua kwa hatua, kidogo kidogo na siku ikifika maeneo hayo na maeneo yote ambayo hayana umeme na maji tutaweza kupeleka.

Katika jambo hili nataka nieleze jambo moja. mtakumbuka kwamba tulikuwa tukitumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya umeme wa kununua mafuta Pemba. Kwa wastani kwa kila mwezi tulikuwa tukilipa si chini ya shilingi milioni mia sita kununua mafuta ya kuendeshea yale majenereta Pemba.

Baada ya kupatikana kwa umeme huu wa kutoka Tanga kuja Pemba, tabaan kiasi kile cha fedha sasa kitapungua na kwa hivyo, shirika litaweza kujipanga vizuri, kuona kiasi kile cha fedha ambacho zamani kikitumika kwenye ununuzi

wa *IDO*. Yale mafuta, sasa kitakwenda katika kuendeleza umeme katika maeneo yetu ya vijiji.

Kwa hivyo, imani yangu kwamba maeneo mengi ambayo hayana umeme yataweza kupata umeme ingawa siwezi kusema kwa leo na kesho, lakini kwa kweli ndio kazi ambayo sasa itakuwa imebaki. Wakati ule tulikuwa tunatibu kaka sasa amebakia mduduupande tu.

Mhe. Spika, pia kuna yale maeneo mengi ambayo yamekuwa na transfoma ambazo zimeungua. Mhe. Spika, hivi sasa tumeshaagiza *transfoma* karibu 26 kule Arusha na tunatazamia baada ya kipindi kifupi zitafika. Kwa hivyo, maeneo mengi yale ambayo yana tatizo hilo yataweza kurudishiwa huduma zake za umeme.

Mhe. Spika, swahibu wangu Mhe. Haji Faki Shaali pamoja na michango yake mingi alizungumzia suala la maji katika maeneo ya Kisiwapanza na maeneo mengine. Lakini pia alizungumzia suala la TUKUZA. Napenda nimthibitishie kwamba, tunaendelea na jitihada kuona maeneo haya ya Kisiwapanda hasa kule mbele kwamba hakufiki maji, basi tunajiandaa kufanya matayarisho ya kuchimba kisima chengine ili yaweze kuongeza nguvu na maji yaweze kupatikana katika eneo lote lile.

Kwa upande wa suala la mita za TUKUZA, Mhe. Spika, napenda nimthibitishie kwamba, shirika linaanya jitihada na linaendelea kwa kasi kubwa kabisa kuendelea kuona bado mita za TUKUZA zinaendelea kufungwa. Mtakumbuka hivi sasa karibu mita 33,000 zimeshafungwa na kati ya hizo mita 27,600 zimefungwa Unguja na mita 5,400 zimefungwa kule Pemba na tunategemea kwa mwaka huu karibu mita za TUKUZA kama elfu kumi zitafungwa Unguja na Pemba kwa pamoja. Kwa hivyo, bado jitihada hizo zinaendelea na tumekuwa tukienda katika maeneo tofauati, leo eneo hili kesho lile.

Lakini kwa waheshimiwa na wale ambao wana uwezo, hata kama yuko kijijini kule ambako bado hakukupangiwa utaratibu wa kupelekwa TUKUZA. Kama yeye mwenyewe akitaka inabidi utaratibu wake mwengine atalazimika kulipia gharama zaidi kidogo. Lakini hata kule atafungiwa mita za TUKUZA. Lakini ajue tu kwamba hakutakuwa na kituo cha kuuzia umeme kule ikiwa kule Tundauwa au kwengine, hakutakuwa na kituo kwa sasa hivi, labda maika ya mbele huko. Kwa sababu huko mbele tunakokwenda azma yetu Unguja nzima na Pemba tuwe na mita hizi za TUKUZA.

Kwa hivyo, mtu wa kijijini ambaye uwezo anao, pengine una gari lako mwenyewe umeme umekwisha unachukua gari unakuja zako mjini basi utaratibu huo upo. Sasa Mhe. Spika, katika hili asiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika: Niwaombe wale Waheshimiwa Wajumbe ambao wanatoka nje kwa dharura, basi wakumbuke kurudi ili tuje tumalize kazi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, jengine swahibu wangu Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumzia suala la Mamlaka ya Maji iimarishwe. Wazo hilo tumelisikia na watendaji wenyewe wapo tutalifanyia kazi. Lakini pia nataka nimtoe wasi wasi Mhe. Said Ali Mwakilishi wa kudumu wa Jimbo la Gando. Yule ni mwakilishi wa kudumu Mhe. Spika, pale, mwaka huu atakuwepo pale, baada ya miaka mitano yuko pale na mingine mpaka mwenyewe atapoamua kuacha.

Nataka nimtoe wasi wasi kabisa, tuna mradi wetu wa *ADB* ambao umehusisha miji yote mitatu, Mkoani, Wete na Chake Chake. Kwa hivyo, maeneo yake yale ya Bopwe, Kizimbani na mengine yataingia katika mtandao huo na hivyo asiwa wa wasi wasi tatizo la maji litaondoka baada ya mradi huu kuanza kazi na hautakuwa na muda.

Jambo jengine Mhe. Spika, alizungumzia juu ya suala la kupatiwa umeme kisiwa cha Fundo. Mhe. Spika, nia yetu ni kuona visiwa vyote vya Unguja na Pemba vinaweza kupatiwa umeme nadhani kwa kule Pemba tulianza na Kisiwa cha Kojani sasa hivi tunakwenda na kisiwa cha Tumbatu hapa. Kwa hivyo, hatua kwa hatua basi maeneo haya mengine nayo tutaweza kupeleka umeme ikiwa huu wa *grid* au vile vile pengine kwa kutumia *solar power*.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Said Ali Mbarouk niwaambie ndugu zangu pale, shemegi zangu, rafiki zangu wa Madaniwa kweli nilisema nitakwenda na sikuwahi kwenda. Lakini Mhe. Spika, pale kuna transfoma imeshawekwa tena imewekewa pale tayari kwenye *pole*. Unajua wanasiasa wakati mwengine hasa wakati wa uchaguzi ukifika huwa tunafanya mambo ya ajabu sana. Lakini jitihada ya kuwa transfoma ile ipo lazima zichukuliwe ili sisi kama shirika basi tuweze kupeleka *wire*. Meneja wa tawi la Pemba pale ananisikia namuomba awasiliane na Mhe. Said ili ile transfoma isikae bure.

Nawashukuru wananchi wale hawakufanya fujo wala kelele wamekuwa wakisubiri. Kwa hivyo, wapelekee salamu zangu hizo, niliahidi kuwa nitakwenda lakini Mwenyezi Mungu hakunijalia, lakini huduma ya umeme tutajitahidi kuona inapelekwa ile transfoma ile isikae bure.

Mhe. Spika, kweli nisije nikamsahau Bi Baby kama ulivyonambia na kama ulivyompamba. Ni kweli huyu mama alifika ofisini kwangu katika suala lake la tatizo la kiwanja pale njia ya kwendea Konde. Sina hakika ushauri gani nilitoa, lakini ushauri niliotoa ambao ninaukumbuka wakati huo ulikuwa unampa haki yeye. Siukumbukii nimesahau. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Said kama

alivyopewa na ujumbe na Bi Baby basi na mimi nakupa ujumbe kwa bibi huyo aje tuwasiliane tena ili tuone vipi tunaweza kukamilisha kazi hiyo.

Mhe. Spika, swahibu wangu Mhe. Hija Hassan Hija kwanza nataka nikupongeze.Ninaomba sana unipelekee salamu zangu kwa wananchi wa Kijiji cha Msengele. Naomba sana usisahau kupeleka salamu zangu hizi. Wale wazee ni wakarimu sana na wana moyo na mchango wao wa shilingi milioni nne ambazo wamezitoa kwa ajili ya kupeleka zile nguzo. Basi nguzo wakati wowote tutazipeleka. Kwa kweli lile eneo lina ugumu wake, tulishindwa katika kipindi hiki na hata tulipokwenda ni kipindi cha tatizo la umeme hapa Unguja hivyo mazoezi mengi ya masuala ya umeme yalisimama.

Hata hivyo, lile eneo ikija mvua hatuwezi kufanya kitu. Nashukuru juzi niliwasiliana nao walisema basi wao nguzo zikipelekwa mpaka pale sipakumbuki, wako tayari watabeba wenyewe kwa kichwa. Napenda nikuthibitishie Mhe. Hija waambie wazee wangu wale wa Msengele wakati wowote ule hali ya ardhi ikiruhusu kufika gari pale tutazipeleka katika kipindi kifupi na kama gari haifiki, basi tutazipeleka pale ambapo wao wamesema na watazifikisha kule.

Katika hali ya mazingira ya kule ningemuomba Mhe. Meneja na najua wale wazee wa kule wanaweza wakatupatia hata nyumba pale ili wale wafanyakazi pale kama ni kazi ya wiki moja, basi wapige kambi pale ili kuweza kuchomeka yale maguzo badala ya kuwa na kazi ya kwenda na kurudi. Kwa sababu mfano mvua ikinyesha trekta halifiki. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi na hoja ile ambayo alisema kwamba atazuia kifungu. Lakini kwa kadiri ninavyokujua na tulivyo mimi na wewe , tuna mengi mimi na wewe tunajuana ukiacha hili, basi naona hakuna haja ya kuzuia kifungu.

Nataka nikulaumu kidogo si sana, kwamba mimi na wewe tulivyo hili jambo la kule Mwambe la watu kuwa wameshakaa miaka miwili wameleta maombi yao. Ni kwamba taarifa zilizopo pale kuna ombi moja tu kutoka Mwambe na lilikuwa la mwaka 2010. Sasa inawezekana wako wajanja, hawa ndugu zangu wa Pemba kuna jina wanawaita, kishoka, hawa ni wafanyakazi ambao wana dhambi zao ni waongo wanawahadaa. Kwa kweli katika hili ningemuomba Meneja wa Shirika la Umeme kwa upande wa Pemba hatua ya kwanza ni kuona wale ambao wamenyang'anywa hizo pesa zao wengine naambiwa shilingi laki nane, laki ngapi. Hatua ya kwanza waende wakamuone Meneja ili waendelee na utaratibu wa kuweza kupatiwa umeme.

Kwenye ile misikiti ambayo iliungiwa umeme bila ya mita nasema haya mengine inawezekana tumeyafanya sisi viongozi, wawakilishi ama wabunge. Unajua unaweza kwenda mheshimiwa hapa kesho msikiti unafunguliwa basi

angalau uwekwe umeme kwa siku ile ya mwanzo tu. Baada ya hapo sasa tunasahau.

Hata juzi hapa Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ni sisi wenyewe. Kulikuwa na ziara ya Makamo wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenye tawi lake jipya amejenga pale, basi tuliona si vibaya kwa siku ile tukamuwekea umeme wa dharura tu, lakini baada ya kuweka walijisahau kidogo. Juzi Meneja katoa agizo kamkatieni. Kwa hivyo, haikuwa dhambi, sasa baada ya kukatiwa ameanza na utaratibu wa kikawaida kurejeshwa umeme.

Kwa hivyo, nasema inawezekana huko. Lakini hatua ya mwanzo ya msingi kabisa ni kuona maeneo yale ambayo kulikuwa na umeme kwa bahati mbaya mira hazikuwekwa nini kilitokea? Sijui, sitaki kuangalia dhambi nataka kuona kwanza nasahihisha dhambi. Wananchi wale kwa kufuata utaratibu Mhe. Hija naomba nenda kawachukue tena kwa gari yako au kama wanayo haya, wende kule wakakamilishe utaratibu. Napenda nikuahidi mita tunazo, *wire* tunao, wote wale ambao walikuwa na maombi yao kazi hiyo itafanywa kwa muda mfupi mara tu baada ya kukamilisha taratibu za kujaza fomu na mambo mengine.

Mhe. Spika, jambo jengine nisije nikasahau ambalo limezungumzwa na wajumbe wengi, kwamba hali ya wananchi wetu vijijini kwa kweli kifedha uwezo wao ni mdogo na haitakuwa vyema kwamba kiasi kikubwa cha fedha kimetumika kupeleka umeme vijijini wananchi wale sasa wakawa wanashindwa kutumia.

Mhe. Spika, ninachokifahamu mimi ni kwamba, shirika lina utaratibu wa kutoa mikopo kwa wananchi wa vijijini si mjini kwa ajili ya kuungiwa umeme. Wanalipa kiasi fulani cha fedha na kiasi fulani wanalipa pole pole. Lakini baada ya kupata barua ya sheha na pia kupata wadhamini. Wadhamini wakubwa hapa mara nyingi wanakuwa ni wabunge na wawakilishi wenyewe. Kwa hivyo, imani yangu kwamba bado zoezi hili litaendelea katika vijiji vyote vya Unguja na Pemba. Sasa wale wawakilishi watachukua dhamana ya wananchi wao ili waweze kupata huduma hiyo, sasa ikiwa mwakilishi yule mteja hakulipa tutamkatia na pengine utaratibu wa kukukata wewe mshahara kupitia Barazani ili ulipie deni lile litafuata baadae.

Mhe. Spika, swahibu wangu Mhe. Subeit Khamis Faki napenda sana nimshukuru. Alitaja vijiji vyake viwili kwa bahati mbaya yeye mwenyewe alivisahau jina, lakini alimradi kimoja ni cha Chupwe na ni kweli hakina maji. Basi tutajitahidi kupitia Mamlaka ya Maji kupeleka maji pale lakini na huo umeme.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alizungumzia suala la maji katika mtaa wa Mwembetanga pale na Vikokotoni, ambapo tatizo la Mji Mkongwe baadhi ya maeneo kumekuwa na tatizo kubwa la maji. Katika maeneo hayo Mhe. Spika, basi kupitia mradi wetu wa maji wa *Phase II* hii ya Mjini Magharibi baada ya kukamilika mwezi ujao nafikiri tatizo hili litapungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba uniruhusu niseme machache dakika mbili. Mhe. Spika, binafsi napenda sana kumshukuru Mhe. Waziri wangu. Katika kipindi hiki cha miaka mitano hakuwa na choyo, mara zote nilipomshauri alikuwa msikivu na aliponambia hili usifanye niliacha. Kwa hivyo, napenda sana kumshukuru kwa ushirikiano wake ambao tulikuwa pamoja katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Lakini pia napenda sana kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi; Wakurugenzi wote na watendaji wengine akiwemo Afisa Mdhamini kule Pemba kwa ushirikiano ambao alinipa katika kipindi chote hiki ambacho nimekuwa Naibu Waziri pale. Kwa hivyo, napenda sana kuwashukuru.

Mhe. Spika zaidi ya hayo nasema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa mara nyengine kunipa nafasi ya kujumuisha michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwenendo wa kikao hiki cha bajeti wizara yangu mpaka hivi sasa naona imepata wachangiaji zaidi kushinda wizara nyengine. Tumepata jumla ya wachangiaji 34 nao ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi)
2. Mhe. Hamad Masoud (Waziri Kivuli Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi)
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Ali Moh'd Bakari
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
7. Mhe. Haji Faki Shaali
8. Mhe. Said Ali Mbarouk
9. Mhe. Hija Hassan Hija
10. Mhe. Subeit Khamis Faki

11. Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej
12. Mhe. Mkongwe Nassor Juma
13. Mhe. Omar Ali Shehe
14. Mhe. Ame Ussi Juma
15. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin
16. Mhe. Haji Mkema Haji
17. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
18. Mhe. Asaa Othman Hamad
19. Mhe. Ali Abdalla Ali
20. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
21. Mhe. Salim Abdalla Hamad
22. Mhe. Abass Juma Muhunzi
23. Mhe. Ali Denge Makame
24. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
25. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
26. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi
27. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Thuwaybah E. Kissasi
2. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
3. Mhe. Ame Mati Wadi
4. Mhe. Rashid Seif Suleiman
5. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo
6. Mhe. Ashura Abeid Faraji
7. Mhe. Mohamed Ali Salim

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kunipa uwezo wa kusimama hapa mbele ya Wajumbe wa Baraza hili tukufu. Nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kutuwezesha kipindi chote hiki afya njema, dhamira thabiti na kutuwezesha kufanikisha majukumu tuliyokabidhiwa na nchi yetu kama mlivyosema wenyewe, kwa ufanisi, umakini na uadilifu mkubwa. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, niendelee kwa kukushukuru wewe Spika wetu kwa kipindi chote hiki, kwa malezi yako na mapenzi yako kwetu kwa namna unavyotuongoza, miaka yote ulivyokuwa ukitusaidia. Nimshukuru pia Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wako kwa mchango wao kwetu. Lakini kwa makusudi niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa kipindi chote hiki kwa namna mlivyokuwa mnatusaidia. Kwa ihisani kubwa ambayo tumekaa sote, kwa heshima na utu tuliousimamisha, niwashukuru na kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie nyote na famila zenu heri na fanaka kwa kila mlilolidhamiria.

Niwaombe pia, aliyekamilika ni Mwenyezi Mungu pekee. Nikiwa ninamaliza muda wangu kwenye wizara hii kwa pale nilipowakosea ninawaomba mnisamehe.

Mhe. Spika, niendelee kukushukuru sana mwenzangu, ndugu yangu, Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi (Mhe. Tafana Kassim Mzee), kwa msaada wake mkubwa kwangu. Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi haikuwa na waziri na naibu waziri, imekuwa na mawaziri wawili ambao kwa kweli tumeshirikiana kwa pamoja na kama mlivyodhihirisha nyinyi wenyewe mafanikio hayo yamepatikana kwa juhudi kubwa sana za Mhe. Naibu Waziri wa Maji anayekwenda kila jimbo, kila mkoa, kila wilaya, kila kijiji na kila mradi ambao umekuwa na mafanikio amekuwa na juhudi kubwa sana za kuusimamia mradi huo. Nakushukuru sana TK (Tafana Kassim), mwenzangu na ninawaomba wananchi wa Jimbo la Uzini wakuchague ili uendelee na mchango wako katika nchi yetu.

Namshukuru sana pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Ndugu Mwalimu Ali Mwalimu. Nakushukuru sana Katibu Mkuu kwa umakini wako, utulivu na busara ambazo umekuwa ukizitumia katika kutusaidia sisi wenzako katika uendeshaji wa wizara hii ngumu sana. nakushukuru sana Ndugu Mwalimu Ali Mwalimu.

Namshukuru pia Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mipango na Sera na viongozi wote wa Wizara ya Maji kwa umoja wenu, kwa juhudi zenu, umakini, mapenzi kwa nchi yenu na mafanikio ya wizara yetu yamedhihirishwa na kauli za kila mjumbe wa Baraza hili anayewakilisha wananchi wa nchi hii aliyesimama kuchangia hotuba ya bajeti yetu.

Mimi na Mhe. Naibu Waziri wangu tunamaliza muda wetu kwenye wizara hii, tunawashukuru sana, tunawatakia kila la heri nyinyi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji kwa uungwana wenu, mapenzi na juhudi zenu katika kutusaidia mimi na Mhe. Tafana. Tunawaomba wataokuja baada ya sisi muwasaidie zaidi ya mlivyotusaidia sisi. Na ile kaulimbiu ya wizara yetu ya uwazi na ukweli muendelee kuisimamia na kwa hao wanaokuja waanzie kwa mlango huo. Tunawashukuru sana Mwenyezi Mungu awajalie kila la heri nyinyi na familia zenu wote ndani ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu pia nishukuru wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa imani yao kwangu na kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Ninawashukuru sana, ninawaombea kila la heri *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie neema, furaha na baraka. Pia ninawaomba waungwana kwamba nina dhamira ya kurudi tena kuomba kuwa mwakilishi wao. Mwenyezi Mungu akinipa uwezo huo, ninawaomba wakati huo ukifika kwa heshima na taadhima

kubwa wanichague kuendelea kuwa mwakilishi wao wa Jimbo la Kiembesamaki.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii makhsusi pia kumshukuru waziri aliyenitangulia mimi Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Kilimo kwa heshima tunamuita babu, sio babu kwa sababu hayuko *fit* aa, sote tunajua babu yuko *fit* sana. lakini tunavyompenda tunamwita babu, kwa busara na hekima zake.

Nakumbuka wakati nikiwa Naibu Waziri kwenye wizara hii, jambo la mwanzo aliponita ofisini kwake tunajiandaa kujibu maswali na majibu kwenye kikao cha mwanzo, akaniambia sikiliza mwanangu, sikiliza kijana wangu. Utapokwenda kwenye Baraza la Wawakilishi na utapofanya shughuli zako za kisiasa daima sema ukweli. Usiende Baraza la Wawakilishi ukawadanganya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wanatambua na kuelewa kila jambo na. Wizara hii mimi nataka niiongoze kwa ukweli.

Matatizo tunayo mengi. Wizara ya Maji mwaka 2002 jamani mlikuwa mnaijua, hakuna kikao hapa kilichokosa maswali 60 hayapungui 50 kwa hali mbaya iliyokuwepo wizara ile kipindi kile. Lakini akasema kwa vile dhamira na nia zetu ni safi, basi sisi tusimame na ukweli. Mafunzo yale nimekuwa nimeweka mbele ya uso wangu tangu siku ile hadi hii leo Mhe. Burhani Haji Saadat nakushukuru sana sana. mbali ya hayo kwa malezi yako na ustahamilivu maana yake mwaka 2000 nilikuwa nina miaka 34 kijana bado, lakini siku hizo ninawaka moto. Waziri alihitaji kuwa na ustahamilivu sana katika kunilea na kunielekeza.

Mhe. Buruhani umefanya hivyo, ninakushukuru sana baba yangu, mzee wangu na ninakuombea Mwenyezi Mungu akujalie kila la heri. Najua Jimbo la Kikwajuni liko *fit* kama ulivyo wewe mwenyewe, lakini tunakuombea *Inshaallah* kwa Mwenyezi Mungu akujaalie mafanikio yalikuwa makubwa zaidi. Mhe. Buruhani kwa niaba yangu mimi, naibu waziri na wenzangu wote ambao mpaka hii leo wanakukumbuka na kukuheshimu tunakushukuru sana.
Nataka nichukue fursa hii pia kuwashukuru Mhe. Spika, wajumbe wakongwe wa Baraza hili tukufu. Nakumbuka kipindi hicho cha mwaka 2000 kilikuwa kigumu sana. Lakini tulipata watu waungwana humu, siasa ilikuwa ngumu. Siasa ya upinzani hata siasa ndani ya Chama cha Mapinduzi, ilikuwa ngumu sana. Lakini nawakumbuka viongozi humu wawakilishi, Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu. Mhe. Kamal Basha Pandu, Mhe. Amina Salum Ali, Mhe. Ali Juma Shamuhuna na hasa Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein.

Baada ya kupigwa maswali magumu na mazito, lakini bado walikuwa na uungwana wa kukutafuta naibu waziri, kukuvuta pembeni na kukuelekeza hapa ulikosea mara ya pili ukijibu basi jiandae hivi, huko nyuma hili jambo lilikuwa hivi, litafiti zaidi, jipange vizuri zaidi. Sasa huo ni uungwana Mhe. Spika.

Hata wewe mwenyewe ulikuwa unatoa fursa tujifunze, lakini ulipowaona vijana wako sasa tumefika pahala taabani ulikuwa unatumia busara ya kiti chako na kutuokoa lakini hatimaye tumeshapata funzo. Tunakushukuru sana niseme tu Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) mtamu na *Inshaallah* mwaka 2010 utakuwa mtamu zaidi *Inshaallah*. (*Kicheko*)

Nasema hivyo kwa dhati ya nafsi yangu Mhe. Spika, hujatukosa umetulea vizuri, umekuwa mkweli kwa wote ambao umewaongoza.

Ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waliotupokea mwaka 2000. tunashukuru sana kwa uungwana wenu. Mmtufunza, mmetusaidia.

Mhe. Spika, sitachukua muda mwingi labda nilizungumze katika utangulizi la mwisho hili la maridhiano. Mhe. Spika, mimi naamini kiongozi yoyote yule ambaye anataka kuongoza watu, lazima aeleweke kwa msimamo wake. Kiongozi huongoza hasubiri kuongozwa ndio sifa ya uongozi. Nchi za Magharibi ukitaka nafasi ya uongozi wanakuuliza udogoni ulivuta bangi, ulilewa, wanataka kujua hata tabia zako za ndani ili wakuelewe wewe unayetaka kuwaongoza wao una msimamo wa aina gani, kwa uchumi, jamii na mengineyo.

Mimi nakiheshimu chama changu na ndio maana chama hiki kinakubalika na Watanzania. Na tangu uchaguzi wa mwanzo mwaka 1995 mpaka hii leo chama hiki kinaendela kupata ridhaa na kukubalika kwa wananchi. Chama cha Mapinduzi katika kuona kwake, katika kutafuta mustakabali uliokuwa mwema wa mashaka yasiokwisha kwenye ardhi hii iliyotukuka tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu Zanzibar, imeona njia sahihi na pekee kuelekea kwenye Serikali ya Pamoja.

Mhe. Spika, mimi Mansour bin Yussuf bin Himid Maftah, nieleze bayana nikiwa nimemuweka Mwenyezi Mungu mbele yangu, mimi naliunga mkono suala hilo. Na ninaamini Wazanzibari sote tutafakari, tupime, tutizame tunakotoka, twendako nini tunahitaji kwa maslahi yetu sisi na vizazi vyetu? Tutaendelea kupigana marungu, kumwagiana *acid*, kutukanana, kususiana hadi lini?

Afroshirazi misingi yake umoja, japo kuwa leo kuna watu wanasema Afroshirazi vurugu hapana, na ndio maana hata kwenye serikali ya mwanzo

Umma Party walikuwemo kwenye serikali ya Mzee Abeid Amani Karume na wengineo. Na wale ambao walijaribu kwenda kunitilia fitina kwenye jimbo langu kwamba huyu Hizbu anataka kushirikiana na Mahibu msipate tabu. Mimi nishawakabili zamani na nishawaambia msimamo wangu ni huu. Tangu mwaka 2005 niliwaambia nitakuja kwenu kwa ukweli wangu na nikikosa kwa ukweli wangu, Wallahi, Billahi, niradhi, lakini siamini hivyo.

Na ninawasihi kila Mzanzibari ifikapo tarehe 31 Julai, 2010 kama kinavyosema Chama cha Mapinduzi twende tukapige kura ya 'NDIO' tujenge Zanzibar iliyo mpya. Ninawaomba Wazanzibari wenzangu tusichukiane kwa mawazo yetu, kwa sababu kuna wengine hawalitaki kabisa. Kuna wengine wanasikiliza upepo, kuna wengine hawajalifahamu, lakini tunapaswa kuheshimiana ndio maana ikaitwa hii nchi ya demokrasia. Na unapotaka jambo basi nenda kwa maneno mazuri umshawishi mwenzio usende ukamtukana, ikiwa mtu halitaki usimtukane, jaribu kumshawishi, jaribu kumvuta, jaribu kumsihi, usimuelewe vibaya kwa sababu na yeye pia Mzanzibari ana haki na mawazo yake.

Mhe. Spika, nikiendelea sasa nije kwenye hoja. Tumezungumza wengi umeme wa vijijini. Umeme vijijini mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 1.5 sio kwa sababu hatuna njia nyengine, tumeshazungumza na wahisani wetu Norway lakini kilichokuja kutokezea kinaitwa *donor fatigue* wenzetu walikuwa wamechoka. Wameshatupa pesa nyingi sana wakasema basi jamani hebu tuacheni tuvute pumzi tufanye tathmini lakini na nyinyi tuwaone hatua mnazochukua.

Baada ya hapo tayari sisi maombi tumeshapeleka tumeshakubaliana kwamba tutayaendeleza mazungumzo hayo kumalizia maeneo yaliyobaki. Lakini na sisi tumeona tuanze kuchukua hatua ya kutenga shilingi bilioni 1.5 kwa maeneo ambayo yamesalia Unguja na Pemba waanze na hatua hiyo tusisubiri wao. Naamini wakiona hivyo watafanya haraka zaidi ya kutuunga mkono.

Hilo pia linajibu suala la Kisiwa Panza. Mhe. Spika, Kisiwa Panza ni kisiwa na gharama zake kupeleka umeme kule ni kubwa. Lakini nalo hilo tayari kwa muda mrefu mimi mwenyewe na wizara yangu tumepeleka ombi mahsusi kwa Ubalozi wa Norway kwamba tukimaliza haya ambayo tumeyafanya kwa mafanikio makubwa ipo haja tukaendeleza upelekaji umeme kwenye visiwa vyengine tukianzia na Kisiwa Panza. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi usishtuke kuona kwamba hujatengewa bajeti, majibu yake ni hayo.

Vifaa vya kuunganishia umeme havipo. Mhe. Spika, ni kweli kipindi cha karibuni kutokana na shirika kukosa mapato kwa zaidi ya miezi mitatu vifaa vilikuwa havipo lakini vimeshaanza kuingia na naamini tatizo la vifaa litaondoka hivi karibuni.

Wale ambao wamepewa fursa kuuza vifaa hivyo kwa bahati mbaya wafanyabiashara wenzetu hawa nao wanafanya mzaha, naona hatujapata hasa watu waliokusudia kuwekeza kwenye biashara hii. Lakini tutaendelea kuwaomba, kuwashajiisha, kuwaratibu ili twende vizuri.

Mhe. Tafana Kassim Mzee amezungumzia suala la wananchi kukopeshwa, kama alivyozungumza Mhe. Haji Mkema Haji Uzi na Ng'ambwa kule wananchi wamekopeshwa kuunganisha umeme. Naamini na wananchi wengine wote vijijini nao dhamira ni hiyo hiyo kila shirika litakapokuwa na nafasi limeamua kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia wananchi vijijini kuunga umeme majumbani mwao na kwenye shughuli zao nyenginezo.

Hili la deni la *TANESCO* na bei ya umeme *ZECO* lilitolewa ufafanuzi mzuri sana tu na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na Mhe. Hamad Masoud Hamad. Tatizo lipo lakini tunaendelea kulizungumza.

Umeme mbadala mimi nimelifahamu kwa nyanja mbili kwamba jamani tusitegemee cha ndugu. Mbali ya kushajiisha nguvu zetu kutafuta umeme mbadala kwa maana ya nishati mbadala jua, upepo, mawimbi ya bahari, lakini pia kila inapowezekana kuhakikisha tuna vinu vya kutosha ili likitokezea la kutokezea tuwe tunajitegemea sisi wenyewe.

Hili la viwanja Pwani Mchangani ni sahihi Mhe. Spika, maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe eneo limepimwa tangu mwaka 1997 bahati mbaya walijitokeza watu kwa makusudi kwenda kuwachochea wananchi. Kazi ya upimaji nawahakikishia wizara yangu itaendeleza tukishirikiana na mkoa na wilaya, lakini pia tutachukua jitihada za makusudi kuendelea kuwaelimisha wananchi. Kila inapopatikana ridhaa inakuwa vizuri zaidi, nguvu hazizai matunda mema. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na Serikali ya Mkoa, Wilaya na wananchi hadi ngazi ya shehia kuwaelimisha na kuifanya hii kazi haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, lililozungumzwa na wengi mafuta na gesi asilia. Mhe. Spika, nahisi tunajitia hofu wenyewe isiyokuwepo. Zanzibar imeshaamua hilo halina mjadala tena. Sawa sawa na mama kuvaa nguo ameshajistiri bado kujipodoa. Sisi tumeshaamua chombo hichi kikubwa kwa niaba ya wananchi, hakuna chombo kikubwa zaidi ya hichi kwa mujibu wa Katiba yetu kinachowawakilisha wananchi. Wananchi ndio nchi na tumeshasema hatutaki mwelekeo wetu huu. Jamani sasa Waheshimiwa Wawakilishi mnahofia nini. *(Makofi).*

Mhe. Spika, huwa ninashangaa hata katika hii semina yetu majuzi *Zanzibar Beach Resort* pale kupata viongozi wengine wanasema nchi yetu changa, rushwa wee, rushwa wee. Mimi huwa najiuliza *Yarabi.* Jambo la mwanzo tulilolifanya nafikiri tunasahau haraka. Katika sera yetu tulisema mifumo ya mikataba na mikataba yote itathibitishwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Hebu niwaulize Waheshimiwa Wajumbe kuna uwazi zaidi unaohitajika kushinda huo. Watu thamanini tunaowawakilisha wananchi wote tutakuwa wala rushwa humu ndani. Nchi gani nyengine iliyochukua maamuzi ya hekima na mazito kama hayo, nionesheni haipo, labda Norway.

Mhe. Spika: Na Spika awe anashuhudia. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Naam. Awe Mhe. Pandu Ameir Kificho amekaa pale anashuhudia na sote halafu jamani tuwalangue wananchi. Hakuna nchi iliyofanya maamuzi kama hayo. Baraza la Mapinduzi linaongozwa na Rais Amani Abeid Karume limelileta kwenu na nyinyi mmelikubali.

Mhe. Spika, tulisema tutakapoanza mifumo, maana yake mifumo ya mikataba iko mingi italetwa hapa, mtaamua mfumo huu ndio tunaoutaka sisi. Mikataba yenyewe huyo waziri atakayekuja baada ya mimi *inshaallah* yatakapokuwa tayari haya mambo kabla hajatia saini atawaletea hapa, au akishakutia saini inabidi lazima aulete hapa. Sasa kama kaweka hiyo *10 percent* au kama mnavyonambia mimi hapa pangu nitajua. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa tuna hofu ya kitu gani wakati maamuzi thabiti ya kulinda maslahi ya kila mzanzibari tumeshayachukua, maamuzi ya kusema hili letu, mafuta pangu tumeshaamua.

Pili mnahofia kwamba tumesita, jamani hatujasita, *aluta kontinua*. Hakuna mtu aliyemsubiri mwenziwe hapa. Wanafunzi 10 wanaondoka mwaka huu kwenda kusoma huko. Maalim Haroun Ali Suleiman ndio amekabidhiwa majukumu ya kuwaratibu na kuwapeleka hawa watu. Labda sasa leo na nitaona jambo la ajabu sana mkimsema Maalim Haroun hamumuamini. Najua jambo hilo sio sahihi kwa utendaji wake na uadilifu wake sote tunamuamini humu ndani. *(Makofi)*

Pili tumeshafanya *needs assessment* kuelewa nini Idara yetu ya Nishati inahitaji. Watu wameshaanza kwenda kusoma kupitia idara ile, wako waliokwenda kwenye kozi fupi, wako wengine sasa wanachukua shahada huko.

Lakini jengine tulikubaliana kwamba kuna mambo mengi na nyeti ambayo tunapaswa kuyazingatia kabla hatujaingia katika maamuzi, tukakubaliana kwamba tufanye *strategic environmental impact assessment*, yaani utafiti mkakati wa kuelewa jamii yetu itaathirika vipi kwa sekta zake zote ikiwa uchumi, kilimo, uvuvi, mazingira. Hilo jambo nalo tumeshazungumza na Serikali ya Norway wameshakubali na hivi sasa anatafutwa Mshauri Mwelekezi aanze hiyo kazi. Tunategemea ndani ya miezi sita ijayo kazi hii itakuwa imemalizika.

Kazi hii sasa itatupa dira kwamba mkichimba mafuta kwenye bahari taathira yake hii, faida zake hizi. Mkichimba nchi kavu watakaoathirika ni hawa, ikiwa matumbawe, ikiwa wavuvi, ikiwa wakulima wa mwani na kadhalika. Utalii utaathirika hivi, usafirishaji baharini utaathirika hivi, mazingira yenu yataathirika hivi. Litatuwekea wazi kwa kila sekta, sasa hilo ndio litatupa mwongozo wa hatua zinazofuata.

Kwa hivyo, niwahakikishie hakuna mtu anayemsubiri mwenziwe hapa. Ninashangaa sasa watu wazima tunaanza kusema aaa tunaomba, hakuna aliyemuomba mtu, barua imesema hili jambo litoke hakuna aliyeomba. Kuna maamuzi yamefanyika lakini jamani tuelewe huu Muungano wetu, ni wetu sote, tuna taratibu ambazo tumetegemea hizo zifuatwe za kistaarabu ziende. Lakini huku tumeshakubaliana sisi yetu yanaendelea. Sasa nafikiri kwa maelezo hayo mtaridhika Waheshimiwa Wajumbe kwamba hakuna aliyemsubiri mtu, sisi *aluta kontinua*.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limezungumzwa na wengi ili nipate kumaliza ndani ya dakika tano zijazo ni huu mradi wa *MDRI (Multilateral Debt Relief Initiatives).* Fedha zilizotengwa kwenye mradi huu ni shilingi bilioni moja. Tumeshanunua mabomba mengi sana yapo, pampu ziko njiani. Mabomba haya yameletwa mahsusi kumaliza matatizo kwenye majimbo hasa ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Hapa alipazungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na majimbo mengine Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo mradi huu wa Wajapan haukufika. Mabomba yapo na kazi hizo zinaendelezwa.

Maeneo mengineyo ambayo mitandao ya siku nyingi, mabomba yaliyokuwepo mengi sana tutakwenda hatua kwa hatua na kuanza kutatua matatizo kwenye shehia hizi.

Jengine lililozungumzwa ni uchafu wa Mji Mkongwe. Lakini nataka nieleze kwamba Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe kazi yake sio usafishaji wa Mji Mkongwe, hayo ni mamlaka ya Baraza la Manispaa. Lakini katika hii sheria ambayo mmeipitisha hapa inaipa mamlaka meno kidogo zaidi kwa ajili ya

kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Lakini hasa usafi wa mazingira na mengineyo ni bado itaendelea kuwa kazi ya Baraza la Manispaa.

Uuzaji wa nyumba za vijijini. Zoezi la uuzaji wa nyumba za vijijini halijasita linaendelea na wengine tayari wameshauziwa na kupewa hati zao kwa Unguja na Pemba.

Magofu iliamuliwa na Baraza hili hili kwamba maamuzi yale yafanywe na Wakuu wa Mikoa kwa kushirikiana na hizo kamati zao walizokuwanazo huko. Kuna baadhi wameshatanguliza maombi hayo, kuna wengine bado.

Jambo jengine alilozungumza Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na niliona kwamba liligusa wengi ni hili eneo linalozungumzwa pale ubavuni mwa nyumba ya Bakhressa, Shehia ya Pwani Mchangani anapokuwa anaegesha magari yake ya *ice-cream.*

Mhe. Spika, siwezi kulizungumzia hili suala kwa maana liko Mahakamani na sijapata taarifa juu ya matokeo ya pale. Lakini ninachoweza kusema kwamba lina historia ndefu, huyu aliyekuwa na hati hivi sasa amerithi hati kutoka kwa wengineo. Kwa hiyo, kwa upande mmoja uhalali anao lakini mpaka Mahakama iamue huko hatuwezi kuingilia mhimili ule.

Kuchelewa kwa kesi za Mahakama ya Ardhi. Mhe. Spika, kesi za Mahakama ya Ardhi kuna maendeleo mazuri tu. Tukilinganisha na mwaka uliopita basi mwaka huu tumefanya vizuri zaidi. Tunategemea mwaka ujao wa fedha tukishakuipata Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, usikilizaji wa kesi na maamuzi zitakuwa kwa haraka zaidi.

Sasa Mhe. Spika, uniruhusu kwa dakika tano niguse suala moja moja la wale ambao sijawagusa kwa pamoja. Mhe. Haji Faki Shaali mengi nimeyajibu kwa pamoja lakini mita za TUKUZA tutaziongeza. Lile jadweli ulilolitaja ni sahihi kweli kompyuta iliruka.

Mhe. Abdulla Juma Abdulla masuala ya maji Tundauwa. Tumedhamiria kwamba hatua kwa hatua tutafika huko. Mhe. Said Ali Mbarouk alizungumzia mradi wa *African Development Bank (ADB)* kuhimizwa, tunaendelea kufanya hivyo. Kitengo cha *maintenance* tumekusikia mheshimiwa. *Transformer* za akiba na masuala mengineyo tutayazingatia.

Mhe. Spika, nayagusia yale ambayo pengine wawakilishi nilihisi pointi ile imemgusa kwa karibu zaidi, kwa hiyo wengine wasione nawaruka nimejaribu kuyazungumza kwa pamoja.

Mhe. Subeit Khamis Faki alizungumzia Chuo cha Kiislam *transformer*. Tunamhakikishia kwamba kazi hiyo tutaifanya. Mhe. Ame Ussi Juma ninamshukuru sana kwa usimamizi wake wa mradi wa maji Kigongoni, ustahamilivu wake kwa hali ya maji Nungwi. Tutaendelea kushirikiana nae ili kutatua matatizo ya pale.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin amezungumzia *transformer* ya Mtondooni kuungua siku nyingi, nalo hilo tutalishughulikia pamoja na hayo mengineyo.

Mhe. Haji Mkema Haji amezungumzia kisima cha Kibele kwamba kila kitu kipo lakini wahudumu hakuna. Kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa vile ataanza kuruhusu uajiri basi tutahimiza kituo chako hichi kipate wahudumu.

Tunakushukuru kwa ustahamilivu wako maana yake sasa hivi Unguja nzima imehamia Jumbi. Tunajua una matatizo mengi lakini tunakushukuru kwa namna unavyotusaidia na kutustahamilia, namna unavyotusaidia kutatua migogoro ya ardhi pale na kuwatuliza wananchi wa jimbo lako. Tunajua nchi yako imekutwisha mzigo mkubwa sana kwa eneo lile lakini tunakushukuru.

Pia tunakushukuru kwa namna unavyosimamia miradi ya umeme na maji katika jimbo lako. Kwa ujasiri wako huo na namna unavyojituma Mhe. Haji Mkema Haji nakuomba unikubalie kama tulivyofanikisha mengine, basi na haya tutashirikiana na tutayafanikisha *inshaallah*. Kipindi hichi cha miaka mitano Mhe. Mkema umefanikisha mengi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alizungumzia kwa sababu ya umeme kuruka. Kipindi cha mwanzo ilikuwa ni wanyama na *transformer* zenyewe kupatiwa *turning* zake. Lakini kila siku zikenda hali hiyo itakaa sawa.

Mhe. Ali Abdalla Ali alizungumzia ukaguzi wa eka na hatimaye patafanywa nini, aliyeuza atapewa nyengine. Hapana hapewi nyengine, ndio kishauza ya kwake aliyokuwanayo ya kumpa hatuna. Wanaoendelea kuuza wanafanya kosa na tumewatahadharisha zamani kwamba haya yatafika watakuja kukosa mtoto na maji ya moto. Bora mtu eka yake abaki nayo alime, kama kajenga kajijengea nyumba yake yeye mwenyewe ya kuishi hapo.

Pia Mhe. Ali Abdalla Ali ameshauri tangi la Michungwa miwili nalo litazamwe. Tumekubali mheshimiwa pamoja na ushauri wako mwengine. Wewe pia tunakushukuru ulivyotusaidia kubeba mradi wa *ACRA* kwa sababu kwako ndio mlangoni. Tunakushukuru kwa ulivyotusimamia uchimbaji wa visima, matangi, usambazaji wa mabomba, umefaidika wewe lakini pia

umehakikisha na wenzio wanafaidika baada yako. Mhe. Ali tunakushukuru sana. Ushauri wako wa kituo cha Ras Kiromoni tunaupokea. *(Makofi)*

Mhe. Mzee Ali Ussi, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, nawe tunakushukuru sana kwa namna ulivyosimamia mradi wa *TASAF*. Tunakubali mradi huu umechelewa mno na tutakusaidia ili tuukwamue. Tunakushukuru pia kwa namna ulivyosaidia miradi mingine ya umeme na maji ndani ya jimbo lako. Naamini wananchi wa Jimbo la Chaani watakulipa kwa juhudi zako hizo. Hizi kasoro kasoro ziliopo tutaendelea kukusaidia.

Mhe. Salim Abdulla Hamad tunaupokea ushauri wako na tutaendelea kushirikiana na wewe. Mhe. Abass Juma Muhunzi alizungumzia tatizo la barabara zinazopita baina ya viwanja ni tatizo la nani. Kwa kweli ni *multilateral* lakini bado nakubaliana na wewe kwamba linahitajika kufanyiwa kazi kwa karibu zaidi ili tuondoshe tatizo hilo na tutazingatia zaidi katika upimaji wa maeneo ya burudani.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk tunakushukuru sana kwa pongezi zako na tunakubaliana na wewe kwamba kuna wananchi wenzetu wanatumia maji kwa *israf*, wengine wanayatafuta, wengine wanamwagia matofali masaa 24 barabarani hata haya hawaoni. Tunawaomba Mamlaka ya Maji tupokee ushauri wa Mhe. Amina na marufuku kwa wale ambao wanatumia maji kwa *israf*. Jipangeni muanze kuchukua hatua ili maji yaenee kwa watu wote. Tumepitisha sera na sheria tuizingatie.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis tunapokea ushauri wako. Majenereta ya Pemba hivi sasa yanaendelea kutengenezwa, moja zima, moja linaendelea kutengenezwa litakuwa tayari hivi karibuni. Jengine spea zake zimeshaagiziwa Uingereza pengine ndani ya miezi miwili mitatu yote matatu yatakuwa yako tayari kusubiri hitilafu ikitokezea. Ushauri wako wa tangi la Konde lililokuwa bovu nalo tunazingatia.

Walionichangia kwa maandishi naomba kwa hisani zao wakubali kwamba nimepokea ushauri wao na tutayazingatia. Labda la Mhe. Ame Mati Wadi kwa vile moja liko la siku nyingi nimsaidie ili apate ufafanuzi.

Mhe. Ame Mati Wadi alizungumzia huu mradi wa Kiashange pale ambao umesinzia sinzia kwa siku nyingi. Nakubaliana nae na tutafanya kazi ya kuisaidia hii hali na hasa umeme Shehia ya Kijini. Nakubaliana nae kwamba Shehia ya Kandwi palikuwa na ahadi ya wizara, lakini kwa bahati mbaya sana ahadi hiyo haikutekelezwa kikamilifu. Mhe. Mati tukutake radhi maana yake tumekuahidi siku nyingi. Unapoahidiwa mbele za wananchi wako linakuwa la

kwako sisi tuko mbali. Lakini wenzangu wananisikia na nimekwisha kuwaagiza, nakuomba utustahamilie lakini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu kazi hii tutaifanya.

Masuala ya maji nimeshayazungumza. Maji Nungwi, Matemwe yapo kwenye mradi ule wa *African Development Bank (ADB),* mikataba tumeshatia saini kazi inaendelea, tunasubiri sasa utekelezaji. Naamini katika mwaka ujao wa fedha utekelezaji huo utaanza na pengine katika bajeti ijayo Mwenyezi Mungu akikujaalia kuwa hai kuichangia utakuwa unazungumzia mengine katika kuwasogezea wananchi wa jimbo lako maendeleo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa basi Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 25 - WIZARA YA MAJI, UJENZI, NISHATI NA ARDHI

Kifungu 03	-	Afisi Kuu Pemba	62,480,000
Kifungu 05	-	Idara ya Ujenzi	37,629,000
Kifungu 07	-	Hifadhi ya Mji Mkongwe	20,900,000
Kifungu 09	-	Idara ya Ardhi na Usajili	1,786,610,000
Kifungu 10	-	Idara ya Upimaji na Mipango Miji	362,000,000
Kifungu 11	-	Idara ya Nyumba na Makaazi	92,000,000
		Jumla ya Fungu	**2,361,619,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 25 - WIZARA YA MAJI, UJENZI, NISHATI NA ARDHI

Kifungu 03	-	Afisi Kuu Pemba	740,029,000

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nipate ufafanuzi. Mimi nimechangia kwa maandishi naruhusiwa kutoa hoja au siruhusiwi?

Mhe. Mwenyekiti: Kimsingi huruhusiwi na hasa hasa katika suala zima la kuzuia fungu, hiyo ndio huruhusiwi kabisa kwa sababu unatakiwa uwe umetoa taarifa mapema katika kuchangia. Sasa kama ni maelezo tu ya kawaida unaruhusiwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, hili si kuzuia fungu ni maelezo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya endelea.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, maelezo yangu ilikuwa ni sera ya ukopeshaji wa umeme kutokana na matatizo makubwa waliyonayo wananchi wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri alizingatie sana suala hili, wananchi wanahitaji sana kukopeshwa huduma ya umeme ili waweze kuutumia.

Mhe. Mwenyekiti: Ni ombi tu, Mhe. Waziri sijui unasemaje?

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, nalipokea na tutalizingatia. Tunaifanya hiyo kazi, hii miezi mitatu ambayo tumekosa umeme kasi yake imepungua. Lakini tunamshukuru, tunayapokea, tutayazingatia kwa karibu zaidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwenye Shirika la Umeme nilitoa masikitiko yangu makubwa kwa watu wa Mwambe wanavyofanyiwa. Nimemuelewa Mhe. Naibu Waziri, nimeyafahamu maelezo ya Mhe. Waziri, nimepokea barua mbili za ushauri nasaha za Barazani humu kwamba nisizuie fungu ninazikubali. Lakini nimeona nisimame nifanye kazi mbili kubwa.

Kwanza sikusudii kuzuia fungu na ninafuta kauli yangu. Lakini nimeona niseme kwamba nililazimika kulalamika kwa sababu watu hao waliofanyiwa kadhia hii walikuwa wamekwenda polisi moja kwa moja. Sasa kwenda polisi maana yake ni kushtaki na kutia aibu Shirika la Umeme.

Kwa hvyo, namuomba Mhe. Waziri sitozuia fungu lakini tukitoka nje basi tuyamalize masuala haya kwa maslahi ya Shirika la Umeme.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba aende polisi, ikiwa kuna watu wanatumia Shirika la Umeme kufanya ubadhirifu pahali pao ni polisi. Sio suala la kumalizana sisi. Nakutaka radhi sana kwa hayo yaliyotokezea, sisi tutafanyakazi ndani ya wizara na shirika kusawazisha. Lakini ikiwa kuna watu wamechukua pesa za watu huko kwa jina la Shirika la Umeme na kazi hiyo haijafanywa huu mwaka wa pili, basi pahali pao ni polisi.

Kwa hivyo, mimi nakushauri ukiwa ni mwakilishi wa wananchi hao, nenda kawaelekeze polisi ili vyombo vya dola navyo vichukuwe hatua na wao watatusaidia sisi ili kurekebisha maovu ambayo yamo kwenye taasisi zetu. Lakini na sisi kwa upande wetu tutafanyakazi ili kulirekebisha hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri namuamini na kauli yake naiunga mkono na nitafanya kazi hiyo.

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	2,217,071,000
Kifungu 05	Idara ya Ujenzi	452,391,000
Kifungu 07	Hifadhi ya Mji Mkongwe	213,905,000
Kifungu 08	Idara ya Nishati	107,589,000
Kifungu 09	Idara ya Ardhi na Usajili	242,969,000
Kifungu 10	Idara ya Upimaji na Mipango Miji	316,957,000
Kifungu 11	Idara ya Nyumba na Makaazi	183,267,000
Kifungu 12	Mahakama ya Ardhi	111,018,000
Kifungu 13	Idara ya Utawala wa Ardhi	133,866,000
Kifungu 14	Msajili wa Ardhi	101,938,000
Jumla ya Fungu		**4,821,000,000**

Kifungu 04 Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Muhyiddin Moh'd Muhyiddin: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la *transformer* ya Tondooni. Maelezo ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na waziri nimeyaelewa, lakini kinachonisikitisha kwamba nimepokea taarifa hivi punde kuwa ilipatikana *transformer* moja kule

Pemba na *transformer* hiyo inataka kupelekwa Mgelema. Wakati *transformer* ya Mgelema imeharibika hivi karibuni kuliko ile ya Mtondooni. Sasa naomba kupata ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Muhyiddin Moh'd Muhyiddin kwa umakini wake na ukali wake katika kutetea wananchi wa jimbo lake.

Mhe. Mwenyekiti, *transformer* ya Mgelema ni mahususi kwa mradi wa maji ule. Tunaelewa tuna tatizo la *transformer* hivi sasa. Mngeyasikia hapo Jimboni kwangu mimi Chukwani nafikiri mngenionea huruma. Nafikiri ningekuwa waziri naweza kuchangia, basi katika hotuba yangu mwenyewe ningechukua kama dakika 15 nalichangia Shirika la Umeme kwa kutafuta *transformer*.

Mhe. Mwenyekiti, ziko *transformer* ambazo ziko njiani na wako wanaandaa mipango hivi sasa kuagizia nyengine ndani ya kipindi cha hii miezi mmoja au miwili, ili hii hali tuliyokuwa nayo mbali kwa Unguja na Pemba ya *transformer* hivi sasa kuiweka sawa. Tatizo kubwa lililokuja kujitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi ambacho umeme ulikatika hapa Unguja, tulianza kuyaona mambo mapya. Huko nyuma tulikuwa tunaibiwa waya tu. Safari hii ulipokatika umeme basi mafuta yale kwenye *transformer* yalianza kugidwa. Mhe. Mwenyekiti, nasikia Bara wanapikia chipsi, wanajichubua na wanayauza. Kwa hivyo, tumepata hasara kubwa sana. Imebidi mbali ya kukosa mapato kwa miezi yote mitatu, lakini taathira kwenye miundombinu hasa kwenye ma-*transformer* imeturejesha nyuma mno.

Kwa hivyo, tunawaombeni Waheshimiwa Wajumbe tustahamilieni vijana wanaendelea na mikakati ya kuweza kuirekebisha hii hali. Lakini itachukua zaidi ya mwezi mmoja, tunakiri, tunawataka radhi na tustahamilieni.

Mhe. Muhyiddin Moh'd Muhyiddin: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kule kuna shughuli maalum ya maji na maji ni uhai, basi nakubaliana na Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kile kijiji cha Machengwe ambako watu wana matatizo ya umeme kwa muda mrefu na tumejitahidi mpaka tumepata nguzo 10, bado nguzo nne kutokana na maelekezo ya shirika.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba itawezekana kunisaidia angalau wale watu wafaidike au la, sikupata maelezo yoyote.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwekilishi atakubaliana na mimi kwamba kwenye Jimbo lake tumefanyakazi kwa karibu sana. Kijiografia jimbo lake gumu, tunajua watu wake wanapata tabu, lakini tumefanya naye jitihada kubwa ili kutatua matatizo yake mengi.

Mhe. Mwenyekiti, ingekuwa wepesi kwangu hapa kuanza kuahidi hapa nguzo mbili au nguzo kumi basi ningeweza kufanya hivyo. Lakini sio utaratibu, sisi tunataka kumsaidia kila mwakilishi hasa aliyeunganisha nguvu zake yeye na wananchi wakapiga hatua, kwa sababu sisi wameshatupunguzia kazi na mnatutafutia wateja.

Mhe. Mwenyekiti, huwa tunayakariri haya yote, halafu tunapokaa kitako baada ya kikao hiki tunatizama lipi tunaweza kulifanya mwanzo. Dhamira yetu ni kuwasaidia nyote. Sasa nakuomba mzee wangu ukubali kwamba nimekusikia, kama tulivyoyafanikisha mengine, basi na haya kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutayafanikisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia mwanangu tuendelee.

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	35,003,480,000
Kifungu 05	Idara ya Ujenzi	374,000,000
Kifungu 08	Idara ya Nishati	22,491,873,000
Kifungu 10	Idara ya Upimaji na Mipango Miji	12,033,933,000
	Jumla ya Fungu	**69,903,286,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kutoa mashirikiano makubwa katika kuendeleza majukumu yetu na mpaka hapa tusitishe shughuli zetu. Kwa maana hiyo basi naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni wakati ambapo tutamsikiliza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ili na yeye aje awasilishe hotuba ya makadirio ya wizara yake.

(Saa 6:40 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Makadirio ya Mapato na Matumizi – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liingie kwenye Kamati ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana kwa mara nyengine tena katika kikao cha bajeti cha Baraza lako tukufu. Hii ni bajeti ya kumi tokea kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Sita.

Mhe. Spika, kikao cha Bajeti cha mwaka huu kinafanyika wakati pamefikiwa maridhiano na maelewano kati ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kukubaliana kuondoa hitilafu na tafauti za vyama vyao vya siasa na kuamua kushirikiana na kuweka utaifa mbele kwa maslahi ya wananchi wote na kuongeza kasi ya maendeleo ya Taifa letu la Zanzibar.

Hali hii imepelekea Chama cha CUF kumtambua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Rais halali wa Zanzibar aliyechaguliwa na wananchi wengi. Hatua ambayo imeleta hali ya kuaminiana na hatimae kupitishwa kwa Mswada wa Sheria wa Kuundwa kwa Serikali ya Kitaifa baada ya uchaguzi ujao wa Rais na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Matumaini yangu kwamba wananchi watajitokeza kwa wingi kupiga kura ya maoni, hatimae kukubali kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mwenyezi aidumishe hali hii kwa maslahi ya taifa letu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri mkubwa wa uongozi wako katika kuliongoza Baraza hili tukufu, kwa misingi ya uadilifu na uaminifu mkubwa na hatimaye kutufikisha salama, kwa mafanikio katika kikao hiki cha mwisho cha bajeti katika awamu hii.

Mhe. Spika, naomba kwa dhati kabisa kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa michango yao mizuri waliyoitoa pamoja na mshikamano na mashirikiano waliyoyaonesha katika kuleta maendeleo ya elimu, katika kipindi chote cha miaka tano iliyopita *(Makofi)*.

Mhe. Spika, napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Ali Suleiman Ali kwa kutuongoza vyema na kutushauri ipasavyo. Wajumbe wa kamati hii waliweza kuichambua na kujadili hotuba ya bajeti kwa undani kabisa na mwishowe kuipitisha. Pia wameweza kuishauri wizara yangu ipasavyo kila walipotembelea shughuli zinazosimamiwa na Wizara yangu.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza kwa dhati msaidizi wangu, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Khamis Jabir Makame kwa mashirikiano makubwa aliyonipa, katika utekelezaji majukumu ya Wizara *(Makofi)*.

Aidha natoa shukrani zangu za dhati kwa watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara yangu wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi na wengine wote waliosalia kwa utendaji wao mzuri wa kazi na mashirikiano mema hadi kufikia leo hii na kuniwezesha kuisoma hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza viongozi wa Bodi ya Elimu, Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya, Kamati zote za Skuli na wazazi wote kwa michango yao ya hali na mali, katika kuziendeleza skuli zetu na hatimaye tukafanikiwa kupata maendeleo makubwa ya kielimu.

Mhe. Spika, kabla ya kuelezea utekelezaji wa mipango ya elimu ya mwaka 2009/2010 na matarajio kwa mwaka 2010/2011, napenda kueleza angalau kwa ufupi maendeleo tuliyoyapata katika kipindi cha miaka 10 (2001 – 2010) chini ya uongozi wa Dkt. Abeid Abeid Karume, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi *(Makofi)*.

Hali ya Maendeleo ya Elimu kwa Kipindi cha Miaka 10 (2001 – 2010)

Mhe. Spika, idadi ya taasisi mbali mbali za elimu, za serikali na za watu binafsi zimeongezeka kutoka 340 mwaka 2001 hadi kufikia 657 mwaka 2010.

Mhe. Spika, idadi ya skuli za maandalizi imeongezeka kutoka 121 (22 za serikali) mwaka 2001 hadi kufikia 238 (27 za serikali) mwaka 2010. Ongezeko dogo kwa upande wa skuli za serikali imetokana kuwa hadi mwaka 2006 ngazi hii ya elimu haikuwa sehemu ya elimu ya lazima. Pia baadhi ya skuli za msingi na msingi na kati za serikali zimeandikisha wanafunzi wa elimu ya maandalizi katika skuli zao. Idadi ya skuli za msingi na kati za serikali zenye madarasa ya maandalizi ni 34 (28 kwa Unguja na 6 kwa Pemba).

Mhe. Spika, idadi ya wanafunzi waliojiunga na elimu ya maandalizi imeongezeka kutoka wanafunzi 13,156 mwaka 2001 na kufikia wanafunzi 29,732 mwaka 2010. Pia asilimia ya uandikishaji wa wanafunzi imeongezeka kutoka asilimia 12.7 mwaka 2001 hadi kufikia asilimia 33.9 mwaka 2010. Jadweli (a) inatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli (a)

Mwaka	Uandikishaji katika ngazi ya Elimu ya Maandalizi	Kima cha Uandikishaji
2001	13156	12.7
2002	15004	16.0
2003	16185	14.7
2004	15601	13.8
2005	18538	15.9
2006	16326	13.9
2007	21538	22.2
2008	21696	20.9
2009	21218	17.8
2010	29732	33.9

Mhe. Spika, katika kuongeza ushiriki wa watoto katika ngazi ya elimu ya maandalizi, Wizara ilianzisha mradi wa utoaji wa elimu ya kwa njia ya Redio ambao unatoa elimu kwa watoto wenye umri wa elimu ya maandalizi na darasa la kwanza. Kituo hiki kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 3 Mei 2007.

Mhe. Spika, kwa upande wa Elimu ya Msingi, idadi ya skuli zimeongezeka kutoka skuli 84 mwaka 2001 na kufikia skuli 299 kwa mwaka 2010. Ukuaji huo umetokana na ongezeko la ushiriki wa watoto katika ngazi hii kutoka wanafunzi 172,465 mwaka 2001 na kufikia 226,812 mwaka 2010, ambayo ni sawa na asilimia 112.1. Jadweli (b) inatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli (b)

Mwaka	Uandikishaji katika ngazi ya Msingi	Kima cha Uandikishaji
2001	172,465	94.6
2002	184,382	98.1
2003	191,959	99.1
2004	199,988	100.3
2005	208,283	101.3
2006	209,241	101.6
2007	214,096	104.6
2008	216,731	104.4
2009	220,819	106.8
2010	226,812	112.1

Mhe. Spika, idadi ya wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi na kati imeongezeka kutoka 205,138 mwaka 2001 hadi kufikia 275,695 mwaka 2010. Aidha kima cha uandikishaji katika ngazi hii kimeongezeka kutoka asilimia 84.2 mwaka 2000 hadi asilimia 105.9 mwaka 2010. Jadweli (c) inatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli (c)

Mwaka	Uandikishaji Dar. 1-Kidato cha 2	Kima cha Uandikishaji
2001	205,138	84.2
2002	225,921	87.7
2003	230,603	89.6
2004	249,851	91.5
2005	252,205	92.6
2006	267,027	91.9
2007	272,967	94.2
2008	279,512	95.7
2009	271,958	103.0
2010	275,695	105.9

Mhe. Spika, kwa upande wa ngazi ya elimu ya sekondari ya fursa (Kidato cha 3 – Kidato cha 4), ushiriki wa watoto umeongezeka kutoka 6,436 mwaka 2001 na kufikia 31,125 mwaka 2010, kima hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 51.5.

Uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya Sekondari ya juu (Kidato cha 5 – Kidato 6) pia umeongezeka kutoka 716 mwaka 2001 na kufikia 4,091 mwaka 2010. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaofaulu mitihani ya Kidato cha nne na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano na cha Sita.

Mhe. Spika, ongezeko la wanafunzi katika ngazi mbali mbali limepelekea kuongezeka kwa idadi ya walimu kutoka walimu 6,457 mwaka 2001 na kufikia 10,997 mwaka 2010. Asilimia ya walimu wasiosomea imepungua kutoka 20.2 mwaka 2001 na kufikia asilimia 6 mwaka 2010. Jadweli (d) inatoa ufafanuzi. Aidha uwiano wa wanafunzi na walimu umepungua kutoka wastani wa wanafunzi 33 hadi 28 kwa mwalimu mmoja.

Jadweli (d)

Mwaka	Idadi ya Walimu	Asilimia ya walimu wasiosomea katika skuli za Serikali	Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mmoja
2001	6457	20.2	33
2002	6731	19.1	31
2003	7393	18.0	32
2004	7633	14.7	31
2005	9335	12.0	28
2006	9055	12.0	29
2007	8998	11.0	30
2008	10485	10.1	29
2009	10727	7.0	28
2010	10997	6.0	28

Mhe. Spika, mitihani ni moja ya kigezo kikubwa kinachotumika katika kupima ubora wa elimu itolewayo visiwani mwetu. Ubora wa elimu umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyodhihirika katika matokeo ya mitihani ya Taifa. Kwa upande wa mitihani ya kidato cha 2, idadi ya wanafunzi waliofaulu na kuteuliwa kuendelea na masomo imeongezeka kutoka 2,960, ikiwa sawa na asilimia 31.6 ya watahiniwa mwaka 2000/2001 hadi kufikia 11,515, sawa na asilimia 54.2 mwaka 2009/10.

Jadweli (e): Watahiniwa wa Kidato cha pili

Mwaka	Idadi ya Watahiniwa	Idadi ya Waliofaulu	Asilimia ya kufaulu
2000/01	9355	2960	31.6
2001/02	8285	3125	37.7
2002/03	9969	4001	40.1
2003/04	10835	4672	43.1
2004/05	12348	5357	43.4
2005/06	13355	6359	47.6
2006/07	15003	7581	48.0
2007/08	14603	7439	50.9
2008/09	29852	16082	53.9
2009/10	21255	11515	54.2

Mhe. Spika, katika mtihani wa Kidato cha 4, idadi ya watahiniwa imeongezeka kutoka 2,806 mwaka 2000 hadi 8,725 mwaka 2009. Idadi ya watahiniwa waliofaulu nayo imeongezeka kutoka 2,169 mwaka 2000 ikiwa sawa na asilimia 77.3 na kufikia 7,066 mwaka 2009 ikiwa sawa na asilimia 81.0. Aidha idadi ya wanafunzi waliopata daraja la kwanza (*Division 1*) imeongezeka kutoka wanafunzi 18 mwaka 2000 na kufikia 40 mwaka 2009. Jadweli (f) inatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli (f): Watahiniwa wa kidato cha nne

Mwaka	Idadi ya Watahiniwa	Idadi ya Waliofaulu	Asilimia ya kufaulu	Waliofaulu Daraja la kwanza	Waliofaulu Daraja la pili
2000	2806	2169	77.3	18	31
2001	3127	2489	79.5	18	36
2002	3285	2799	85.2	34	59
2003	3539	3267	92.3	59	58
2004	4286	4046	94.4	43	95
2005	5389	4897	90.9	55	104
2006	6334	5014	79.2	50	118
2007	7250	6136	84.6	121	169
2008	8446	6533	77.4	64	124
2009	8725	7066	81.0	40	166

Mhe. Spika, matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita yanaendelea kuwa mazuri, licha ya kupanda na kushuka kwa baadhi ya miaka. Katika mwaka 2000/01, jumla ya watahiniwa 300 walifanya mtihani huo na watahiniwa 270 walifaulu ikiwa sawa na asilimia 90.0 ya watahiniwa wote. Katika mwaka 2009/2010, kati ya wanafunzi 2,308 waliofanya mtihani, watahiniwa 1940 walifaulu ikiwa ni sawa na asilimia 84.1. Jadweli (g) inatoa ufafanuzi zaidi.

Jadweli (g) Watahiniwa wa kidato cha Sita

Mwaka	Idadi ya Watahiniwa	Idadi ya Waliofaulu	Asilimia ya kufaulu	Waliofaulu Daraja la kwanza	Waliofaulu Daraja la pili
2000/01	300	270	90.0	6	41
2001/02	355	343	96.6	14	60
2002/03	261	258	98.9	20	78
2003/04	411	404	98.3	46	123
2004/05	522	493	94.4	36	107
2005/06	1005	970	96.5	118	253
2006/07	1566	1249	79.8	26	115
2007/08	1432	1185	82.8	15	102
2008/09	1959	1659	84.7	39	131
2009/10	2308	1940	84.1	43	189

Mhe. Spika, elimu mjumuisho ilianzishwa rasmi mwaka 2004 kwa kuanzia na skuli 30 za majaribio za Unguja na Pemba, Idadi hiyo imeongezeka hadi kufikia 86 mwaka 2009/10. Aidha idadi ya wanafunzi nayo imeongezeka kutoka 896 mwaka 2004 na kufikia 3,883 mwaka 2009/10.

Kutokana na mahitaji ya walimu wa elimu mjumuisho, mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho yameanzishwa rasmi katika Chuo cha Kiislam Mazizini katika mwaka wa masomo 2006/2007.

Mhe. Spika, Wizara inaendelea kufungua vituo zaidi vya elimu Mbadala katika Skuli mbali mbali za Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapatia elimu vijana wenye umri kati ya miaka 13 na kuendelea ambao hawakubahatika kuandikishwa skuli, au waliacha masomo njiani kutokana na sababu mbali mbali.

Katika kipindi cha Miaka kumi iliyopita, idadi ya vituo vinavyotoa elimu Mbadala vimeongezeka kutoka vituo 3 mwaka 2000 na kufikia vituo 49 mwaka 2009/10. Aidha idadi ya wanafunzi katika vituo hivyo nayo imeongezeka kutoka 80 mwaka 2000 hadi kufikia 1,289 mwaka 2009/10.

Mhe. Spika, Sera mpya ya Elimu ilitayarishwa na kuanza kutumika rasmi mwaka 2006. Mabadiliko makubwa katika Sera hii ukilinganisha na Sera iliyopita ya mwaka 1995 ni kubadilika kwa mfumo wa elimu kutoka 7-3-2-2-3 na kuwa 2-6-4-2-3. Katika mfumo huu mpya muda wa elimu ya lazima umeongezeka kutoka miaka 10 hadi miaka 12.

Mabadiliko haya yamefanya elimu ya maandalizi ya miaka miwili kuwa ni sehemu ya elimu ya msingi, elimu ya msingi kutolewa kwa miaka sita, kufutwa kwa darasa la maandalizi ya sekondari (*OSC*) na elimu ya sekondari ya miaka minne kuwa ni sehemu ya elimu ya lazima.

Mabadiliko mengine ni kuimarishwa kwa mfumo wa ukaguzi wa elimu, kuimarisha ubora wa elimu kupitia marekebisho ya mitaala na Mihutasari yake, Mafunzo ya Walimu, na Upatikanaji wa Vifaa vya kusomeshea na vya kujifunzia.

Mhe. Spika, utekelezaji wa sera hii umeshaanza kwa kuandaliwa na kuanza kutumika mtaala mpya wa elimu ya maandalizi na wa ngazi ya elimu ya msingi, ambapo wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza mwaka wa 2010 wameshaanza kutumia mtaala huo wa msingi wa miaka 6 ya elimu ya msingi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita maendeleo makubwa yamepatikana katika Hifadhi za Nyaraka na Makumbusho na Mambo ya Kale. Ukarabati mkubwa na mdogo umefanyika katika makumbusho zetu zote za Unguja na Pemba na vifaa mbali mbali vimenunuliwa na kusambazwa katika makumbusho hayo. Aidha, njia za kisasa za kutunza nyaraka na kumbukumbu kwa kutumia kompyuta imeanzishwa na inaendelea vizuri.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la skuli, wanafunzi na walimu matumizi ya sekta ya elimu nayo pia yameongezeka kutoka shilingi 5,934,400,000/= mwaka 2000/01 ikiwa ni sawa na asilimia 12.5 ya bajeti ya serikali hadi kufikia shilingi 33,224,000,000/= mwaka 2009/10, sawa na asilimia 15.6 ya Bajeti ya Serikali.

Kuongezeka kwa matumizi ya serikali kwa sekta ya elimu kunadhihirisha namna serikali yetu ilivyotoa kipaumbele kwa sekta ya elimu. Ninatoa shukurani zetu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuipa kipaumbele sekta ya elimu. Pia shukurani maalum ziende kwa uongozi wa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mashirikiano makubwa wanayotupa *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mafunzo kwa walimu wa Maandalizi na wa darasa la kwanza katika kutumia mihutasari mipya yametolewa. Mafunzo mengine mbali mbali kwa walimu wa Hisabati na Sayansi yametolewa na yanaendelea kutolewa; kambi mbali mbali za sayansi kwa ajili ya kuinua kiwango cha elimu ya sayansi kwa watoto wa kike zimeshaanza kwa Unguja na Pemba.

Vile vile Ujenzi wa skuli mpya na madarasa mapya kwa skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari umefanyika na unaendelea; Warsha mbali mbali za stadi ya maisha na mapambano dhidi ya maradhi ya UKIMWI zimetolewa na zinaendelea kutolewa kwa wanafunzi na walimu Unguja na Pemba; wakaguzi wa elimu kwa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya kazi zao na matumizi ya kompyuta.

Wakaguzi pia wamepatiwa nyenzo za kufanyia kazi kama vile usafiri, kompyuta, printa na fotokopia kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi za ukaguzi. Walimu wakuu wa skuli zote za Unguja na Pemba na baadhi ya wajumbe wa kamati za skuli nao wamepatiwa mafunzo juu ya uongozi na uendeshaji wa skuli n.k.

Mhe. Spika, katika kutekeleza kwa ufanisi Sera ya Elimu ya mwaka 2006, wizara imeandaa mpango mkuu wa muda mrefu wa miaka nane (8) wa utekelezaji wa sera hiyo pamoja mpango wa muda mfupi wa miaka mitatu (3). Aidha katika kusaidia utekelezaji wa sera hiyo, pia wizara inaandaa rasimu ya Sheria ya Elimu itakayoendana na mabadiliko ya Sera mpya ya Elimu.

Mhe. Spika, mafanikio haya makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka kumi yanatokana na sera madhubuti ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, kwa kuwashirikisha wananchi katika kujiletea maendeleo. Aidha amani na utulivu uliopo hapa visiwani umechangia kupatikana kwa mafanikio hayo.

Napenda kuwashukuru na kuwapongeza wananchi kwa michango yao ya hali na mali katika kuimarisha sekta ya elimu. Aidha napenda kuwashukuru viongozi katika ngazi zote, wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kuwahamasisha wananchi wa majimbo yao katika kujiletea maendeleo.

Vile vile napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo wa ndani na nje waliounga mkono juhudi zilizoanzishwa na wananchi. Miongoni mwa washirika hao wa maendeleo ni Serikali za Sweden, Japan, Ufaransa, Iran, Oman, Misri, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Jamhuri ya Watu wa Korea, Canada, India, Malaysia, na Mashirika ya Kimataifa ya *SIDA, USAID*, Benki ya Dunia, *ADB, IDB, BADEA, UNICEF,UNESCO, UNFPA, ADEA*, *Aga Khan Foundation, Aga Khan Education Services*, na Shirika la *Book Aid International*. Pia nawashukuru washirika wa ndani kama vile *ZAYADESA*, *FAWE* Zanzibar, na *TASAF* kwa misaada yao mbali mbali *(Makofi)*.

Jadweli (h):

Mwaka	**Kiwango cha Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ya Elimu**
2001/02	399,709,959
2002/03	1,728,501,703
2003/04	3,137,037,058
2004/05	4,862,261,455
2005/06	8,259,290,681
2006/07	5,411,962,420
2007/08	5,779,720,930
2008/09	3,127,273,313
2009/10	8,225,200,722
JUMLA	**40,930,958,241**

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kuelezea utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 na matarajio ya utekelezaji kwa mwaka 2010/2011.

Muundo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Spika, kutokana na kupitishwa kwa Sera ya Uundaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume inayoongozwa na Mkurugenzi, muundo wa wizara yangu umebadilika. Hivi sasa tuna taasisi nne zinazojitegemea. Muundo mpya wa wizara ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho A ambacho kinatoa ufafanuzi zaidi.

Idara ya Sera na Mipango

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2009/2010

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi kumi ya maendeleo iliyotengewa jumla ya shilingi 4,425, 000,000/- za SMZ. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010, jumla ya shilingi 2,155, 000,000/- zilikuwa zimekwishatolewa ikiwa ni sawa na asilimia 49.0 ya makadirio. Utekelezaji halisi wa miradi ulikuwa kama ifuatavyo:-

Programu ya Uimarishaji wa Elimu ya Msingi

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 400,000,000/- za SMZ na RMB 5,000,000/- ikiwa sawa na Shilingi 850,000,000/- za Serikali ya Watu wa China. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 Shilingi 460,000,000/- zilizotolewa na SMZ na kutumika ikiwa ni sawa na asilimia 115 ya makadirio.

Mradi huu uliongezewa Shilingi 100,000,000/= baada ya kufanyika uhaulishwaji wa fedha kutoka kifungu chengine kutokana na mahitaji makubwa ya kumalizia majengo ya madarasa yalioanzishwa na wananchi. Kwa upande wa Serikali ya Watu wa China fedha zote zilizopangwa zilitolewa. Utekelezaji halisi wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

i) Jumla ya madarasa 50 yamekamilika na kuanza kutumika, na madarasa 53 tayari yameshaezekwa na yanasubiri utiaji wa sakafu, plasta na rangi. Vile vile jumla ya madarasa 301 yamefikia hatua ya kuezekwa, madarasa 126 yamo katika hatua za ujenzi wa kuta na nguzo na madarasa 114 yamefikia hatua mbali mbali za ujenzi kuanzia ukusanyaji wa vifaa hadi kuinua kuta. Jadweli 11 (a-d) zinatoa uchambuzi zaidi;

ii) Ujenzi wa Skuli mpya ya Kijichi, Wilaya ya Magharibi Unguja ambayo imefadhiliwa na Serikali ya Watu wa China umekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, siku ya Alkhamis tarehe 17 Juni 2010;

iii) Ukarabati wa majengo umekamilika katika skuli za Mwembe ladu, Jang'ombe Sekondari, Kiembe Samaki Msingi, Kiembe Samaki Sekondari, Kombeni, Bububu Sekondari, Upenja, Bumbwini, Jongowe, Uroa, Unguja Ukuu kwa Unguja na Skuli za Mitiulaya, Konde, Vikunguni, Ng'ombeni na Kisiwa Panza kwa Pemba. Pia kazi za ukarabati zinaendelea katika skuli za Bububu Msingi, Biashara Mombasa na Mtopepo;

iv) Mafunzo yametolewa kwa walimu mbali mbali wa skuli za Unguja na Pemba yakiwemo ya kompyuta na utumiaji wa mtaala mpya wa elimu ya msingi; na

v) Mihutasari mipya ya elimu ya msingi imechapishwa na kusambazwa maskulini.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 800,000,000/- za SMZ. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 jumla ya Shilingi 170,000,000/= za SMZ sawa na asilimia 21.3 zimetolewa na kutumika. utekelezaji halisi wa malengo ulikuwa ni kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa skuli mbili mpya za maandalizi unaendelea huko Potoa, Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja na Ungi Wilaya ya Micheweni Pemba; na

ii) Mswada wa vitabu kwa ajili ya kufundishia elimu ya maandalizi umetayarishwa.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa na SMZ pekee na ulipangiwa kutumia jumla ya TSh.650,000,000/- na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

iii) Kufanya ukarabati na upanuzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume; na

iv) kufanya ukarabati na upanuzi wa Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja na kununua vifaa vya ufundi.

Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 jumla ya Shilingi 130,000,000/- Ikiwa ni sawa na asilimia 20 ya makadirio zilipatikana na zilitumika. Utekelezaji wa malengo ni kama hivi ifuatavyo:

i) Vifaa vya uchongaji kwa ajili ya Skuli ya Sekondari ya Ufundi, Kengeja vimenunuliwa na kufikishwa skuli;

ii) Kazi za ukarabati wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume zinaendelea; na

iii) Kazi za ujenzi wa jengo la madarasa manne katika skuli ya Sekondari ya Ufundi, Kengeja zimeanza kwa kazi za upimaji wa kiwanja na upigaji wa matofali.

Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Kiislam Micheweni Pemba

Mhe. Spika, mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 50,000,000/- za SMZ. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 jumla ya Shilingi 25,000,000/- za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 50 za makadirio zilitolewa. Kazi za upigaji plasta, utiaji sakafu, uwekaji wa dari na uwekaji wa madirisha na milango katika ukumbi wa mitihani zimefanyika na kukamilika.

Mradi wa Upanuzi wa Uimarishaji wa Huduma za Maktaba

Mhe. Spika, mradi huu ulitengewa Shilingi 150,000,000/- za SMZ kwa ajili ya ukamilisha wa ujenzi wa jengo la Maktaba Kuu Unguja na kufanya maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la Maktaba huko Chake Chake Pemba. Jumla ya Shilingi 110,000,000/- sawa na asilimia 73.3 za fedha zote zimepatikana na kutumika kwa kazi zifuatazo:-

v) Kazi za urekebishaji wa baadhi ya sehemu za Maktaba kuu zilizoonyesha dosari ndogo ndogo zilifanyika;

vi) Vifaa vya ofisi, samani na kompyuta vimenunuliwa;

vii) Eneo kwa ajili ya Ujenzi wa jengo la Maktaba kuu huko Pemba limepatikana na kazi za usanifu michoro zimeandaliwa.

Mradi wa Uanzishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar

Mhe. Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA) na ulitengewa Shilingi 1,400,000,000/- za SMZ na Shilingi 5,824,000,000/= kutoka BADEA. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010, jumla ya Shilingi 560,000,000/- za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 40 ya makadirio zilipatikana, na kwa upande wa BADEA jumla ya Shilingi 940,099,578/= zilipatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kazi za ujenzi wa majengo manne ya Chuo Kikuu yako katika hatua mbali mbali za ujenzi; na

(ii) Zabuni za ununuzi wa samani, vifaa vya maabara na karakana za masomo ya uhandisi zimeandaliwa na zitatangazwa hivi karibuni.

Mradi wa Uanzishaji wa Elimu Mbadala na Amali

Mhe. Spika, mradi huu ambao unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) ulitengewa jumla ya Shilingi 200,000,000/- za SMZ na Shilingi 1,200,000,000/- za ADB. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010, jumla ya Shilingi 120,000,000/- za SMZ ikiwa ni sawa na asilimia 60 za makadirio na fedha zote kutoka kutoka ADB zilipatikana. Utekelezaji halisi wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala huko Wingwi Mtemani Pemba umefikia hatua ya kumwaga zege la kukamilisha sehemu ya chini ya jengo;

ii) Zoezi la kuwapatia mafunzo wakufunzi 14 wa vituo vya kazi za amali vya Mkokotoni na Vitongoji limekamilika. Pia walimu wawili wamemaliza mafunzo ualimu kutoka Chuo cha Mafunzo ya Ualimu ya Ufundi huko Morogoro;

iii) Vituo vya kazi za amali vya Mkokotoni na Vitongoji vimeanza kufanya kazi; na

iv) Jumla ya shilingi 946,000,000/= zimetumika kwa kuzikopesha asasi tatu za kifedha na vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa 23. Jumla ya wajasiriamali 2,875 wakiwemo wanawake 1,841 wamefaidika na mikopo hiyo.

Mradi wa Ukamilishaji wa Ujenzi Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Spika, mradi huu ambao unatekelezwa na SMZ pekee ulitengewa Shilingi 150,000,000/- na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa ghala;

(ii) Kununua samani kwa ajili ya Afisi ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Pemba; na

(iii) Kukamilisha ujenzi wa uzio katika Makao Makuu ya Wizara.

Hadi kufikia tarehe 31Mei, 2010 jumla ya Shilingi 100,000,000/= zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 66.7 ya makadirio na zilitumika kwa kazi za ukamilishaji wa ujenzi wa ghala la Wizara, kununua samani kwa ajili ya afisi ya Pemba na ujenzi wa uzio na kuendelea na ujenzi wa maeneo ya kuegeshea magari na vibanda vya walinzi.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima

i) Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa pamoja kati ya SMZ, Benki ya Dunia, BADEA na USAID. Mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 500,000,000/- za SMZ na Shilingi 11,823,700,000/- za Benki ya Dunia, BADEA na USAID. Hadi kufikia 31 Mei, 2010 jumla ya TSh 290,000,000/- za SMZ sawa na asilimia 58 ya makadirio zilipatikana na USD 781,485.32 za Benki ya Dunia.

Utekelezaji halisi wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

ii) Mikataba kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya maktaba za skuli na vitabu vya kiada vya sekondari kwa masomo ya Kiingereza, Uraia, Jiografia, Kiswahili, na masomo ya Ufundi na Biashara imeshatiwa saini. Baadhi ya vitabu vimeshasilishwa Wizarani;

iii) Kazi za kufanya tathmini ya zabuni za ujenzi wa skuli 15 mpya za sekondari za vijijini imekamilika na inasubiri maamuzi ya Benki ya Dunia kabla ya kutiliana saini mkataba wa ujenzi na wakandarasi;

iv) Michoro kwa ajili ya kazi za ukarabati wa skuli za sekondari za Hamamni, Tumekuja, Forodhani kwa Unguja na Utaani, Uweleni na Fidel Castro kwa Pemba zinaendelea kutayarishwa. Hatua itakayofuata ni kutangaza zabuni kwa wakandarasi;

v) Michoro kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa huko Mchanga Mdogo Pemba tayari imeshaandaliwa na kazi inayoendelea ni utayarishaji wa zabuni kwa ajili ya kutafuta mkandarasi wa ujenzi;

vi) Tathmini ya zabuni za Mshauri wa ujenzi na usanifu michoro kwa ujenzi wa skuli 2 za sekondari imekamilika na imewasilishwa BADEA kwa maamuzi. Mkataba wa mshauri wa ujenzi unatarajiwa kutiwa saini mara tu ya BADEA kuridhia tathmini iliyowasilishwa;

vii) Walimu 300 wa sekondari wanaofundisha masomo ya Sayansi na Hesabati kwa Kidato cha tatu na nne wamepatiwa mafunzo ya kukuza uwezo na ufanisi wa kufundisha masomo hayo; na

viii) Mikataba ya ununuzi wa vifaa vya maabara imetiwa saini na vifaa hivyo vinatarajiwa kuwasilishwa Wizarani hivi karibuni.

Mradi wa kumbukumbu za Kihistoria na Hifadhi ya Mambo ya Kale
Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa pamoja kati ya SMZ na Benki ya Dunia kupitia mradi wa MACEMP na unasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Mali asili, Mifugo na Mazingira ulitengewa jumla ya Shilingi 25,000,000/- za SMZ na Shilingi 260,000,000/- kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha zoezi la upimaji na kuyapatia hati miliki maeneo yote ya kale;

ii) Kukamilisha kazi za kuweka alama na vielelezo katika maeneo ya kale;

iii) Kuendelea na kazi za matengenezo ya magofu kupitia mpango wa TASAF;

iv) Kuyafanyia matengenezo makubwa makumbusho ya Kasri Forodhani;

v) Kuyafanyia matengenezo makubwa majengo ya Beit-el Ajaib, Mnazi mmoja na Gofu la Mtoni;

vi) Kuanzisha Makumbusho za kanda (site museums) katika maeneo ya Kale kama vile Chwaka Tumbe, Mkumbuu, Fukuchani na Kuumbi;

vii) Kuboresha mfumo wa uhifadhi wa kumbukumbu katika taasisi za serikali kwa kutoa mafunzo na ushauri;

viii) Kuendelea na tafiti za kale hasa katika maeneo ya mapango;

ix) Kuufanyia matengenezo msikiti wa kihistoria Kizimkazi.

Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 jumla ya Shilingi 25,000,000/- Ikiwa sawa na asilimia 100 ya makadirio zilipatikana kutoka SMZ na Shilingi 23,800,000/- zilipatikana kutoka Benki ya Dunia. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Jumla ya maeneo 37, Unguja 15 na Pemba 22, yameshapimwa na maeneo na hati miliki kwa maeneo ya Msikiti wa kale Kizimkazi, eneo la kale Chwaka, Magofu ya Fukuchani, magofu ya Dunga, Gofu la Kizimkazi na Mvuleni zimepatikana;

ii) Jumla ya maeneo 18 yenye magofu yameekewa mabango ya maelezo (information boards) na alama (sign boards);

iii) Jumla ya maeneo 11 ya magofu ya kale yamekamilisha kazi zao za matengenezo kupitia mpango wa TASAF Unguja na Pemba;

iv. Baadhi ya sehemu za Makumbusho ya Kasri Forodhani zilizokuwa katika hali mbaya zilifanyiwa matengenezo na sasa hali yake inaridhisha;

v. Makumbusho ya kanda (site museums) katika maeneo ya kale ya Chwakatumbe, Mkumbuu, Fukuchani na Kuumbi tayari yameshajengwa; na

vi. Msikiti wa Kale wa Kizimkazi Dimbani umefanyiwa matengenezo makubwa kutokana na msaada wa Serikali ya Marekani na sasa uko katika hali nzuri.

Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2010/2011

Mhe. Spika, Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepanga kutekeleza jumla ya miradi kumi ya Maendeleo. Kati ya Miradi hiyo, miradi sita itatekelezwa kutokana na bajeti ya SMZ pekee na minne itatekelezwa kwa mashirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Jadweli namba 47 inatoa uchambuzi zaidi. Malengo ya miradi mbali mbali itakayotekelezwa itakuwa kama ifuatavyo:-

Mradi wa Upanuzi wa Uimarishaji wa Huduma za Maktaba

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee na umetengewa Shilingi 150,000,000/=. Mradi huu una malengo yafuatayo:-

i) Kununua vitabu, samani na kompyuta ; na

ii) Kuanza kazi za ujenzi wa Tawi la Maktaba Kuu huko Pemba.

Mradi wa Uimarishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar

Mhe. Spika, mradi huu ambao unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu Afrika (BADEA) una malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu;

ii) Kununua wa vifaa vya Maabara, Samani na vifaa vya karakana; na

iii) Kuanza kutumia majengo ya Chuo Kikuu.

Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 1,725,000,000/- za SMZ na Shilingi 5,552,664,000/= kutoka *BADEA*.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano makubwa kati ya SMZ, Wananchi na Washirika mbali mbali wa Maendeleo wakiwemo *USAID*, *UNICEF*, Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*) pamoja na wahisani wengine mbali mbali. Mradi huu una malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 180;

ii) Kuwapatia walimu Mafunzo mbali mbali yakiwemo ya kompyuta, mafunzo juu ya kutumia lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kufundishia, mafunzo juu ya mtaala mpya wa ngazi ya msingi, mafunzo juu ya kufundisha katika mfumo wa elimu mjumuisho;

iii) Kuandaa na kuchapisha vitabu vya kiada kwa ajili ya madarasa ya kwanza na la pili;

iv) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa madarasa ya awali wa msingi;

v) Kuzifanyia ukarabati skuli 15, Unguja na Pemba;

vi) Kuzipatia samani skuli mbali mbali;

vii) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu wasiosomea kwa njia ya elimu masafa; na

viii) Kufanya mageuzi wa mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za elimu.

Jumla ya Shilingi 500,000,000/- za SMZ na Shilingi 8,998,354,000/= kutoka *SIDA*, *USAID* na *UNICEF* zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha malengo ya mradi huu.

Mradi wa Chuo cha Kiislam Micheweni Pemba

Mhe. Spika, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi 50, 000,000/- za SMZ pekee. Mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kujenga Uzio; na

ii) Kufanya ukarabati wa baadhi ya madarasa

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali

Mhe. Spika, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika vya wanawake na wahitimu kutoka vituo vya mafunzo ya amali ili waweze kujiajiri na kuendeleza fani walizosomea;

ii) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala huko Wingwi Mtemani;

iii) Kununua samani na vifaa vya kufundishia; na

iv) Kuanza kutumika.

Jumla ya Shilingi 150,000,000/- za SMZ zimetengwa kwa mradi huu.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya Serikali na wafadhili mbali mbali wakiwemo Benki ya Dunia na *BADEA*. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kuzipatia skuli za sekondari vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia;

ii) Kuzipatia samani skuli mbali mbali;

iii) Kuanza ujenzi wa skuli za sekondari 15 Unguja na Pemba;

iv) Kuanza ujenzi wa kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo;

v) Kununua vifaa vya ofisini;

vi) Kuanza matengenezo ya skuli za sekondari za Forodhani, Tumekuja, Hamamni, Fidel-Castro, Utaani na Uweleni; na

vii) Kuanza ujenzi wa skuli mbili za sekondari katika eneo la Kibuteni, Unguja na Mkanyageni, Pemba.

Mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi 900,000,000/- za SMZ na Shilingi 31,510,000,000/= kutoka Benki ya Dunia na *BADEA*.

Mradi wa Ukamilishaji wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi 75,000,000/- kutoka SMZ pekee na utakuwa na malengo yafuatayo:_

i) Kukamilisha ujenzi wa eneo la maegesho ya magari; na

ii) Kununua samani, kompyuta na vitendea kazi vyengine.

Mradi wa Kumbukumbu za Kihistoria na Hifadhi ya Mambo ya Kale

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mradi huu utaendelea kutekelezwa kwa ushirikiano kati ya SMZ na Benki ya Dunia. Mradi utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kufanya ukarabati mkubwa wa majengo ya makumbusho yakiwemo, kumbusho la Mnazi Mmoja, *Beit-el-Ajab* na Jumba la Wananchi "*People Palace*" ;

ii) Kukamilisha zoezi la upimaji na kuyapatia hati miliki maeneo yote ya kale;

iii) Kukamilisha kazi za kuweka alama na vielelezo katika maeneo ya kale; na

iv) Kuendelea na kazi za matengenezo ya magofu ya Mtoni na sehemu nyengine.

Jumla ya Shilingi 25,000,000/- za SMZ zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 mradi huu utateelezwa na SMZ pekee. Malengo ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i) Kuendelea na ujenzi wa madarasa katika Skuli ya Sekondari ya ufundi Kengeja;

ii) Kuipatia vifaa vya karakana; na

iii) Kuendelea na ukarabati ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume.

Mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi 500,000,000/-

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2010/2011, mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya SMZ na UNICEF. Malengo ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

viii) Kukamilisha ujenzi wa skuli mbili za maandalizi;

ix) Kutoa mafunzo ya mtaala mpya kwa walimu wa maandalizi;

x) Kutoa mafunzo ya ualimu wa maandalizi kwa njia ya radio; na

xi) Kununua vifaa vya kufundishia.

Mradi umetengewa jumla ya shilingi 400,000,000/ za SMz na Shilingi 320,936,000/= za *UNICEF*

Utafiti na Uchapishaji

Mhe. Spika, wizara inaendelea na uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa kwa Utafiti Mkuu wa *SACMEQ* wenye lengo la kupima ubora wa elimu itolewayo.

Zoezi hilo litafuatiwa na uandishi wa ripoti. Utafiti huo unajumuisha nchi 15 za Kusini mwa Jangwa la Sahara na kati mwa Bara la Afrika zikiwemo Zanzibar; Tanzania Bara; Botswana; Namibia; Lesotho; Msumbiji; Afrika ya Kusini, Malawi, Zimbabwe, Zambia, Swaziland, Kenya, Uganda, Mauritius; Seychelles. Utafiti huu umetusaidia katika kupima uwezo wa wanafunzi wetu wa madarasa ya msingi. Ripoti za awali zimeonyesha kuwa kiwango chetu kinaonekana kuongezeka.

Ukusanyaji na Uchambuzi wa Taarifa za Elimu

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 wizara iliendelea na utayarishaji wa mfumo wa kuwekea taarifa katika ngazi ya skuli. Vile vile wizara ilipanga kutoa mafunzo kwa walimu wakuu na walimu wanaoshughulikia taarifa za elimu katika skuli.

Mfumo huo wa uwekaji wa skuli umefanyiwa mabadiliko kwa kuandaa upya madodoso yanayosambazwa maskuli. Marekebisho hayo yamesaidia sana katika kuwezesha kupata taarifa kutoka skuli kwa urahisi sana. Pia mafunzo ya utumiaji wa mfumo huo yametolewa kwa walimu na maafisa wa elimu.

Mhe. Spika, mfumo huo wa uwekaji wa taarifa katika ngazi za skuli utasaidia kuimarisha ubora wa taarifa za elimu ambazo zinasaidia kupima utekelezaji wa mipango mbali mbali ya elimu. Mfumo huo pia utazisaidia skuli kuweza kupanga mipango ya maendeleo ya skuli kwa kutumia taarifa hizo kwa skuli husika.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, wizara ikishirikiana na *SIDA*, *USAID* na *UNESCO* itaendelea na kuuimarisha zaidi mfumo huo wa utoaji taarifa kwa kununua vifaa mbali mbali vya kufanyia kazi, kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu wakuu na walimu wanaoshughulikia taarifa za takwimu za skuli kwa wilaya 4 zilizobakia na pia kuuimarisha mfumo mzima wa kuwekea kumbukumbu za elimu unaotumika katika ngazi ya wizara.

Masuala ya Jinsia

Mhe. Spika, mafunzo juu ya masuala ya kijinsia yameendelea kutolewa kwa maafisa wa elimu na walimu wa skuli mbali mbali Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha walimu wanazingatia vyema masuala ya usawa wa kijinsia katika kutoa elimu kwa wanafunzi katika skuli. Kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 jumla ya walimu 288 wa Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo kati yao wakiwemo walimu wakuu 96 na walimu Washauri Nasaha 192. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuandaa mafunzo zaidi kuhusu masuala ya kijinsia kwa maafisa wa Elimu na walimu wa skuli mbali mbali.

Sera ya Elimu

Mhe. Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu, Wizara imeandaa mpango wa utekelezaji wa muda mfupi (miaka Mitatu) ambao unatokana na mpango mkuu wa elimu wa miaka minane. Mpango huo wa utekelezaji ndio utatekelezwa kwa mashirikiano na washirika wetu wa maendeleo na tayari Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) na USAID, zimetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo.

Mhe. Spika, utekelezaji wa mpango huo utaambatana na kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu maafisa na walimu. Mafunzo hayo yatalenga katika fani mbalimbali zikiwemo; fani ya Uchumi katika Elimu, Mipango katika elimu, Uongozi wa Fedha, Fani ya Ufundi wa Ujenzi, Fani ya Ukaguzi wa elimu, Utafiti wa Elimu, Uongozi na utawala wa Elimu, Elimu Mjumuisho, Uchambuzi wa takwimu, Elimu ya Maandalizi kwa ajili ya wakufunzi katika vyuo vya ualimu na vituo vya walimu wa maandalizi n.k.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kuhimiza na kueneza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) kama ni nyenzo muhimu ya kufundishia na kujifunza. Katika kuimarisha hilo, Walimu wakuu 20 wa Skuli za sekondari za Serikali na za Binafsi walipatiwa mafunzo mafupi juu ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano huko katika Taasisi ya Acharya nchini India.

Pia mafunzo yalitolewa kwa wataalamu ambao watasaidia katika kutatua matatizo ya kiufundi. Aidha, tarehe 9 Juni 2010, Wizara imetiliana saini Makubaliano (*MOU*) ya mashirikiano na *USAID* na kampuni binafsi za kimataifa za *Microsoft*, *Intel*, *Cisco* na *Zantel* juu kueneza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na katika skuli za zetu zote za msingi pamoja na vituo vya walimu na vyuo vya ualimu.

Mhe. Spika, kwa lengo la kuzihifadhi na kupatikana kirahisi taarifa muhimu za kielimu, Wizara kwa mashirikiano na Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*), inatayarishaji tovuti (*website*) ya Wizara. Mpango huu utakapokamilika taarifa muhimu za kielimu zitaweza kuhifadhiwa na ofisi zetu zitaweza kubadilishana taarifa kwa haraka zaidi na kwa gharama nafuu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, wizara inakusudia kukamilisha uandaaji wa tovuti ya wizara, kuandaa mafunzo kwa walimu wa skuli mbali mbali za msingi juu ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuzipatia skuli vifaa mbali mbali kama vile kompyuta na vifaa vyengine.

Mapambano Dhidi ya Maambukizo ya VVU/UKIMWI

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na washirika mbali mbali iko mstari wa mbele katika kuendeleza mapambano dhidi ya Ukimwi hasa katika utoaji wa elimu ya stadi za maisha kwa walimu na wanafunzi, kujikinga na maambukizi ya ukimwi, pamoja na kupambana na unyanyapaa kwa wale walioambukizwa. Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010, Mafunzo ya stadi za maisha na kujikinga na ukimwi yametolewa kwa wanafunzi 90, walimu wa masomo ya sayansi 416, walimu wa masomo mengine 700, walimu wakuu 380 na walimu washauri wa skuli 200. Pia Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI Zanzíbar (*ZAC*), pamoja na Wizara ya kazi, Ajira na maendeleo ya wanawake na watoto imeandaa mwongozo wa kufundishia stadi za maisha kwa vijana walio ndani na nje ya skuli, "*National Lifeskills Framework*". Mwongozo huo umechapishwa na kusambazwa maskulini.

Pia, mafunzo ya utumiaji wa muongozo huo yametolewa kwa maafisa mbalimbali wa elimu, walimu wakuu, na walimu wa masomo ya *Geography, Biology, Civics* na *English*. Mhe. Spika, Wizara, kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI ya Zanzibar imenunua Televisheni 20 (12 Unguja na 8 Pemba) pamoja na *Video* (12 Unguja na 8 Pemba) na kuzisambaza katika skuli 20 za Unguja na Pemba zilizoshiriki katika kampeni ya kuwalinda wanafunzi na unyanyasaji wa kijinsia na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi, skuli hizo ni Jang'ombe "A", Chumbuni, Bububu"A", Bububu "B", Kusini, Kiongoni, Kiboje, Ghana, Nungwi, Mkwajuni, Mahonda, na Kiwengwa kwa Unguja na Vitongoji, Michakaini, Kangani Msingi, Mtambile, Ole Msingi, Kangagani Msingi, Finya na Sizini kwa Pemba. Vifaa hivyo vimepelekwa na kukabidhiwa kwa viongozi wa klabu za Afya za skuli hizo ili vitumike kwa kuangalia filamu na matukio mbali mbali yanayohusiana na mapambano ya Virusi Vya Ukimwi/UKIMWI pamoja na unyanyapaa. Kwa kweli vifaa hivyo vitasaidia kuimarisha taaluma ya Virusi Vya Ukimwi/UKIMWI na jinsi ya kupambana nao.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *UNICEF* pia imefungua klabu za Afya 20 kwa skuli ambazo zilizokuwa hazikubahatika kuwa nazo hapo kabla. Klabu hizo zitasaidia wanafunzi kuweza kuelimishana wenyewe kwa wenyewe masuala mbalimbali yanayohusiana na Afya zao pamoja na mapambano juu ya Virusi Vya Ukimwi/UKIMWI. Wizara pia imejiandaa na kuweka mikakati imara ya kuendeleza mapambano ya Virusi Vya Ukimwi/UKIMWI kwa mwaka ujao. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kutoa mafunzo zaidi kwa walimu wote juu ya matumizi ya mwongozo juu ya mwongozo wa ufundishaji wa stadi za maisha.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kusimamia shughuli za uendeshaji kazi na utumishi, utunzaji wa kumbukumbu za wafanyakazi, uratibu na uendeshaji wa mafunzo ya wafanyakazi na huduma za msingi za wafanyakazi kwa mujibu wa kanuni za utumishi.

Mhe. Spika, hadi Juni 2010, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 14,458 wakiwemo wanawake 8,643 na wanaume 5,815, ambao kati yao 9,938 wamo katika kada ya ualimu.

Katika kupunguza uhaba wa walimu, jumla ya walimu wapya 620 wameajiriwa na kupangiwa kazi hasa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Wilaya za Micheweni na Mkoani, ambazo ndizo zilizokuwa na upungufu mkubwa wa walimu. Jumla ya wafanyakazi 120 wamestaafu kazi au wamestaafishwa, wafanyakazi 10 waliacha kazi kwa hiari au kufukuzwa kwa makosa mbali mbali ya kinidhamu na wafanyakazi 21 walifariki dunia. Aidha wafanyakazi 20 walipewa uhamisho wa kwenda kuendelea na kazi katika taasisi mbali mbali za Serikali.

Mhe. Spika, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi, idara hii ilisimamia upatikanaji wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi mbali mbali. Gari 5 zilinunuliwa kwa ajili ya kuimarisha utendaji katika Idara ya Nyaraka na Makumbusho, Idara ya Ukaguzi wa Elimu, Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Pia, jumla ya vespa 20 zilinunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, Waratibu wa Elimu Mbadala na Watu Wazima na Maafisa wengine wa Idara mbali mbali. Gari moja kati ya hizo iko Pemba kwa shughuli za uimarishaji wa Elimu ya Msingi.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuwaendeleza kielimu watumishi wetu, jumla ya wafanyakazi 332 wamepatiwa nafasi za kujiunga na masomo mbali mbli. Kati yao 5 wamejiunga na masomo ya cheti, 114 stashahada, 170 Shahada, 40 Shahada ya uzamivu na 3 shahada ya uzamili

Mhe. Spika, katika juhudi za kuwapa motisha walimu ili waendelee kuipenda na kuienzi kazi yao, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliupitisha muundo wa Utumishi wa Walimu ambao ulizingatia sifa za kielimu na uzoefu wa kazi wa mwalimu. Pia muundo huo ulizingatia kuingiza posho la kufundishia la asilimia 25 ambalo sasa limeunganishwa na mshahara wa mwalimu (*Consolidated Salary*). Walimu wote wamelipwa mishahara yao mipya tokea mwishoni mwa mwezi Aprili 2010.

Mhe. Spika, Wizara iliendelea na jitihada za kuwasaidia na kuwapa motisha wafanyakazi wake ili waweze kuyamudu mahitaji muhimu ya maisha. Wizara imewadhamini wafanyakazi kupata mikopo ya fedha taslim, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Kwa ujumla wafanyakazi 3114 walifaidika na mikopo hiyo yenye thamani ya Shilingi 912,841,415/-.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Posta, Benki ya *FBME*, Benki ya *CRDB*, Ushirika wa Kuweka na Kukopa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kampuni nyengine za watu binafsi kwa kuwapatia wafanyakazi wetu mikopo ya aina mbali mbali ambayo imewasaidia katika kuimua hali zao za kimaisha. Nawaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuwasaidia wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, idara itasimamia uajiri wa walimu katika wilaya zilizobakia kwa kadri tutakavyoweza kupata kibali cha kuajiri walimu wapya. Pia idara itasimamia upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya mahitaji ya ofisi zetu mbali mbali.

KITENGO CHA URATIBU WA OFISI YA WAZIRI NA UHUSIANO

Mhe. Spika, Kitengo cha Uratibu wa Afisi ya Waziri na Mahusiano, katika mwaka wa 2009/2010 kiliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za afisi ya waziri kwa ufanisi mkubwa. Miongoni mwa shughuli zilizofanikishwa ni pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano na nchi mbali mbali, na mashirika ya kimataifa.

Katika kulifanikisha hili, tumekutana na Mabalozi wa nchi mbali mbali waliopo nchini na viongozi wa mashirika ya kimataifa, kufanya ziara katika nchi rafiki, na kuhudhuria mikutano mbali mbali ya kimataifa.

Mabalozi tuliokutana nao ni wa kutoka nchi za Uturuki, India, Marekani, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*), Iran na Canada, Sweden, Egypt na Uingereza. Aidha tulikutana na Wawakilishi wa Mashirika ya *UNESCO*, ujumbe wa Saudi Arabia, Ujumbe kutoka India na Ujumbe wa *USAID*, *CIDA*, *British Council*, Benki ya Dunia na *SOS*.

Pia tulifanya ziara katika nchi mbali mbali kama vile, Ufaransa, Senegal, Brazil, Malaysia, Iran, Oman na Kenya. Mikutano na ziara tulizozifanya zimesaidia sana katika kuimarisha uhusiano wetu na washirika wetu wa maendeleo, kujifunza mambo mapya na pia kupata misaada mbali mbali ambayo imesaidia katika kuimarisha sekta ya elimu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, kitengo kitaendelea kuongeza ufanisi wa kazi kwa kujenga mawasiliano ya karibú zaidi na ofisini za ubalozi na Mashirika mbali mbali ya Kimataifa.

IDARA YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Spika, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi ina jukumu la kusimamia elimu ya maandalizi na elimu ya msingi pamoja na elimu ya Madrasa na Vyuo vya *Quraan*. Pia idara inasimamia skuli za binafsi za maandalizi na za msingi ili kuhakikisha kuwa zinasomesha kwa mujibu wa muhtasari uliyokubalika.

ELIMU YA MADRASA NA VYUO VYA QURAN

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, idara imefanya ziara za kikazi katika madrasa na vyuo vya *Quraan* pamoja na kukusanya taarifa za idadi ya walimu, wanafunzi na vyuo vya *Quraan* kwa Unguja na Pemba kwa kushirikiana na Masheha na Maafisa wa Elimu wa Mikoa na Wilaya.

Katika ziara hizo, walimu wa vyuo vya *Quraan* wamehamasishwa kutafuta njia mbadala za kuwapa adhabu wanafunzi wao badala ya kutegemea matumizi makubwa ya bakora, jambo ambalo linachangia utoro kwa wanafunzi.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 kuna jumla ya vyuo vya *Quraan* 1,175 kwa Unguja na Pemba vyenye jumla ya wanafunzi 276,211 kati yao wanawake 149,992 na wanaume 126,219. Vile vile kuna jumla ya walimu 8,857 wakiwemo wanawake 2,963 na wanaume 5,894.

Pia kuna jumla ya skuli za maandalizi za madrasa thamanini na nne (84) zinazosimamiwa na *Zanzibar Madrasa Resource Centre* zinazofundisha kwa misingi ya dini ya kiislamu. Idara imeendelea na juhudi zake za kuzisaidia madrasa na vyuo vya *Quraan* kwa kuzipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kila hali inaporuhusu.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 idara imeazimia kutoa mafunzo kwa walimu wa Vyuo vya *Quraan* kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo na kuwapatia mbinu bora za ufundishaji zitakazowafanya watoto kuvutiwa na kupenda kusoma katika vyuo hivyo ili kupata maadili mema.

Mafunzo hayo yamelenga kuwajengea walimu tabia ya kushirikiana na skuli pamoja na taasisi nyengine zinazotoa elimu ili kumuwezesha mtoto kupata elimu kwa pande zote. Hali hii itasaidia kuondoa manunguniko kwa walimu wa Vyuo vya *Quraan* kuwa muda mwingi watoto hushughulika na mambo ya Skuli na kuyapuuza mafunzo ya vyuoni.

ELIMU YA MAANDALIZI

Mhe. Spika, Elimu ya Maandalizi ni sehemu ya elimu ya lazima kwa kila mtoto wa Zanzibar. Katika mwaka 2009/2010, idadi ya skuli za maandalizi ni 238, kati ya hizo skuli 27 ni za serikali na skuli 211 ni za binafsi. Pia zipo jumla ya skuli za serikali 34, kati ya hizo skuli 14 ni za msingi na 20 ni za msingi na kati ambazo zimeanzisha madarasa ya maandalizi katika skuli zao.

Skuli za maandalizi za serikali zina jumla ya wanafunzi 4043, kati yao wasichana ni 2,082 na wavulana ni 1,961. Pia madarasa ya elimu ya maandalizi yalioko katika skuli za msingi na kati za serikali yana jumla ya wanafunzi 1,641, wakiwemo wasichana 843 na wavulana 798.

Mhe. Spika, pia zipo skuli za maandalizi za binafsi zenye jumla ya wanafunzi 17,681 wakiwemo wasichana 9,027 na wavulana 8,654.Vile vile vipo Vituo 178 vya mradi wa kutoa elimu ya maandalizi kwa njia ya Redio (*RISE*) ambavyo vina jumla ya wanafunzi 6,367 wakiwemo wasichana 3,264 na wavulana 3,103.

Idadi hiyo inafanya idadi ya wanafunzi wote walioko katika ngazi ya elimu ya maandalizi kufikia 29,732 ikiwa ni sawa na asilimia 33.9 ya watoto wanaopaswa kuwepo katika elimu katika ngazi hiyo. Ikilinganishwa na asilimia 17.8 ya uandikishaji ya mwaka 2009/2010 ni wazi kuwa tumepata mafanikio makubwa sana.

Mhe. Spika, idara imeendelea kushirikiana na washirika mbali mbali wa maendeleo ya elimu likiwemo shirika la kuhudumia watoto *UNICEF* katika kuandaa vitabu vya watoto vinavyoendana na mtaala wa elimu ya maandalizi na kuwapatia walimu mafunzo ya namna ya kutumia vitabu hivyo. Mafunzo hayo yalitolewa kwa walimu wa Skuli 30 za Unguja na 18 za Pemba. Vitabu hivyo vimeanza kutumika katika skuli za majaribio na katika mwaka 2010/2011 vitasambazwa na kutumika kwa skuli zote za maandalizi.

Mhe. Spika, idara inaendelea kushirikiana na mradi wa *RISE* (*Redio Instruction to Strenghen Education*) katika kuwapatia elimu ya maandalizi watoto wadogo kwa njia ya redio katika Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja na Micheweni Pemba hasa katika maeneo ambayo bado hayana skuli za maandalizi karibu na maeneo yao. Kwa mwaka 2010/2011 mradi utaandaa mafunzo ya walimu wa maandalizi kwa njia ya Radio.

Hatua hii itasaidia katika kuongeza upatikanaji wa walimu waliosomea ngazi hii ya elimu ili kukabiliana na ongezeko la skuli na madarasa ya maaandalizi katika skuli zetu za msingi na kati. Katika mwaka 2010/2011, Idara inakusudia

Mhe. Spika, Katika kujenga ushirikiano na kubadilishana uzoefu katika uendeshaji na utoaji wa elimu ya maandalizi, Walimu wa Skuli za maandalzi kutoka Arusha walitembelea Zanzíbar na kukutana na wenzao wa Zanzíbar. Pia walimu wakuu ishirini na nne (24) wa skuli za maandalizi za Zanzibar walitembelea Mkoa wa Arusha kwa lengo la kuzidi kuimarisha maelewano na kubadilishana uzoefu wa uanzishaji wa madarasa ya maandalizi katika Skuli za Msingi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, wizara itaendelea, kuhamasisha jamii na watu binafsi wenye uwezo wa kuanzisha skuli za mandalizi ili kuongeza ushiriki wa watoto katika ngazi hii ya elimu na kufikia asilimia 40 ifikapo mwaka 2011/2012. Pia tunakusudia kuongeza vituo vingi zaidi vitakavyotowa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio.

ELIMU YA MSINGI

Mhe. Spika, elimu hii inatolewa katika jumla ya Skuli 240 za Serikali na Skuli 59 za sekta binafsi. Hadi kufikia mwezi Machi 2010, idadi ya wanafunzi katika skuli za msingi imefikia 226,746 sawa na asilimia 112.0 ikilinganishwa na wanafunzi 220,819 sawa na asilimia 106.8 katika mwaka 2009.

Aidha, wizara imeweza kuwapatia nafasi watoto wote 31,092 walioandikishwa darasa la kwanza mwaka 2010. Kati ya hao 15,600 ni wavulana na 15,492 ni wasichana.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, walimu wa skuli za msingi 423 wamepatiwa mafunzo kupitia Mradi wa *Roots and Shoots*. Kwa kushirikiana na Taasisi ya *Jane Godall*, walimu wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu za ufundishaji kwa walimu wa masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi, Walimu Wakuu, Washauri wa Vituo vya Walimu na wakaguzi kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ngazi hii ya elimu bado inakabiliwa na matatizo ya uhaba wa nafasi, ingawa juhudi kubwa zinafanywa na wananchi, Serikali na washiriki wa maendeleo za kujenga madarasa mapya na Skuli mpya. Wizara bado inaendelea na hatua za kuwahamasisha wananchi kujenga madarasa na skuli mpya ili kwenda sambasamba na ongezeko la watoto.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, idara kwa kushirikiana na shirika la *UNICEF* na Wizara ya Kazi, Vijana na Maendeleo ya Wanawake na Watoto inakusudia kutoa mafunzo juu ya mbinu za ukomeshwaji wa utumikishwaji wa watoto kama mpango wa kitaifa unavyoelekeza.

SEKSHENI YA HUDUMA ZA WANAFUNZI

Mhe. Spika, Seksheni ya huduma za wanafunzi inashughulikia ustawi wa wanafunzi pamoja na kuwajengea wanafunzi uzalendo na mbinu za uongozi bora.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010, jumla ya skuli mia moja na thamanini na tano (185) zimefanya uchaguzi wa viongozi wapya wa serikali za wanafunzi. Viongozi hawa wa serikali za wanafunzi wamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na walimu katika kuongoza shughuli mbali mbali za uendeshaji na utunzaji wa mazingira ya skuli.

Viongozi wa serikali za wanafunzi wameweza kutembeleana na kubadilishana mawazo juu ya namna ya kufanikisha utendaji wa kazi zao.

Mhe. Spika, viongozi wa serikali za wanafunzi za Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu za kujiepusha na maambukizi ya UKIMWI na dawa za kulevya. Katika mwaka 2010/2011 Idara itaendelea kuziiimarisha serikali za wanafunzi kwa kuzipatia mafunzo ya aina mbali mbali.

IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI

Elimu ya Sekondari

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 elimu ya sekondari ilitolewa katika skuli 227, kati ya hizo skuli 197 ni za serikali na 30 ni za watu binafsi. Hadi mwezi Machi, 2010, walikuwepo jumla ya wanafunzi 48,883 wa sekondari katika ngazi ya sekondari ya awali (kidato cha kwanza na cha pili), ambao ni sawa na asilimia 84.3 ya wanafunzi wote wanaostahiki kuwepo katika elimu ya ngazi hii. Jadweli namba 16 inatoa uchambuzi zaidi.

Pia kwa ngazi ya elimu ya sekondari ya kidato cha tatu na cha nne na elimu ya ufundi walikuwepo wanafunzi 35,453. Kwa jumla idadi ya wanafunzi katika ngazi ya sekondari (Kidato cha 1 hadi Kidato cha 6) imefikia 84,099 kati yao 39,890 ni wavulana na 44,209 ni wasichana. Jadweli namba 16,20 na 21 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, wizara ina kusudia kuongeza madarasa zaidi ya kidato cha 3 na 4 na 5 na 6 katika skuli za sekondari kwa kadri ya idadi ya wanafunzi wanaofaulu mitihani ya kidato cha pili na kidato cha nne inavyoongezeka ikiambatana na upatikanaji wa walimu wenye sifa na vifaa vya kufundishia.

Huduma za Dakhalia

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010, dakhalia zetu zilihudumia jumla ya wanafunzi 1,993 (wavulana 988 na wasichana 1005) kama inavyoonekana katika Jadweli Namba 24. Idadi hii ni kubwa kidogo ukilinganisha na wanafunzi 1,897 waliokuwepo mwaka 2008/2009. Wanafunzi wanaoishi dakhalia ni wale wanaojitegemea kwa chakula. Napenda kuwashukuru wazazi na wananchi kwa kuweza kuwapatia huduma ya chakula watoto wao. Pia ninapenda kuwapongeza wanafunzi wanaoishi dakhalia kwa kuishi kwa amani na utulivu katika dakhalia zetu.

Serikali za Wanafunzi

Mhe. Spika, serikali za wanafunzi zina jukumu la kusaidia katika kudumisha nidhamu za wanafunzi maskuli na pia ni mojawapo ya mbinu ya kuwaandaa vijana kuwa viongozi wa baadae.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2009/2010, jumla ya skuli 185 zilifanya uchaguzi wa viongozi wa serikali za wanafunzi baada ya uongozi uliokuwepo kumaliza muda wake. Pia, Umoja wa Serikali za Wanafunzi wa Zanzibar (USEWAZA) umeanzishwa rasmi kwa madhumuni ya kusimamia uongozi wa wanafunzi na kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazowakabili wanafunzi katika maendeleo yao ya elimu na kutambua wajibu wao katika skuli zao.

Umoja huu umepata usajili wake rasmi kutoka kwa Mrajisi mwezi Septemba, 2009 na kuanza kujitangaza katika skuli zote za Unguja na Pemba kupitia katika vipindi vya TVZ na ziara katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

Kazi za Ujasiriamali

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, skuli zetu mbali mbali ziliendelea na kutoa mafunzo ya vitendo kuhusu ujasiriamali kwa wanafunzi. Shughuli nyingi zinazofanyika ni pamoja na biashara ya duka, kilimo cha mbogamboga, kuotesha vitalu vya miti, na kutengeneza mafagio. Shughuli hizi sio tu zimesaidia katika kuwafundisha wanafunzi ujasiriamali bali pia zimeziwezesha skuli kupata fedha ambazo zimesaidia katika kutatua matatizo yao kama matengenezo madogo madogo, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa vya michezo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, mkazo mkubwa utawekwa katika upandaji wa miti wa matunda katika maeneo ya skuli kwa ni aya kuongeza mapato ya skuli lakini pia kuyafanya mazingira ya skuli kuwa ni ya kuvutia zaidi.

IDARA YA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Mfuko wa Elimu ya Juu

Mhe. Spika, Mfuko wa Elimu ya Juu unajukumu la kuwapatia udhamini wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu vya ndani na nje ya Tanzania. Kwa mwaka 2009/2010 mfuko ulitengewa jumla ya shilingi 2,300,000,000/- kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi walioomba nafasi za elimu ya juu. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010 jumla ya shilingi 1,500,000,000/- zilipatikana na kutumika ikiwa ni sawa na asilimia 65.2 ya makisio.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, mfuko uliwadhamini wanafunzi 625 waliokwenda masomoni badala ya wanafunzi 300 waliokadiriwa awali, ikiwa ni ziada ya vijana 325 zaidi ya makadirio. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi waliopata sifa za kujiunga na taasisi za elimu ya juu. Kwa sasa tunao jumla ya wanafunzi 976 katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi. Kati yao wanaume ni 522 na wanawake 454. Jadweli Nam.25 (a) na (b) zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, katika mwaka huu uongozi wa bodi ya mfuko ulifanya ziara za kujitangaza katika skuli mbali mbali za sekondari za juu Unguja na Pemba ili kuutangaza zaidi kwa wanafunzi na kuwafahamisha taratibu za kuwasilisha maombi. Nimatarajio yetu kuwa ziara hizo zitasaidia katika kuwaandaa wanafunzi kuwasilisha maombi yao kikamilifu na kwa wakati.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, mfuko umetengewa jumla ya shilingi 2,500,000,000/-. Kiasi hiki cha fedha ni kidogo ukilinganisha na mahitaji ya vijana wanaoendeleana na wapya watakaojiunga na vyuo mbali mbali mwaka huu. Wizara itajitahidi kuwadhamini wanafunzi wengi zaidi kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2010/2011, Serikali kwa kushirikiana na kampuni ya *Ras Al Khaimah Gas Tanzania Ltd* inakusudia kupeleka wanafunzi nje ya nchi kwa ajili ya kusomea fani zinazohusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta kwa ni ya kuandaa wataalamu watakaobobea katika nyanja hio. Pia kwa kupitia ushirikiano huo huo tunakusudia kupeleka wanafunzi watakaosomea udaktari huko *Rasi Al-khaimah*. Aidha tunatarajia kupeleka wanafunzi katika nchi za Oman na Iran ambazo zimeonyesha ni aya kutupatia nafasi za masomo ya juu katika fani mbali mbali kufuatia ziara niliyoifanya katika nchi hizo hivi karibuni.

Sayansi na Teknolojia

Mhe. Spika, jitihada za kuendeleza taaluma ya sayansi na teknolojia zimeendelezwa. Kambi za Sayansi zilizohudhuriwa na wanafunzi wa kike 560 zimefanyika kwa lengo la kuwahamasisha wanafunzi wa kike kupenda masomo ya Sayansi na Hesabati. Kambi hizi za kutwa zimefanyika katika Vituo vya Walimu viliopo Unguja na Pemba. Kambi hizi zimefanyika kwa ushirikiano na taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya hapa Zanzíbar *FAWE*.

Napenda kuishukuru *FAWE* kwa michango yake ambayo imesaidia katika kuwahamasisha na kuwasaidia watoto wa kike waweze kusoma bila ya vikwazo vikubwa na wapende masomo ya sayansi na teknolojia. Katika kutilia mkazo masomo ya sayansi skuli nyingi zilipatiwa ushauri wa namna ya kujenga maabara zitakazokua na kiwango kinachokubalika. Pia walimu wanaosomesha masomo ya sayansi walipatiwa ushauri na mafunzo ya namna ya usomeshaji wa masomo ya sayansi kwa kutumia vifaa vya maabara kikamilifu.

Mhe. Spika, katika kupunguza uhaba wa vifaa vya maabara katika skuli zetu, Wizara kwa kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima, imeshatiliana saini mikataba na kampuni mbali mbali za kuleta na kusambaza vifaa vya maabara kwa skuli za sekondari 19 za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2010/2011, wizara itaendelea na juhudi ya kuandaa kambi nyingi zaidi za sayansi ili wanafunzi wengi zaidi waweze kuvutika zaidi na masomo ya sayansi na wafanye vizuri zaidi katika mitihani yao.

Taasisi za Elimu ya Juu

Mhe. Spika, hivi sasa, zipo taasisi nne za elimu ya juu. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume ikiwa ni taasisi za Serikali na Chuo Kikuu cha Zanzibar na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani ambavyo ni vya binafsi.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*)

Mhe. Spika, Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kimepata mafanikio makubwa tokea kuanzishwa kwake. Kwa mwaka 2009/2010, Chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 693 wa Shahada ya kwanza kati yao 286 (sawa na asilimia 41) ni wanawake ukilinganisha na wanafunzi 496 waliokuwepo mwaka jana.

Pia wapo wanafunzi 52 wa fani ya Kompyuta katika ngazi ya cheti na stashahada. Chuo pia kina Taasisi ya elimu endelevu ambayo inatoa huduma za kuwapatia elimu wananchi wanaopenda kujiendeleza katika fani mbali mbali.

Mhe. Spika, Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kimeeendelea kutoa mafunzo ya Lugha mbali mbali na elimu katika ngazi ya stashahada kupitia taasisi yake ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI). Katika mwaka 2009/2010, walikuwepo jumla ya wanafunzi 460, kati yao 141 ni wanaume na 319 wanawake wanaochukua masomo ya Stashahada ya lugha. Pia wanafunzi 152 wa kigeni (wanaume 61 na wanawake 91) wamejiunga na TAKILUKI kujifunza lugha ya Kiswahili.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzíbar kinatarajia kuandikisha wanafunzi 250 kwa masomo ya Stashahada ya Lugha na wanafunzi wa kigeni 210 kwa mafunzo ya muda mfupi ya Lugha ya Kiswahili. Pia kimelenga kuongeza programu zake ikiwemo ya Stashahada ya Ualimu wa Sayansi na ya Uongozi, na somo la Lugha ya Kitaliana.

Mhe. Spika, Mahafali ya tano ya Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar yalifanywa tarehe 12 Disemba 2009. Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Taifa ambae pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Amani A. Karume amewatunuku Shahada, Stashahada na vyeti wahitimu katika fani mbali mbali.

Katika mahafali hayo, jumla ya wahitimu 191, wakiwemo wanawake 87 walitunukiwa Shahada ya kwanza. Kati ya hao wanafunzi 132 walitunukiwa shahada ya Sanaa na Elimu; na wanafunzi 48 walitunukiwa shahada ya fani ya Sayansi na Elimu; na kwa mara ya kwanza kabisa Chuo kiliwatunuku wanafunzi 11 shahada ya Sayansi ya Kompyuta (*BSc. in Computer Science).*

Mhe. Spika, kwa ngazi ya stashahada, wahitimu 79 walitunukiwa Stashahada ya Lugha/Elimu, na 17 wa fani ya Sayansi ya Kompyuta. Pia wahitimu 8 wakiwemo wanawake 2 walitunukiwa vyeti katika fani ya Sayansi ya Kompyuta.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2009/2010, Chuo kimeweza kuimarisha mashirikiano yake na taasisi na vyuo vikuu mbali mbali vya kigeni. Miongoni mwa vyuo hivyo ni cha South Carolina State University cha Marekani, Chuo Kikuu cha Edward Mondlane cha Msumbiji, Chuo Kikuu cha Humboldt cha Ujerumani na Chuo Kikuu cha Bristol cha Uingereza. Pia, wafanyakazi 10 wamepelekwa masomoni katika nchi mbali kati yao 6 ni wahadhiri kwa nia ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzíbar kitaendelea kuimarisha shughuli zake zaidi kwa kuandaa program mpya za masomo, kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo zaidi , kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, na kuendelea kuchukua wanafunzi wapya katika fani na viwango mbali mbali.

Mhe. Spika, Napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Dkt. Amani A. Karume kwa Uongozi wake mzuri na wenye hekima katika maendeleo ya Chuo. Pia napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa chini ya Mwenyekiti wake mpya Mhe. Hassan Nassor Moyo kwa kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu na ufanisi mkubwa.

Aidha nampongeza Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa, Profesa Ali Seif Mshimba na watendaji wake wote pamoja na wanafunzi kwa kusimamia vizuri maendeleo ya chuo katika hali ya amani, nidhamu na utulivu mkubwa ambayo ndio chachu ya sifa na maendeleo ya Chuo.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani

Mhe. Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani kinaendelea na juhudi zake za kujiimarisha katika nyanja mbali mbali ili kiweze kupata usajili wa kuwa Chuo Kikuu kamilifu nchini. Chuo cha Elimu hivi sasa kina jumla ya wanafuzi 907 kati ya hao wanawake ni 397 kutoka nchi sita, ikiwa ni Uturuki, Sudan, Kenya, Somalia, Tanzania Bara na Zanzibar.

Katika mwaka wa masomo wa 2010/2011, Chuo kimepanga kuchukua wanafunzi wapya wapatao 350. Chuo Kikuu Kishiriki kimeshatoa wahitimu wa Shahada ya kwanza wapatao 865 wakiwemo wanawake 395 kutoka mataifa mbali mbali.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Chuo kimeanzisha maktaba ya kupitia mtandao (*electronic library*) ambayo inasaidia sana wahadhiri kupata taarifa mbali mbali za kitaaluma. kwa kuondosha upungufu wa wahadhiri Chuo kimepanga kuajiri wahadhiri wapatao 11 kutoka mataifa mbali mbali baada ya mwaka wa fedha 2009/2010 kushindwa kupata wataalamu wazalendo ambao walipewa kipaumbele zaidi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo kilipanga kutekeleza ujenzi wa majengo ya ofisi, madarasa na nyumba za wafanyakazi ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi na wafanyakazi. Hatahivyo, kutokana na sababu mbali mbali ujenzi huo haukufanyika na unatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, juhudi za kutafuta mkandarasi zimeshaanza kuchukuliwa. Majengo hayo ni yanatarajiwa kugharimu kiasi cha Shilingi 1,550,000,000/=

Mhe. Spika, katika kuimarisha uchapishaji wa majarida na kazi za wakufunzi na walimu, Chuo kimeweza kununua mitambo mipya kwa gharama ya zaidi ya Shilingi 130,000,000 na kuweza kufanya kazi katika kiwango cha ufanisi kinachokubalika. Licha ya kiwanda kufanya kazi za Chuo, pia kimekuwa kikifanya kazi za vyuo mbali mbali, mashirika na taasisi mbali mbali.

Ufanisi wa kiwanda umekuwa ukiongezeka kila mwaka, kwa mwaka uliopita kiwanda kilichangia asilimia 15 ya bajeti ya Chuo na kwa mwaka 2010/2011, kiwanda cha uchapaji kinatarajia kuchangia asilimia 20 ya bajeti ya chuo na asilimia iliyosalia itachangiwa na Makao Makuu ya Shirika la *Africa Muslims Agency* iliyopo nchini Kuwait.

Mhe. Spika, Katika kuimarisha mazingira na ustawi wa Chuo, Chuo kimeweza kununua samani za kutosha kwa ajili ya madarasa. Pia, Chuo kwa kushirikiana Kamati ya Maendeleo ya Chukwani kimeweza kujenga hodhi la kuhifadhia maji lenye uwezo wa lita 100,000 ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na tatizo la maji katika eneo hilo.

Chuo Kikuu cha Zanzibar

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2009/2010 Idadi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Zanzíbar imeongezeka na kufikia 1,972 (1119 wanaume na 853 wanawake) ukilinganisha na wanafunzi 1,727 waliokuwepo mwaka 2008/2009. Wanafunzi hao wanasoma fani ya Sheria, Biashara, Utawala, Uchumi na Teknolojia ya Mawasiliano Jadweli Nam 28 inatoa ufafanuzi zaidi.

Pia, Chuo Kikuu cha Zanzíbar, kimetoa wahitimu 524 (wanawake 347 na wanaume 177). Katika mwaka wa masomo 2010/2011, Chuo kimepanga kupokea wanafunzi wapya 500 katika fani mbali mbali kwa mwaka wa kwanza.

Mhe. Spika, Chuo kimeendelea kujitangaza na kujulikana zaidi nje ya nchi yetu. Kwa mara ya kwanza chuo kimepokea wanafunzi waliojiunga kutoka nchi za Lesotho, Botswana na Burundi. Wanafunzi wengine wa kigeni wanatoka katika nchi za Kenya, Uganda, Zambia, Malawi na Rwanda.

Chuo kinalengo la kupokea wanafunzi kutoka eneo lote la Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara na kwengineko. Kwa madhumuni ya kujipanua, Chuo kinakusudia kufungua matawi katika sehemu mbali mbali kwa kuanzia na Dar es Salaam, ambapo mipango imeshaanza kwa ajili ya kupata majengo kwa kazi hiyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Chuo Kikuu cha Zanzibar kimeendelea kujiimarisha kwa kukamilisha majengo ya kumbi za mihadhara pamoja na mikutano na kuanzisha fani nyengine za kitaaluma. Chuo kimeanzisha shahada ya Uzamili katika fani ya sheria mchanganyiko (*Comparative Laws*), Stashahada ya Sheria ya Jinai (*Criminal Justice*). Chuo pia kinajipanga kwa ajili ya kutoa stashahada nyengine za uzamili pamoja stashahada mbali mbali.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na uhaba wa wahadhiri, Chuo kimeendelea kuajiri wahadhiri mkazo mkubwa umewekwa katika kuajiri wahadhiri wazalendo ambao hadi sasa wamefikia zaidi ya asilimia 73 ya wahadhiri wote. Pia jitihada zimeendelea katika kuwapeleka masomoni wahadhiri wa kitanzania ili wafikie katika kiwango cha udaktari na waweze kukabiliana na ukuaji wa chuo na kupunguza kutegemea wahadhiri kutoka nje.

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume

Mhe. Spika, kufuatia kuanzishwa rasmi kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume uongozi wa taasisi unaojitegemea ulitangazwa rasmi katika mwezi wa Oktoba, 2009 ikiwemo uteuzi wa Mwenyekiti, Mkurugenzi na wajumbe kumi wa bodi.

Mhe. Spika, malengo makuu ya kuanzishwa taasisi hii ni kuweza kutoa taaluma katika ngazi ya stashahada, stashhada ya juu na shahada katika fani za ufundi, sayansi na teknolojia na hivyo kuweza kutosheleza mahitaji ya nchi katika fani hizo. Taasisi kwa kushirikiana na Bodi imeandaa mipango ya muda mfupi na mrefu itakayoiwezesha taasisi hiyo kutekeleza majukumu yake

Mhe. Spika, katika hatua mbali mbali za kuimarisha taasisi hiyo, Taasisi imeandaa muundo wa Utumishi wa wafanyakazi wake. Muundo huu amabao umeshawasilishwa wizarani umezingatia maslahi ya wafanyakazi kwa mujibu wa sifa na uzoefu wao wa kazi kama zilivyo Taasisi nyengine za elimu ya juu. Muundo huo wa utumishi utakapoanza kutumika utasaidia sana katika kujenga ari za uwajibikaji na kuwavutia wataalamu wengine kufanya kazi katika taasisi hiyo.

Mhe. Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume imeweza kupiga hatua kubwa katika kufanikisha malengo iliyojiwekea. Utekelezaji halisi ni kama hivi ifuatavyo:-

i) Kushajiisha na kuwatafutia ufadhili wanafunzi wa kike 40 kwa masomo ya awali ya Diploma;
ii) Kufanya manunuzi ya vikalio 105 kwa mashirikiano na KOICA;
iii) Kumaliza utengenezaji wa chumba cha komyputa chenye kompyuta 25 na vifaa vya kufundishia kwa mashirikiano ya Taasisi na KOICA;
iv) Kufikia lengo la kupeleka walimu 3 kuchukua shahada za juu kila mwaka na kuwa na walimu 13 waliopo masomoni;
v) Kufikia lengo la kusajili wanafunzi 100 kwa kila mwaka wa masomo.
vi) Kukamilisha utengenezaji wa dakhalia ya wasichana;
vii) Kufufua njia za ndani kwa kuweka vidaraja ili kurudisha haiba ya Taasisi;
viii) Kukamilisha kutengeneza sheria ndogo ndogo za mitihani, fedha, na wafanyakazi;
ix) Kukamilisha mpango kazi wa miaka mitatu 2010/2013;
x) kuyafanyia matengenezo, maeneo yaliyobomoka, jengo la madarasa na kuweka uzio kuzunguka eneo la Taasisi;
xi) Kuweka mpango madhubuti wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Taasisi; na
xii) Kujenga mashirikiano mazuri na Taasisi nyengine ndani na nje ya nchi.

Wafanyakazi na Wanafunzi

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2010, Taasisi ilikuwa na jumla ya wanafunzi 237 wavulana 182 na wasichana 55. Pia ina jumla ya wafanyakazi 71, wakiwemo wakufunzi 51 (wanawake 20) na wasiokuwa walimu 20 (wanawake 2). Vile vile wakufunzi 12 wapo masomoni kwa mafunzo ya shahada ya pili. Wakufunzi hao watakaporejea kutoka masomoni watasaidia sana katika kupunguza uhaba wa wakufunzi.

IDARA YA MAFUNZO YA UALIMU

Mafunzo ya Ualimu

Mhe. Spika, mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya cheti na stashahada yanatolewa katika vyuo vitatu vya ualimu ambavyo ni Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja, Chuo cha Kiislamu Kiuyu Micheweni Pemba na Chuo cha Benjamin Mkapa cha Wete Pemba.

Kwa mwaka 2009/2010, vyuo hivyo vilikuwa na jumla ya wanafunzi 2,618, wanaume 628 na wanawake 1,990. Kati ya wanafunzi hao 56 walihudhuria mafunzo ya Cheti cha Ualimu wa Elimu Mjumuisho, 1,264 Stashahda ya Ualimu wa Msingi na 1354 Stashahada ya Ualimu wa Sekondari. Jedwali 30 (a) (b) na (c) inatoa ufafanuzi). Aidha jumla ya wanafuzi 785 wakiwemo wanaume 251 na wanawake 534 wamehitimu mafunzo ya ualimu katika vyuo hivyo mwaka huu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, vyuo hivyo vinatarajiwa kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu kwa kuandikisha wanafunzi wapya katika ngazi ya Stashahada ya ualimu msingi, sekondari na cheti cha ualimu mjumuisho. Wizara inakusudia kuimarisha mafunzo ya ualimu kwa kuvipatia vyuo hivyo walimu wenye ujuzi, kuvipatia vifaa na usafiri.

Mafunzo ya Ualimu Kazini

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Vituo vya Walimu vimeendelea kuratibu mafunzo ya ualimu kazini. Warsha za masomo zimeendeshwa kwa masomo mbali mbali kukidhi mahitaji ya walimu na skuli. Aidha jumla ya walimu 100 kutoka skuli 20 za msingi na sekondari zenye matatizo ya madarasa yenye wanafunzi wengi walipatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za kufundishia madarasa yenye wanafunzi wengi.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utendaji katika vituo vya walimu, waratibu wa vituo na washauri wa masomo wa vituo vyote 11 vya walimu waliandaliwa warsha ya kuwajengea uwezo wa kuongoza, kuandaa na kusimamia programu za mafunzo kazini.

Mhe. Spika, Idara imeandaa mafunzo kazini kwa walimu 500 wa Sayansi na Hisabati wa sekondari (Kidato cha 3 na cha 4) juu ya kukuza uwezo wao na ufanisi wa kuyafundisha masomo hayo. Pia walimu wakuu 300, wakaguzi wa elimu 40, waratibu wa vituo na washauri wa masomo 45 nao wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuongoza na kusimamia skuli kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Wizara inaendelea na utaratibu wa mafunzo ya ualimu kwa njia ya elimu masafa kwa walimu wa skuli za msingi wasiosomea ualimu. Walimu wapatao 630 wakiwemo wanaume 115 na wanawake 515 wamejiunga na mafunzo hayo mwezi wa Februari 2010. Mafunzo hayo yanaendeshwa katika vituo vyote tisa vya walimu vilioko Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, walimu 30 wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya mtandao (*internet*), maafisa wa elimu na wafanyakazi wengine 39 wamepatiwa mafunzo ya awali ya kompyuta, na wafanyakazi 11 wamepatiwa mafunzo ya matengenezo ya kompyuta '*trouble shooting'*. Pia walimu wakuu 20 walishirikia mafunzo ya kompyuta katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya *Acharya* nchini India.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 wizara itayaimarisha mafunzo ya ualimu kwa kuviimarisha vituo vya walimu ili viweze kukidhi haja ya kutoa mafunzo bora kwa walimu, kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu kuhusiana na masomo wanayofundisha na mbinu bora za kufundishia masomo hayo kwa kupitia vituo vya walimu.

Pia itatoa mafunzo ya Kiingereza na Mawasiliano kwa walimu wa Kiingereza, Hisabati, Sayansi na Sayansi Jamii msingi, kuandaa mafunzo kwa walimu wa skuli za maandalizi kwa njia ya redio kwa kupitia vituo vya walimu, kuimarisha mtaala wa ualimu diploma ya msingi kutokana na mabadiliko ya mitaala ya msingi, kutoa mafunzo ya elimu mjumuisho kwa walimu wote, kutoa mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa walimu 300 wa skuli za msingi na sekondari na kuandaa ser aya mafunzo ya ualimu kazini.

IDARA YA UKAGUZI WA ELIMU

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, kazi za ukaguzi zilikwenda vyema, idara imenunua basi moja jipya, na mabasi madogo mengine mawili yanatarajiwa kuwasili nchini hivi karibuni kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukaguzi wa skuli.

Mhe. Spika, idara imezifanyia ukaguzi jumla ya skuli 166 Unguja na Pemba. Idadi hii ni kubwa kulinganisha na lengo lillopangwa la kukagua skuli 160. Jumla ya skuli 14 zilifanyiwa ukaguzi mkuu, 44 ukaguzi wa ziara, 83 ukaguzi wa ziara fupi fupi, 12 ukaguzi wa usajili na 13 ukaguzi maalumu. Skuli zilizofanyiwa ukaguzi zilipatiwa ripoti zake zinazooonyesha uzuri na kasoro zilizoonekana na kupatiwa ushauri wa aina mbali mbali wa namna ya kuimarisha shughuli zao.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utendaji, wakaguzi, walipata mafunzo mbali mbali. Miongoni ya mafunzo hayo ni uongozi na utawala wa uendeshaji wa skuli, "*mentoring"*, elimu mjumuisho na matumizi ya vitabu vya elimu ya maandalizi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, idara ina lengo la kuzikagua skuli 180 zikiwemo skuli 135 za serikali na 45 za binafsi. Kati ya hizo skuli 16 zitafanyiwa ukaguzi mkuu, skuli 47 ukaguzi wa ziara, skuli 90 ukaguzi wa ziara fupi fupi, skuli 13 ukaguzi wa usajili na skuli 14 ukaguzi maalumu.

Pia idara inakusudia kutafuta mtaalamu mwelekezi kwa ajili ya kuangalia namna ya kuimarisha shughuli za ukaguzi kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Vile vile Idara inakusudia kufanya mapitio ya dodoso la ukaguzi na viwango vya elimu vya skuli. Aidha idadi ya wakaguzi wataongezwa ili kulingana na ongezeko la skuli, walimu na wanafunzi.

IDARA YA MITAALA NA MITIHANI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, idara ilisimamia uandishi wa mihutasari mipya ya elimu ya msingi kwa darasa la kwanza hadi la sita pamoja na kuratibu uchapishaji wake. Mihutasari hiyo imeanza kutumiwa na wanafunzi waiojiunga na darasa la kwanza wa mwaka 2010. Idara pia ilisimamia mafunzo ya awali ya matumizi ya mihutasari hiyo kwa walimu 900 wanaosomesha darasa la kwanza.

Mhe. Spika, kwa upande wa uandishi na uchapishaji wa vitabu, idara kwa kushirikiana na shirika la *UNICEF* ilisimamia uhariri na uchapishaji wa vijitabu vya kusomea wanafunzi wa skuli za maandalizi kwa masomo ya Sayansi, Lugha na Hisabati. Pia, Idara iliratibu utoaji wa mafunzo ya awali kwa walimu 106 ambao wanasomesha vijitabu hivyo kwa majaribio.

Vile vile, idara iliratibu taratibu za awali za ununuzi wa vitabu vya Kiingereza, Kiswahili, Historia, Jiografia, Uraia masomo ya Biashara, Ufundi na Sayansi ya Kompyuta kwa wanafunzi wa vidato vya 1 hadi 6. Vitabu hivi vitanunuliwa kupitia Mradi wa Elimu ya Lazima unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, jumla ya wanafunzi 22,179 walifanya mtihani wa darasa la 7 mwezi wa Novemba 2009 na jumla ya wanafunzi 18,812 walifaulu kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza ikiwa ni sawa na asilimia 84.8 ikilinganishwa na asilimia 84.6 ya wanafunzi waliofaulu mtihani huo mwaka 2008.

Kwa upande wa mtihani wa kidato cha 2, kati ya wanafunzi 21,255 waliofanya mtihani huo mwezi Novemba, 2009 wanafunzi 11,515 ikiwa ni sawa na asilimia 54.2 walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha 3 katika skuli mbali mbali. Matokeo haya ni mazuri yakilinganishwa na ya mwaka 2008 ambapo asilimia 53.9 ya wanafunzi walifaulu. Jadweli Namba 31 na 32 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa mtihani wa Taifa wa kidato cha nne, kati ya wanafunzi 8,725 wa skuli za Serikali na binafsi waliofanya mtihani huo mwezi Oktoba 2009, wanafunzi 7,066 wamefaulu ikiwa ni sawa na asilimia 81.0. Aidha, kati ya wanafunzi waliofaulu, 1,984 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika skuli za Serikali mwaka 2010/2011, wakiwemo wanafunzi 1,214 kutoka skuli za Serikali, 140 wa skuli binafsi na 630 wanafunzi wa faragha. Jadweli namba 33 (a) na (b) zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, kati ya wanafunzi 2,388 waliofanya mtihani wa Taifa wa kidato cha sita, mwezi Februari 2010, wanafunzi 1,940 ikiwa ni sawa na asilimia 84.1 walifaulu. Asilimia hii ni ndogo ikilinganishwa na ya mwaka 2009 ambapo kati ya wanafunzi 1,959 waliofanya mtihani, wanafunzi 1,659 ikiwa ni sawa na asilimia 84.7 walifaulu.

Hata hivyo, idadi ya wanafunzi waliofaulu na kupata sifa za kuendelea na masomo ya elimu ya juu kwa mwaka 2010 ni wengi zaidi ukilinganisha na wa mwaka 2009. Jadweli namba 34 inatoa uchambuzi zaidi. Aidha, kati ya wanafunzi 40 waliofanya mtihani wa stashahada ya ufundi wanafunzi 15 sawa na asilimia 37.5 ya watahiniwa walifaulu na wanafunzi 25 walitakiwa kurudia mitihani ya baadhi ya masomo.

Mhe. Spika, kwa upande wa mtihani ya Ualimu, kati ya wanafunzi 125 waliofanya mtihani ya stashahada ya Ualimu (sekondari) katika chuo cha kiislam Mazizini na chuo cha Kiislam Kiuyu Micheweni wanafunzi 18 sawa na asilimia 14.4 walifaulu na wanafunzi 67 watarudia mitihani yao. Aidha, kati ya wanafunzi 213 waliofanya mtihani wa Stashahada ya Ualimu (Msingi) katika Chuo cha Kiislam Mazizini na Benjamin William Mkapa wanafunzi 295 sawa na asilimia 94.8 wamefaulu na wanafunzi 16 watarudia mitihani yao.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, idara itasimamia marekebisho ya vitabu vya wanafunzi wa elimu ya maandalizi (baada ya majaribio) na baadaye kuchapishwa kwa matumizi ya wanafunzi wote wa skuli zote za maandalizi. Idara pia itaratibu mafunzo ya awali ya matumizi ya mihutasari mipya kwa wakaguzi wa elimu, walimu wakuu wa skuli za msingi kwa walimu wanaosomesha darasa la pili 2011. Aidha, idara itaratibu uandishi wa vitabu vya wanafunzi wa madarasa ya I – IV kwa kufuata mihutasari mipya.

IDARA YA ELIMU MBADALA NA WATU WAZIMA

KISOMO:

Mhe. Spika, nchi yetu bado inayo watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu, ingawa idara husika inatoa msukumo mkubwa kupambana na hali hii. Tatizo hili linachangiwa zaidi na ongezeko kubwa la idadi ya watu, utoro, uhamiaji na kukatisha masomo njiani kwa vijana wetu kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za kifamilia.

Mhe. Spika, pamoja na matatizo hayo, idara imeendelea na jukumu lake la kuondoa tatizo la kutojuwa kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wananchi wetu. Katika mwaka 2009/10, jumla ya wanakisomo 6,980 walikuwemo madarasani, wanawake wakiwa 6,053 na wanaume 1,927. Jadweli namba 35 inatoa uchambuzi zaidi. Jumla ya wanakisomo 5837 walifanyiwa upimaji, kati yao wanawake wakiwa 4961 na wanaume 876.

Jumla ya wanakisomo 487, wanawake wakiwa 389 na wanaume 98 wameweza kujikombowa. Katika hatua ya nne kwa mwaka 2010/11, idara itaendelea kuwahamasishaji wananchi wengi zaidi kujiunga na madarasa ya kisomo katika sehemu zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika juhudi za kuhamasisha na kufanikisha kisomo cha watu wazima, idara iliadhimisha sherehe za Juma la Elimu ya Watu Wazima kiwilaya kwa hapa Unguja, katika mtindo ambao umeonekana kuleta mafanikio makubwa. Mtindo huo, ni kuendesha semina au kongamano, pamoja na kutoa mafunzo maalum kwa masheha, wajumbe wengine wa vijiji, juu ya suala zima la umuhimu wa kisomo.

Idara imefanikiwa kufanya kongamano ambalo liliwashirikisha waratibu wote, wakuu wa vituo, pamoja na maafisa wengine wanaoshughulikia suala la kisomo. Vikundi vya ushirika, viliendelea kuonyesha sanaa zao za mikono, kama kawaida ya maadhimisho mengine ya Juma hilo. Kwa upande wa Pemba sherehe hizo zilifanyika Ki-Mkoa, katika siku tofauti. Maadhimisho ya sherehe hizi yataendelezwa kila mwaka.

Elimu Mbadala

Mhe. Spika, wizara imeendelelea kutoa mafunzo ya elimu mbadala kwa vijana wenye umri kati ya miaka 13 na kuendelea ambao hawakubahatika kwenda skuli au waliacha masomo njiani kutokana na sababu mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 vimekuwepo vituo 49 vya Elimu Mbadala vyenye jumla ya wanafunzi 1289. Katika kipindi hiki vijana 552 wamejiunga na madarasa ya kawaida katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba baada ya kufanyiwa upimaji na kuonekana wanauwezo wa kusoma katika madarasa ya kawaida. Aidha wanafunzi watatu (3) kutoka vituo vyenye madarasa ya elimu mbadala wamefaulu na kuchaguliwa kuingia katika madarasa ya michepuo na wanafunzi watano wameingia kidato cha kwanza.

Mhe. Spika, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo kimepata maendeleo makubwa. Hivi sasa kituo kina jumla ya wanafunzi 223, wakiwemo wanawake 120, na wanaume 103, ambao wanaendelea na masomo yao. Mbali na masomo ya kawaida wanafunzi hao pia wanajifunza fani za umeme, ushoni, kompyuta, house-keeping na nyenginezo. Katika mwaka 2010/2011, Idara itaendelea kuwahamasisha vijana kujiunga katika vituo vilivyoko karibu nao pamoja na Kituo cha Elimu Mbadala,Rahaleo ili waweze kupata ujuzi wa zile fani ambazo wangezihitaji.

Mafunzo ya Kazi za Amali

Mhe. Spika, Idara imeendelea kutoa mafunzo mbali mbali ya kazi za amali kwa wanakisomo waliomaliza hatua za tatu na nne, na pia kwa vijana waliomaliza elimu ya lazima (kidato cha pili). Mafunzo hayo yanatolewa katika fani za Sayansi Kimu (Ushoni na Upishi), Useremala, Kilimo na ufugaji.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Kituo cha Sayansi Kimu kilichopo Idarani kilikuwa na jumla ya vijana 102 wa kike wanaochukua mafunzo ya fani za upishi na ushoni. Vijana 47 walikuwa wakichukua mafunzo ya ushoni na 35 upishi. Kati yao vijana 73 wamefanya mitihani ya *VETA*. Pia, wanafunzi wapya 65 wamejiunga na kituo na wameanza mafunzo yao.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, idara itaendelea kutoa mafunzo ya kazi za amali katika fani mbali mbali kulingana na mahitaji ya vijana wetu tutaowapokea katika kipindi hiki.

Vituo vya Kujiendeleza

Mhe. Spika, vituo vya kujiendeleza vinaendelea kuandikisha vijana wengi waliomaliza elimu ya lazima na wale ambao wamemaliza Kidato cha Nne na cha Sita ambao wanania ya kuongeza elimu yao. katika mwaka 2009/2010, jumla ya wanafunzi 5,215 wamejiunga katika vituo mbali mbali vya kujiendeleza Unguja na Pemba. Jadweli namba 36 inatoa uchambuzi zaidi.

Katika mwaka 2009/2010, kati ya watahiniwa wa faragha 10,230 waliofanya mitihani ya Kidato cha Nne, watahiniwa 5,400 sawa na asilimia 52.79 walifaulu mitihani yao. Kwa upande wa mitihani ya Kidato cha Sita, kati ya watahiniwa wa faragha 1,757 waliofanya mitihani hiyo, watahiniwa 1091, walifaulu ikiwa ni sawa na asilimia 62.1 ya watahiniwa wote. Jadweli namba 37 (a-c) inatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa somo la sheria, kituo kilikuwa na wanafunzi 78 wakiwemo wanaume 49 na wanawake 29, kati ya hao wanafunzi 57 walikuwa wa kiwango cha Stashahada na 21 ngazi ya Cheti. Wanafunzi 14 ngazi ya Stashahada wamehitimu mafunzo yao, wakiwemo wanaume 10 na wanawake 4.

Programu za Wanawake

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, juhudi za kuwaendeleza wanakisomo wanawake pamoja na kuwahamasisha kujiunga pamoja katika vikundi vya uzalishaji mali ziliendelezwa. Hivi sasa vipo vituo 69 vya akinamama Unguja na Pemba. Miongoni mwa shughuli za uzalishaji zinazoendeshwa na vikundi vya wanakisomo ni ufugaji wa mbuzi wa maziwa huko Kimembe (Kaskazini "A") na ufugaji wa kuku kwa vikundi vilioko Upenja, Kijagi, Mbuyutende na Kigongoni.

Pia akina mama wa vikundi mbali mbali wamepatiwa mafunzo na miongozo mbali mbali juu ya kuendesha miradi yao kitaalamu. Katika mwaka 20010/2011, idara itaendelea na uhamasishaji wa wanakisomo ili waweze kujiunga pamoja na kuanzisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji mali, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo na utaalamu wa miradi yao mbali mbali ya uzalishaji mali na utafutaji wa masoko kwa ajili ya kuuza bidhaa zao.

Elimu kwa Vyombo vya Habari

Mhe. Spika, vyombo vya habari vilivyopo nchini vimesaidia sana katika kuendeleza kisomo cha watu wazima. Katika mwaka 2009/2010 idara imefanikiwa kurusha vipindi 42 vya Redio na vipindi 12 vya Televisheni. Aidha idara imefanikiwa kuchapisha makala matatu katika gazeti la "ZANZIBAR LEO".

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Idara inakusudia kurusha hewani kipindi kimoja cha Redio na kimoja cha Televisheni kwa kila wiki. Vile vile Idara itaendelea kutayarisha na kuchapisha makala zinazohusu elimu mbadala na watu wazima kwa lengo la kuelimisha jamii. Aidha huduma za maktaba mjini na vijijini zitaendelea kuimarishwa ili ziweze kuwasaidia wanakisomo katika kujiongezea maarifa juu ya kazi zao mbali mbali pamoja na suala zima la kisomo, katika vituo vyao.

MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya mafunzo ya amali katika vituo vilivyoanzishwa na Serikali na mashirika binafsi.

Mhe. Spika, Vituo vya Mafunzo ya Amali vya Mkokotoni katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Vitongoji, Mkoa wa Kusini Pemba. Vimeanza kazi zake baada ya kufunguliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzíbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Amani Abeid Karume tarehe 27 na 29 Septemba, 2009.

Pia Kituo cha Kazi za Amali cha Mwanakwerekwe kimeeendelea kutoa mafunzo mbali mbali. Kwa Jumla vituo hivyo vina jumla ya wanafunzi 449 kati yao wanawake 170 wanaume 279 wanaojifunza fani mbalimbali. Jadweli Na. 40(a) inatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali pia inaratibu shughuli mbali mbali za maendeleo ya mafunzo ya amali ikiwemo mitihani ya biashara "*National Bussiness Examination* (NABE)" na ile ya Ufundi Stadi (*Trade Test na CBET*) inayotayarishwa na Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi ya Tanzania Bara (VETA). Jumla ya vijana 976 kati ya hao 244 ni wanawake na 732 ni wanaume walifanya mitihani hiyo kama inavyoainishwa katika Jadweli Na.41 (a- b).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2010/2011, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzíbar inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Amali na Mafunzo ya mwaka 2005 na Sheria ya Mafunzo ya Amali Namba 8 ya 2006;
b. Kuijengea uwezo Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Bodi ya Wakurugenzi ya Mafunzo ya Amali kwa mujibu wa Sheria ya Mafunzo ya Amali Na. 8 ya 2006;
c. Kuanza ujenzi wa Ofisi Kuu ya Mamlaka;
d. Kukagua na kusajili upya vituo vyote vya mafunzo ya amali hapa Zanzibar;
e. Kujenga uzio katika vituo vya mafunzo ya amali, Mkokotoni na Vitongoji;
f. Kuendelea kuielimisha jamii kuhusu muundo na taratibu, mipaka na majukumu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Bodi ya Wakurugenzi ya Mafunzo ya Amali kwa mujibu wa Sheria ya Mafunzo ya Amali Na. 8 ya 2006;
g. Kuiimarisha Mamlaka kwa kuongeza wafanyakazi na kuipatia vitendea kazi na usafiri wa uhakika ili kuweza kufanya kazi mbali mbali za ufuatiliaji, mafunzo na shughuli nyengine za Mamlaka kwa ufanisi zaidi;
h. Kuongeza uwezo wa wafanyakazi wa Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo kwa mujibu wa kazi na fani zao ndani na nje ya nchi;
i. Kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu na mafunzo ya viwandani kwa walimu watakaofundisha vituo vyote vya mafunzo ya amali vilivyosajiliwa na Mamlaka;
j. Kununua vifaa, zana, nyenzo na mitambo ya uzalishaji na ya kufundishia kwa lengo la kutoa mafunzo kwa walimu watakaofundisha vituo vyote vilivyosajiliwa na Mamlaka;
k. Kutoa na kusimamia mafunzo ya amali kwa vijana 1500 katika vituo mbali mbali vya mafunzo ya amali ndani na nje ya nchi;
l. Kuratibu upatikanaji wa nafasi za mafunzo ya amali kwa vijana katika vituo mbali mbali vya mafunzo ya amali ndani na nje ya nchi;
m. Kutoa mafunzo ya stadi za maisha kwa wakufunzi, wafanyakazi na wanafunzi wa vituo vya mafunzo ya amali;
n. Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wakufunzi, wafanyakazi na wanafunzi wa vituo vyote vya mafunzo ya amali vilivyosajiliwa;
o. Kuendeleza uhusiano na mashirikiano kati ya Mamlaka na Mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusika na Mafunzo ya Amali.
p. Kutafuta maeneo ya uzalishaji na uwekezaji ili kuongeza mapato ya Mfuko wa Maendeleo ya Mafunzo ya Amalil; na
q. Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa mafunzo ya amali kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu pamoja na sera na sheria zinazotawala utoaji na mafunzo ya amali na ajira.

IDARA YA NYARAKA, MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

Hifadhi za Nyaraka na Tafiti

Mhe. Spika, Divisheni ya Nyaraka na Kumbukumbu iliendelea na kazi zake za kawaida za kuhudumia watafiti na ukusanyaji wa kumbu kumbu katika Maofisi mbali mbali ya serikali. Jumla ya watafiti 90 wa ndani na nje waliendesha tafiti zao na kupatiwa huduma mbali mbali.

Shughuli za utafiti zilifanyika katika mapango ya Kale ya Kiwengwa (Unguja) na pango la Makangale (Pemba). Pia jumla ya nyaraka 66 zilizokuwa katika hali mbaya zilifanyiwa matengenezo ya kitaalamu.

Aidha Taasisi mbali mbali zikiwemo, Wizara ya Maji, Ujenzi Nishati na Ardhi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mahakama za Chake Chake, Wete na Mkoani, Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana, Wizara ya Kilimo na Mazingira, na Wizara ya Afya zilikaguliwa na kupatiwa huduma za kitaalamu, kwa kufanyiwa tathmini na kupewa ushauri juu ya uhifadhi bora wa Nyaraka.

Mhe. Spika, ushauri na mafunzo mafupi yametolewa kwa wafanyakazi wa taasisi za serikali wa masjala kuhusu kuimarisha mfumo wa uhifadhi wa kumbu kumbu.

Taasisi zilizopatiwa ushauri, kwa upande wa Unguja ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati; Chuo cha uandishi wa Habari; Ofisi ya Mkuu wa wilaya Mjini; Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ; na mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa Chuo cha Utawala wa Umma.

Kwa upande wa Pemba ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mahkama ya Mkoani, Mahkama ya Chake Chake na Idara ya Ardhi na usajili.

Mambo ya Kale

Mhe. Spika, kazi za matengenezo ya Magofu ya Kale kupitia mpango shirikishi wa Jamii – *MACEMP*/*TASAF* Unguja na Pemba ziliendelea vyema. Mpaka kufikia mwezi wa Mei, jumla ya maeneo 11 yamekamilisha kazi zao. Maeneo hayo ni : Chwaka–Tumbe,Ole-Mandani, Mkumbuu, Chambani-Mjini, Mkomani- Vitongoji na Pujini kwa upande wa Pemba. Kwa Unguja ni : BiKhole – Bungi,Maruhubi,Pango la Kuumbi,Pango la Machanga na Fukuchani. Wakati huo huo zoezi la kuyapima na kuyapatia hatimiliki maeneo ya Kale ziliendelea vyema. Mpaka sasa jumla ya maeneno 37 Unguja 15 na Pemba 22 yameshapimwa.

Mhe. Spika, kazi za kuweka mabango ya maelezo *(Information Boards*) na alama (*Sign Boards*) ziliendelea. Jumla ya maeneo 18 yamewekewa taarifa ambayo ni Magofu ya Maruhubi, Mangapwani, Mwinyi –Mkuu, Dunga, Unguja – Ukuu, Mwana-Mpambe, kwa upande wa Unguja na Pemba ni : Kimeleani-Fundo, Pango la Makangale, Mabaki ya athari za Utumwa–Mgagadu,Mgoli–Piki,Shamiani–Mwambe, Mkumbuu, Mkamandume, Mtule-Kengeja, Mitondooni, Kisiwa – Panza, kwa Bi Popo – Makoongwe. Taratibu za kupatiwa hatimiliki kwa baadhi ya maeneo yaliyokwisha pimwa zimekamilika.

Maeneo yafuatayo tayari yameshaombewa Hati Miliki nayo ni : Msikiti wa Kale – Kizimkazi, Magofu ya Kale-Kizimkazi, Msikiti wa Shakani, Eneo la Kale-Chwaka, Magofu ya Fukuchani, Magofu ya Dunga, Gofu la Kizimbani, na Mvuleni.

Mhe. Spika, pia Msikiti wa Kale wa Kizimkazi – Dimbani umefanyiwa matengenezo makubwa kutokana na msaada wa Serikali ya Marekani wa US$ 21,500 na sasa umo katika hali nzuri. Shughuli za Utafiti zilifanyika katika mapango ya Kale ya Kiwengwa Kaskazini – Unguja na Pango la Makangale. Pia Kitabu maalum cha *"Zanzibar and the Swahili Coast 30,000 Years Ago"* kimechapishwa kutokana na matokeo mazuri ya utafiti wa Pango la Kuumbi.

Makumbusho

Mhe. Spika, licha ya kukabiliwa na tatizo la umeme lililochukua karibu miezi mitatu Makumbusho zetu za Beit-el-Ajaib, ya Kasri na Mnazi mmoja ziliendelea na huduma zake ambapo jumla ya Wageni 23,219 wa nje na ndani, wengi wao wakiwa wanafunzi wa skuli. Jumla ya skuli 165 zenye jumla ya Wanafunzi 12,896 na Walimu 710 walitembelea Makumbusho za Beit- el- Ajaib n aya Kasri.

Makumbusho zimeiingiza jumla ya US$ 12,276 sawa na shilingi 16,185,836.64 na Shilingi za kitanzania 39,411,943.00 hadi mwezi Februari,2010. Kati ya wageni hao, kulikuwa na wageni rasmi 74 wa Serikali, wakiwemo Viongozi wa Kitaifa na Kimataifa kutoka nchi mbalimbali.

Mhe. Spika, baadhi ya sehemu za Makumbusho ya Kasri zilizokuwa katika hali mbaya zilifanyiwa matengenezo na sasa hali yake inaridhisha.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi Sita walipelekwa masomoni katika Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam kwa mafunzo ya Diploma ya Hifadhi za Makumbusho na vitu vya Kale.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo :-

i) Kukamilisha zoezi la kuyapatia hati miliki maeneo yaliyobakia;
ii) Kuendeleza zoezi la kuweka vielelezo katika maeneo ya kale;
iii) Kuifanyia matengenezo makubwa Makumbusho ya Kasri – Forodhani;
iv) Kuufanyia matengenezo ukuta wa Kihistoria. Eneo la Kale – Maruhubi;
v) Kuendelea na zoezi la kuanzisha Makumbusho za Kanda Chwaka, Tumbe, Mkumbuu, Fukuchani na Kuumbi;
vi) Kuendeleza Tafiti za Kale hasa katika mapango likiwemo Pango la Kiwengwa;
vii) Kuendeleza zoezi la uhifadhi bora wa Nyaraka na Kumbukumbu katika Taasisi za Serikali kwa mafunzo na ushauri;
viii) Kukamilisha kazi za matengenezo makubwa za Makumbusho ya Beit – El- Ajaib, Mnazi – Mmoja na Gofu la Mtoni; na
ix) Kuifanyia matengenezo Nyumba ya Watumwa – Mangapwani.

KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2009/2010 Kitengo cha Elimu Mjumuisho kimeweza kutekeleza shughuli kwa kutoa kipaumbele katika kuandaa sera ya Elimu Mjumuisho, kuwajengea uwezo walimu juu ya taaluma ya elimu mjumuisho na kununua na kusambaza vifaa kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mhe. Spika, rasimu ya Sera ya Elimu Mjumuisho imeandaliwa kwa kuwashirikisha washirika mbali mbali zikiwemo taasisi za kiserikali na zisizokuwa za kiserikali. Rasimu ya Sera hiyo imewasilishwa wizarani kwa kujadiliwa na inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu.

Mhe. Spika, jitihada za kuwajengea uwezo walimu ili waweze kufundisha katika mazingira ya mjumuisho zinaendelea. Kwa mwaka 2009/2010, Jumla ya walimu 2,390 wakiwemo wanaume 808 wanawake 1,582 walipatiwa mafunzo ya lugha ya alama na '*Braile'*.

Aidha mafunzo ya elimu mjumuisho yanaendelea kutolewa huko Chuo cha Kiislamu, Mazizini na kwa mwaka 2009/2010, walimu 51 wamejiunga na mafunzo hayo katika ngazi ya cheti. Walimu 8 wamejiunga na mafunzo kama hayo katika ngazi ya stashada na shahada katika vyuo vya Tanzania Bara na Uganda.

Mhe. Spika, vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu vimenunuliwa na kugaiwa katika skuli zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa vyenyewe ni mashine za kuandikia wanafunzi wasioona na karatasi zao, baiskeli za magurudumu matatu, miwani na fimbo nyeupe kwa ajili ya wasioona. Aidha kitengo kimeendelea kuhamasisha jamii kwa kushirikiana na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili na wadau wengine ili wazazi wawapeleke skuli watoto wenye mahitaji maalum.

Mhe. Spika, hatua zetu za uendelezaji wa Elimu Mjumuisho zimeweza kuwavutia wageni mbali mbali. Katika mwaka 2009/2010, Zanzibar ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano wa Mtandao wa Afrika kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu wa akili ambao ulikuwa na Ujumbe wa Elimu Mjumuisho. Mkutano huo uliamuliwa ufanyike Zanzibar kutokana na kilio cha muda mrefu cha wajumbe wa mtandao huo kutaka kuona jinsi Zanzibar ilivyopiga hatua katika utekelezaji wa Elimu Mjumuisho.

Aidha, ugeni mwingine ulitoka Kenya, katika taasisi Jumuia inayoshughulikia watoto wanaoishi katika mazingira magumu na Jumuiya inayoshughulikia watoto viziwi. Aidha Kitengo kilipata mialiko mbali mbali kutoka nje inayohusu uimarishaji wa elimu mjumuisho iliyofanyika Tanzania Bara na Zambia.

Mhe. Spika, kitengo kinaendelea na juhudi zake za kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum waliofikia umri wa kwenda skuli wanaandikishwa ili kupata haki yao ya msingi ya elimu. Kwa mwaka 2010/2011 idadi ya wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa imefikia 421 katika skuli zote za Unguja na Pemba. Aidha Kitengo kitaendelea na utekelezaji wa shughuli zake kama zilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa elimu kama ifuatavyo:-

- Kukamilisha Sera ya Elimu Mjumuisho, ambayo itakuwa dira ya utekelezaji wa Elimu Mjumuisho Zanzibar;
- Kuendelea kutoa mafunzo ya Lugha ya alama na Braille ili wanafunzi viziwi na wasioona waweze kujifunza kwa ufanisi zaidi; na
- Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuvisambaza kwa wanaovihitaji.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wa kimaendeleo wa ndani na wa nje wa nchi kwa michango yao iliyofanikisha utekelezaji wa elimu Mjumuisho. Washirika wenyewe ni Jumuia kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu Akili Norway (*NFU*), Shirika la Maendeleo la Norway (*NORAD*). Jumuiya kwa Ajili ya watu wenye Ulemavu wa Akili Zanzibar (*ZAPDD*). Shirika *Sight Savers International (SSI)*. Mradi wa kuendeleza Elimu Tanzania (*CREATE*). Agakhan Foundation na *USAID*, UWZ, ZANAB. Chama cha Maalbino, CHAVIZA na wote ambao majina yao hayakutajwa.

KITENGO CHA URAJIS

Sheria ya Elimu

Mhe. Spika, katika kutekeleza Sera mpya ya Elimu ya mwaka 2006, wizara imeandaa Rasimu ya Sheria mpya ya Elimu. Rasimu hiyo ya sheria imeandaliwa kwa kukusanya michango kutoka washirika mbali mbali wa elimu wakiwemo walimu, wajumbe wa kamati za skuli, masheha, watu maarufu na wasomi. Hivi sasa rasimu hiyo inafanyiwa marekebisho kabla ya kuwasilishwa katika vyombo vya juu vya serikali na hatimaye kuletwa katika Baraza lako tukufu.

Kesi za Ardhi za Skuli

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 Afisi ya Mrajis imeshughulikia kesi mbili, ambazo zinahusiana na kuvamiwa maeneo ya skuli. Moja ya kesi hizo ni ya skuli ya Kizimkazi Mkunguni na nyengine ni ya Skuli ya Welezo *(Makofi)*.

Leseni za Walimu

Mhe. Spika, afisi iliendelea kushughulikia maombi ya leseni za walimu, Jumla ya walimu 597 walipatiwa leseni za kusomesha katika skuli za serikali na za binafsi, kati yao walimu 412 waliosomea na 185 wasiosomea

Maombi ya Usajili wa Skuli

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, wizara ilipokea maombi 9 ya usajili wa skuli za serikali na skuli 20 za binafsi. Skuli zote hizo zilifanyiwa ukaguzi na kutolewa tarifa ya mambo yaliyoonekana. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Afisi ya Mrajis wa Elimu itaendelea kushughulikia maombi ya usajili wa skuli za serikali na za binafsi.

Kesi za ujauzito na Ndoa za Wanafunzi

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, kesi 37 za ndoa za wanafunzi ziliripotiwa na kati ya hizo kesi 7 zilikuwa baina ya wanafunzi kwa wanafunzi. Pia kulikuwa na kesi 16 za ujauzito za wanafunzi ziliripotiwa, ambapo kesi 3 zilikuwa baina ya wanafunzi kwa wanafunzi. Idadi ya kesi za ujauzito na ndoa zimepungua ukilinganisha na kesi 84 zilizoripotiwa katika mwaka 2008/2009.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, kitengo hiki kitaendelea kushughulikia kesi za ujauzito kwa mujibu wa Sheria Nam. 4 ya 2005 ya kuwalinda Wari na Watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Pia kitaendelea kushughulikia kesi za ndoa za wanafunzi kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982.

Mapato

Mhe. Spika, hadi mwezi Machi 2010, kitengo hiki kiliingizia mapato yenye jumla ya Shilingi 5,227,300/. Kati ya mapato hayo shilingi 2,715,800/- zimetokana na usajili wa skuli, ada ya usajili wa wanafunzi na Fomu ya usajili na shilingi 2,511,500/- zimetokana na mauzo ya leseni za walimu na kuongeza muda. Katika mwaka 2010/2011, Kitengo kitaendelea kukusanya mapato ya usajili wa skuli za binafsi, na leseni za walimu.

Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Bodi za Mikoa na Wilaya zilifanya vikao vya kuzungumzia maendeleo ya elimu katika Mikoa na Wilaya. Bodi hizo hukutana kwa kujadili mambo mbali mbali ikiwa pamoja na kufanya tathmini ya matokeo ya mitihani mbali mbali. Vikao vya bodi vimeweza kusaidia sana katika kusukuma maendeleo ya elimu katika maeneo yanayohusika. Katika mwaka 2010/2011, Bodi hizo zitaendelea na vikao vyao kujadili mambo mbali mbali kuhusu elimu.

Baraza la Elimu

Mhe. Spika, Baraza la Elimu lilifanya kikao chake cha kawaida kujadili mambo mbali mbali ikiwa pamoja na suala la udanganyifu katika mitihani. Wajumbe wa Baraza walitoa maoni yao ya jinsi ya kuzuia wimbi la udanganyifu katika mitihani na kuwasilisha maoni hayo Wizarani.. Katika mwaka 2010/2011,Baraza la Elimu litaendelea na kazi zake kama kawaida na kuishauri Wizara ipasavyo kuhusiana na maswala mbali mbali ya maendeleo ya elimu.

KITENGO CHA USHAURI NASAHA

Mhe. Spika, Kitengo hiki kina majukumu ya kutoa ushauri nasaha, na kusaidia kutatua matatizo ya wanafunzi yanayowarejesha nyuma katika masomo yao, Kwa mwaka wa 2009/2010, kitengo kwa kushirikiana na Kamati ya UKIMWI ya Wizara, kimeweza kutoa mafunzo ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia na ukimwi kwa walimu 150 wa masomo ya sayansi wa sekondari na msingi wa skuli za serikali na za binafsi, na walimu wakuu na wenyeviti wa kamati za skuli 70. Aidha, Kitengo kwa kushirikiana na Wizara ya Vijana, Ajira, Wanawake na Watoto kiliweza kutoa mafunzo kama hayo kwa wanafunzi 1,800 wa skuli mbali mbali, kwa wilaya zote za Unguja. Aidha, Kitengo kilishiriki katika kutoa mafunzo ya ushauri nasaha kwa viongozi wa vilabu vya afya 48 kutoka skuli mbali mbali za Unguja na Pemba, wakiwemo wanawake 24 na wanaume 24.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, kitengo hiki kitaendelea kuhamasisha umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike, kwa washirika mbali mbali wa elimu hasa wazee, kutoka wilaya tofauti za Unguja na Pemba na pia kutoa mafunzo na kutoa ushauri nasaha katika kupambana na ajira za watoto, mimba za utotoni, ndoa za mapema, kubakwa na

matatizo ya ujana na malengo yao baada ya masomo kwa maisha yao ya baadae.

KITENGO CHA UKAGUZI WA HESABU ZA NDANI

Mhe. Spika, Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani cha Wizara kina jukumu la kukagua hesabu za mapato na matumizi katika Idara zote za Wizara na skuli zote za Serikali za Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2009/2010, kitengo kimeweza kukagua hesabu zote za ndani katika makao makuu ya Wizara pamoja na kufuatilia vifaa vilivyopelekwa katika skuli mbali mbali ambavyo hununuliwa kutoka bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo, ili kuangalia thamani halisi ya bidhaa zilizopelekwa na ujenzi uliofanyika. Kitengo pia kimeweza kukagua skuli 60 za maandalizi, msingi na sekondari. Aidha Kitengo kimekagua Taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku ambazo hujitegemea katika kutekeleza mipango yake. Taasisi hizo ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Idara ya Maktaba

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2009/2010, Kitengo kimeandaa mwongozo wa usimamizi wa fedha kwa walimu wakuu na washika fedha wa skuli za Unguja na Pemba ili kufanikisha usimamizi wa michango inayotolewa na wazazi kwa maendeleo ya skuli.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara kupitia kitengo hiki itaendelea kufanya ukaguzi wa mahesabu ya Idara zake na skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

KITENGO CHA MICHEZO NA UTAMADUNI

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 kitengo kimeendelea kutoa mafunzo ya michezo mbali mbali ikiwemo ya mpira wa kikapu na mpira wa wavu kwa walimu mbali mbali wa Wilaya za Unguja na Pemba. Mafunzo hayo ya muda mfupi yalitolewa kwa kuwatumia wataalamu wa ndani na nje hasa kutoka Marekani. Katika mafunzo hayo walimu walijifunza mbinu mbali mbali za namna ya kuwafundisha wanafunzi mbinu za michezo hiyo. Aidha kitengo kilishirikiana na Idara ya Mitaala na Mitihani katika kuandaa muhutasari huo uliozingatia matakwa ya michezo ili kuibua vipaji vya wanafunzi vilivyojificha katika fani ya michezo kuanzia ngazi ya msingi

Mheshimiwa Spika. Kitengo kimefanya tathmini ya mafunzo ya michezo yanayotolewa na walimu wetu katika skuli mbali mbali za hapa Zanzibar. Tathmini

hiyo ilifanywa kwa kuwashirikisha wanafunzi katika mashindano ya michezo mbali mbali kuanzia ngazi ya kanda, wilaya, mkoa na hatimaye taifa katika tamasha la elimu bila ya malipo. Pia wanafunzi ambao walionyesha vipaji vya juu katika michezo ya riadha na mpira wa kikapu waliteuliwa kuunda timu ya Zanzibar iliyoshiriki mashindano ya *UMISETA* yaliyofanyika huko Kibaha Tanzania Bara.

Vijana hao waliiwakilisha vyema Zanzibar na kufanikiwa kupata nafasi za kwanza hadi za tatu katika mbio mbali mbali walizoshiriki na nafasi ya pili kwa upande wa Mpira wa Kikapu. Hii inadhihirisha kwamba vijana wetu wana vipaji vya kutosha ambavyo vinahitaji kuendelezwa. Katika mwaka 2010/2011, wanamichezo 105 watashiriki katika mashindano ya *UMISETA* yatayofanyika Kibaha, Tanzania Bara kuanzia tarehe 20 hadi 30 Juni 2010

Mhe.Spika, kwa mwaka 2010/2011, kitengo cha Michezo na Utamaduni kina lengo la kuendelea kuwapatia taaluma ya michezo walimu wa fani mbali mbali za michezo katika skuli zetu za Unguja na Pemba. Aidha kuendelea kutoa mashirikiano na misaada mbali katika kuhakikisha mtaala wa somo la michezo unatekelezwa na kufuatwa katika skuli zote kwa kushirikiana na Idara ya Mitaala na Mitihani pamoja na Idara ya Ukaguzi wa

Elimu. Lengo ni kutoa wachezaji wenye taaluma ya michezo mbali mbali. Pamoja na hayo kitengo kimekusudia kuendelea na utaratibu wa kufanya tathmini ya mwaka ya michezo inayofundishwa na kuchezwa na wanafunzi wetu katika skuli mbali mbali kwa kuandaa Tamasha la Elimu Bila ya Malipo na kuwashirikisha wanafunzi wenye vipaji vya juu zaidi katika timu za Taifa za wanafunzi zinazoshiriki katika mashindano mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, kitengo kitaandaa mafunzo kwa wanafunzi yatakayohusiana na UKIMWI na madawa ya kulevya kupitia michezo ili kusaidia kupunguza kazi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na matumizi ya madawa ya kulevya kwa vijana na kuwafanya vijana wawe karibu zaidi katika shughuli za michezo badala ya kujiingiza katika anasa na starehe zitakazowapelekea kuharibu mustakbal wa maisha yao ya baadae na kurejesha nyuma maendeleo ya taifa.

KITENGO CHA UNUNUZI NA UGAVI

Mhe. Spika, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi *(Procurement Management Unit)* ambacho ndicho Sekretariati ya Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Amali kinaendelea kufanya kazi zake vizuri. Katika mwaka 2009/2010, Kitengo kwa kushirikiana na Bodi ya Zabuni kilitayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini jumla ya tenda 34 za manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi zenye thamani ya jumla ya TShs. 44,446,934,650/-. Miongoni mwa zabuni hizo ni za ujenzi wa Skuli 15 za Sekondari za vijijini kwa Unguja na Pemba, ambazo jumla ya skuli 8 zitajengwa Unguja na 7 Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Kitengo kinakusudia kutayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini tenda zinazohusiana na ujenzi wa skuli mpya za ghorofa 3 za Sekondari katika mkoa wa Mjini-Magharibi, ujenzi wa kampasi mpya ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa huko Mchangamdogo Pemba na upanuzi wa Skuli ya Shamiani Pemba. Pia Kitengo kinakusudia kutayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini tenda zinazohusiana na ukarabati mkubwa wa skuli 6 za Sekondari za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Kitengo pia kinakusudia kutayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini tenda za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa madarasa 120 kwa Unguja na Pemba. Jumla ya madarasa 72 yatajengwa Unguja na 48 yatajengwa Pemba.

BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA

Mhe. Spika, mojawapo ya jukumu la Bodi ya Huduma za Maktaba ni kusambaza huduma za maktaba katika sehemu zote za Zanzibar. Hivi sasa Maktaba Kuu inatoahuduma zake katika mazingira mazuri na inahudumia watu wengi zaidi. Mbali ya kuazimisha vitabu, Maktaba Kuu imeanza kutoa huduma za maktaba kwa njia ya mtandao ili kuwawezesha watumiaji kupata vitabu viliomo katika "*e-book library*" za vyuo vikuu mbali mbali duniani. Kwa kufanikisha zoezi hilo Shirika la Huduma za Maktaba limejiunga na ushirikiano wa maktaba za Tanzania (*consortia)* iitwayo *COTUL* ambayo itakuwa wakala wa kuruhusu majarida na vitabu vya e-library kutoka Shirika la *INASP* na kuwezesha maktaba kupokea na kusoma majarida hayo.

Mhe. Spika, Shirika la Huduma za Maktaba kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzíbar imeanzisha mafunzo ya awali ya ukutubi ambayo huendeshwa katika Chuo Kikuu cha Taifa kwa muda ya miezi mitatu.. Lengo kuu ni kuendelea kushirikiana na kuweza kuanzisha mafunzo ya Cheti cha Ukutubi katika Taasisi hiyo.

Mhe. Spika, Shirika lilipokea msaada wa vitabu na samani kutoka mashirika mbali mbali kama vile *NGO ya AHAS* kutoka Denmark na Book Aid International kutoka

Uingereza. Vitabu vilivyopatikana vimegaiwa kwa skuli mbali mbali na taasisi za elimu ya juu kama vile vyuo vikuu viliopo hapa nchini. Vile vile kutokana na mafanikio ya utoaji wa huduma za maktaba kwa njia ya maboksi kwa skuli za majaribio, washirika wetu *"Book Aid International"* imeamua kuendelea kutoa msaada zaidi ili skuli nyingi zaidi zifaidike na mradi huo.

Mhe. Spika, Ili kuongeza ufanisi wa huduma zinazotolewa na Maktaba Kuu na tawi lake liliopo Chake Chake wafanyakazi wamepatiwa nafasi za mafunzo katika Chuo cha Ukutubi huko Tanzania Bara na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)* . Pia wafanyakazi waliopo kazini wanashiriki katika semina za kuwaongezea ujuzi wa kazi zao.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2010/2011, Bodi ya Huduma za Maktaba itashirikiana na NGO ya Mjumuiko wa Jumuiya za Kijamii Zanzibar - *MJUKIZA* kuziimarisha maktaba za kijamii *(Community libraries)* katika mtaa wa Kiembe Samaki na Chumbuni na kuanzisha nyengine katika maeneo tofauti ya kisiwa cha Unguja. Hali kadhalika Shirika litaimarisha huduma zake katika kitengo cha *American Corner* kichopo katika Maktaba kuu ya Chake Chake ili kutoa fursa zaidi kwa wananchi kukutana na kujadili mambo ya maendeleo na kutumia fursa ziliopo kwa kujielimisha zaidi.

MAPATO

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya TShs 150,000,000/- kutoka vianzio vya idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale, na Ada za leseni za walimu pamoja na uandikishaji wa skuli za binafsi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010, TShs 60,825,080.64/- zilikusanywa na kuwasilishwa ikiwa sawa na asilimia 41% ya makadirio. Kati ya fedha hizo TShs. 55,597,779.64/- zilitokana na vianzio kutoka Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale na TShs 5,227,300/- kutokana na ada za leseni za walimu na uandikishaji wa skuli binafsi. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakusudia kukusanya jumla ya TShs 135,720,000/= na kuziwasilisha Hazina.

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa

ufanisi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla TShs 47,093,000,000/= kati ya hizo TShs. 4,475,000,000/- ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na TShs 42,618,000,000/= zilizobakia ni kwa ajili ya kazi za kawaida. Jadweli Nam 47 na 48 zinachambua zaidi.

MWISHO

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba yangu napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, viongozi wote wa mikoa, wilaya, Majimbo, Shehia na wananchi wote kwa ujumla wakiwemo wananchi wa jimbo langu la Makunduchi kwa misaada na mashirikiano yao ya dhati waliyonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Halikadhalika ninaishukuru Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ushirikiano mkubwa iliyotupa wakati wote wa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Pia napenda kuwashukuru walimu na wafanyakazi wote kwa bidii wanayoionesha katika kutekeleza majukumu yao licha ya changamoto mbali mbali zinazowakabili. Pia, pongezi na shukrani nyingi ziwaendee wanafunzi wote wa skuli za Serikali na za binafsi za Unguja na Pemba kwa kuwa watulivu, wenye nidhamu na kuonesha juhudi kubwa katika masomo yao.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa uvumilivu na kwa utulivu mkubwa. Vile vile natanguliza shukrani zangu za dhati kwao kwa michango watakayoitoa katika kujadili hotuba hii ambayo nategemea itakuwa ya msaada mkubwa kwangu kwa wizara yangu na kwa Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, tarehe 19 Jun, 2010 nilitangaza nia yangu ya kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi ujao, nimechukua fomu tarehe 24 Jun, 2010 nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakichangia hotuba hii waelewe kuwa ninakabiliwa na jambo hilo hivyo wasinichoshe sana kwani kuna kazi ambayo inanikabili mbele yangu

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mwenyekiti kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na Mwenye kurehemu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa min-ajili ya kuijadili Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri alivyotangulia kutoa maelezo yake kwamba tusimchoshe sana mimi nampongeza tu kuwa ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi ambae ana haki ya kuomba ridhaa kwa wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, kwa kuitikia kugombea kiti cha urais wa Zanzibar nampongeza sana.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa, napenda pia kushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yetu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Khamis Jabir Makame, kwa uchapakazi wao unaosaidia kukamilisha utekelezaji wa malengo ya kielimu ya Wizara hii. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kuwasilisha mbele ya Kamati yetu Taarifa ya bajeti ya Wizara yao. Kamati iliridhishwa na mashirikiano yaliyoonyeshwa na Watendaji wa Wizara hii wakati wa kujadiliwa bajeti yao mbele ya kamati yetu.

Mhe. Spika, **k**imsingi, Kamati yetu imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa yanayoleta tija na ufanisi wa hali ya juu. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kuijadili bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa umakini na umahiri wa hali ya juu. Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
Mhe. Ali Hají Ali	-	Mjumbe
Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
Mhe. Haji Faki Shaalí	-	Mjumbe
Mhe. Hasnuu Moh'd Hají	-	Mjumbe
Mhe. Moh'd Ali Salim	-	Mjumbe
Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe

Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu
Ndg. Salmin Amour Abdalla	-	Katibu

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la wanafunzi na mahitaji ya Wizara kwa ujumla, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeongeza matumizi ya sekta hii ya Elimu hadi kufikia asilimia 15.6 ya bajeti ya Serikali kuu ambayo ni jumla ya shilingi 33,224,000,000/=. Tunaipongeza Serikali kwa kuijali sana sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepania kwa dhati kabisa kuleta maendeleo ya Elimu hapa Zanzibar kwa kuongeza idadi ya taasisi za elimu na kuhakikisha ubora wa taasisi hizo. Hadi kufikia mwaka 2010, taasisi hizo za Serikali na binafsi zimefikia 657.

Mhe. Spika, Kamati ilipokea kwa furaha taarifa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesimamia kupatikana kwa maslahi zaidi ya walimu, ambapo hivi karibuni walimu wa visiwa hivi walipatiwa nyongeza maalumu ya mishahara. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa jitihada zaidi zinahitajika ili kuwajengea mazingira mazuri zaidi walimu wa Zanzíbar kwa nia ya kukuza maendeleo ya elimu na kuwadhibiti walimu wasikimbilie Tanzania Bara kwa kufuata maslahi yaliyo bora zaidi. Ni ukweli ulio bayana kuwa Walimu wengi wa Zanzibar wamekuwa wakikimbilia Tanzania Bara na maeneo mengineyo duniani kwa madhumuni ya kutafuta maslahi bora zaidi. Kwa mantiki hii, ikiwa tutashindwa kuwadhibiti walimu wetu kwa kuwaongezea maslahi bora zaidi basi walimu wengi wazuri na wenye uzoefu wanaweza kutukimbia na hatimae wanafunzi wetu kuendelea kufeli katika mitihani ya kidatu cha nne na sita.

Mhe. Spika, Kamati yetu imesikitishwa mno na migogoro isiyo ya lazima inayotokea mara kwa mara baina ya viongozi wa chama cha walimu *(ZATU)* na Wizara ya Elimu. Kwa vile pande zote hizi ni mihimili ya kukuza maendeleo ya elimu nchini, tunashauri zikutane pamoja na kujadili kwa kina chanzo cha migogoro hiyo ili hatimaye ufumbuzi upatikane.

Mhe. Spika, Sekta ya Elimu ndiyo muhimili mkuu wa maendeleo ya nchi yeyote duniani. Hakuna hata nchi moja iliyoendelea duniani ilhali watu wake wanaipuuza elimu. Kutokana na umuhimu wa elimu katika kukuza uwajibikaji na maendeleo yakinifu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzíbar imejipangia kufanya kazi zake kikamilifu kupitia Idara zake kwa matumizi ya jumla ya shilingi za Kitanzania 47,093,000,000/=.

Mhe. Spika, tunaipongeza Wizara ya Elimu kwa upanuzi na uimarishaji wa huduma za maktaba nchini ambapo hivi karibuni jengo jipya la maktaba kuu Unguja lilifunguliwa . Aidha, Kamati imeridhishwa na maelezo kuwa Wizara imetenga kiasi cha shilingi milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=) kwa ajili ya ununuzi wa samani na kufanya maandalizi ya ujenzi wa maktaba kuu kisiwani Pemba. Kamati inaitaka Wizara kuchukua kila juhudi ili kukamilisha ujenzi wa maktaba Pemba kwa haraka itavyowezekana. Kama ilivyo kwa Unguja, wananchi wa Pemba nao wana kila haki ya kupata huduma za kimaktaba. Katika dunia ya leo inayokimbilia katika kilele cha sayansi na teknolojia, huduma za maktaba ni muhimu mno kwa shabaha ya kukuza ufahamu wa watu wetu katika kujikombowa kiuchumi na kukuza maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mashirikiano makubwa na benki ya Kiarabu ya maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Wizara imefanikiwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa chuo kikuu cha Taifa cha Zanzíbar huko Tunguu. Hadi kukumilika kwake, mradi huo unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi 7,324,000,000/=.

Mhe. Spika, Mradi wa uimarishaji wa Elimu ya msingi hapa Zanzíbar ambao utagharimu kiasi cha shilingi 1,250,000,000/=. Hadi kufikia mwezi Mei, 2010 fedha zote za mradi huo zilipatikana pamoja na kujitokeza wafadhili wengine kutoka *UNICEF*, *UNESCO* na *NFU* ambao waliuimarisha zaidi mradi huo.

Mhe. Spika, Aidha, kumekuwa na tetesi kwamba Walimu zaidi ya 20 wa Skuli ya Msingi ya Fuoni hivi karibuni wamepewa uhamisho na kupelekwa katika skuli mbalimbali na hivyo kupelekea upungufu mkubwa wa walimu skulini hapo. Kamati inaomba ufafanuzi wa kina juu ya ukweli wa suala hili na sababu zilizopelekea uamuzi kama huo. Jee, Wizara haioni kuwa kuwahamisha walimu wengi kama hao ikiwa ni miezi michahe tu tuliyonayo kuelekea kwenye mitihani ya Taifa kunaweza kuwatia wasiwasi wanafunzi wetu?

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ujenzi wa skuli mpya ya Kijichi, Wilaya ya Magharibi Unguja, chini ya ufadhili wa Serikali ya watu wa China ambayo imefunguliwa rasmi tarehe 17 Juni, 2010. Kuanzishwa kwa skuli hii ya aina yake kutawawezesha wanafunzi wenye vipaji maalumu kuendelezwa na hivyo kujenga wataalamu watakaoendeleza jitihada zetu za kujikwamua na hali mbaya ya uchumi hapo baadaye.

Mhe. Spika, tunatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuendelea vyema na utekelezaji wa mradi wa Elimu mbadala na Amali, kwa mashirikiano makubwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*. Vituo vya amali vya Mkokotoni na Vitongoji vimeanza kutoa mafunzo tangu Febuari, 2010 ambapo jumla ya wanafunzi 390 wakiwemo wanawake 130

wanaendelea na mafunzo hayo katika fani za ushoni, ufundi Magari, uashi, useremala na upishi.

Baada ya mafanikio hayo makubwa kwa Wizara, mradi huu pia unatarajia kukamilisha ujenzi wa kituo cha elimu mbadala huko Wingwi mtemani-Pemba.

Mhe. Spika, Idara ya elimu ya juu imetengewa jumla ya shilingi 2,500,000,000/= kwa ajili ya kuwadhamini vijana wanaojiunga na vyuo mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha. Kwa kweli, kiasi hichi ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya hivi sasa. Tunaiomba Serikali iitizame Idara hii kwa jicho la huruma na kuiongezea kasma yake kila hali inaporuhusu kwani kuwekeza zaidi katika elimu ni njia sahihi ya kuelekea kwenye safari ya maendeleo.

Mhe. Spika, Taasisi tatu za fedha zimepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi 500,000,000/= ambazo zimekopeshwa kwa wajasiriamali 1,957. Wizara pia imetoa mikopo yenye thamani ya 446,000,000/= kwa *SACCOS* 23 abayo iliwanufaisha wajasiriamali 918.

Mhe. Spika, tunatoa pongezi zetu za dhati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuandaa mpango wa kuwapeleka wanafunzi nje ya nchi kwa nia ya kusomea fani za utafutaji na uchimbaji wa mafuta ili kuandaa wataalamu wazalendo watakaofanya kazi kwa maslahi ya Taifa lao na kupelekea ustawi wa jamii ya wazanzibari.

Mhe. Spika, Miundombinu ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta yoyote ile ya kijamii. Kwa kuzingatia hilo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilianzisha mradi wa ujenzi wa Makao makuu ya Wizara, ambapo hadi kufikia Mei 2010, asilimia 100% ya fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar zilikwishatolewa. Hatua ya ukamilishaji wa ujenzi huu inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Tunaishukuru Serikali yetu kwa mchango wake madhubuti katika kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Mhe. Spika, Jumla ya maeneo 37 yamepimwa Unguja na Pemba kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kumbukumbu za kihistoria na hifadhi ya mambo ya kale ambao umetekelezwa na SMZ kwa mashirikiano na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *MACEMP*. Mradi huo umetengewa jumla ya shilingi 48,800,000/= . Msikiti wa kale wa Kizimkazi umefanyiwa matengenezo makubwa. Makumbusho ya kanda yamejengwa katika maeneo ya kale ya Chwaka Tumbe, Mkumbuu, Fukuchani na Kuumbi. Matengenezo makubwa ya

majengo ya makumbusho ya Jumba la wananchi "*people's palace*", Beit el ajab na Mnazi mmoja yanatarajiwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya maendeleo kama *SIDA*, itaendelea kuuimarisha mfumo wa utoaji taarifa za kina za elimu kwa jamii na Taifa kwa ujumla ili kuwawezesha kutoa maoni na ushauri wao kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika**,** "Nyota njema huonekana alfajiri". Kwa kuijali kauli hiyo ya wahenga, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanzisha mradi wa uimarishaji wa elimu ya maandalizi, ambao alianza mwaka 2009/2010. Hadi kufikia Mei 2010, skuli mbili za maandalizi zimejengwa katika maeneo ya Potoa na Msuka na vitabu vya masomo ya maandalizi vimetayarishwa na kufanyiwa majaribio.

Wizara ilianzisha mradi wa utoaji wa elimu kwa njia ya redio kwa watoto wenye umri wa elimu ya maandalizi kwa kuanzisha kituo maalumu ambacho kilizinduliwa rasmi mnamo tarehe 3 Mei, 2010.

Kazi Kubwa ya kuwahamasisha wananchi kuanzisha skuli za maandalizi ilifanywa na jumla ya skuli za msingi 36 zimeanzisha madarasa ya maandalizi.

Mhe. Spika, Mradi wa kutoa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio kupitia kipindi cha "tucheze tujifunze" unaendelea vyema katika Wilaya ya Magharibi, Wilaya ya Kaskazini 'A' na Micheweni. Jumla ya wanafuni 3,140 wamenufaika na mradi huo kwa kupatiwa nafasi ya masomo ya darasa la kwanza mwaka, 2010.

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara imejiandaa kikamilifu kuanza matengenezo ya Skuli za Sekondari za Fide-castro, Hamamni, Tumekuja, Uweleni na Utaani kwa nia ya kuongeza ufanisi wa utoaji wa taaluma katika skuli hizo.

Mhe. Spika, tukijikita katika uimarishaji wa elimu ya ufundi, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 700,000,000/= kutoka mfuko wa Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar. Taasisi ya Karume ya sayansi na teknolojia imeimarishwa, skuli ya Sekondari ya ufundi ya Kengeja imefanyiwa matengenezo pamoja na kupatiwa vifaa vya karakana kupitia Maradi huu, na hivyo kuwaweka tayari wahitimu wa taasisi hizo kuhimili vishindo vya ushindani wa kiteknolojia vinavyoendelea kukua duniani kote.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa shughuli za kawaida, Wizara ilikadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 35,188,283,000/= Ambapo hadi kufikia mwezi Mei

2010, asilimia thamanini na nane (88.3%) ya fedha hizo zilitolewa. Huu ni mwelekeo mwema, kwani Serikali kuu imetilia maanani uimarishaji wa shughuli za Wizara hii, katika harakati za kujiletea maendeleo yetu.

Mhe. Spika, Uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya maandalizi umefikia asilimia thelethini na nne (34%) ya watoto wote wenye umri wa kwanza mafunzo hayo Ambapo zaidi ya asilimia hamsini ni watoto wa kike. Hii ni hatua muhimu kwani jamii imeonesha mwamko wa kuwapatia elimu ya maandalizi watoto na hasa wa kike.

Kwa upande wa elimu ya msingi, jumla ya wanafunzi walioandikishwa ni 227,911 ambayo ni sawa na asilimia 112.6 . Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendeleza mafanikio haya.

Elimu ya Sekondari ina jumla ya wanafunzi 80,056 sawa na asilimia sitini na sita (66.2%) ya wanafunzi wote waliohitajika kuwa katika ngazi hiyo. Ni jambo la kufurahisha sana kwamba zaidi ya nusu ya wanafunzi hawa ni wanawake, hali inayoashiria kwamba kweli Zanzíbar imekusudia kuleta ukombozi wa kweli wa mtoto wa kike.

Mhe. Spika, Vyuo vikuu vitatu tulivyonavyo hapa Zanzíbar vinaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wapatao 2,803 wa fani Mbaimbali Ambapo asilimia thelathini na tisa (39%) ni Wanawake.

Mhe. Spika, utekelezaji wa mpango wa Sera ya Elimu unaoambatana na kuwapatia mafunzo walimu katika fani mbalimbali unaendelea kama fani ya uchumi katika Elimu, ambayo ni muhimu kwa watendaji wa Wizara hii.

Aidha, Kamati inatoa wito kwa Wizara kuendelea na mikakati yake ya kutoa taaluma zaidi kwa walimu wa Sayansi na Hesabu kwa nia ya kuondoa kabisa tatizo sugu la upungufu wa walimu wa masomo hayo katika skuli zetu na kuwawezesha watoto wetu kuwa tayari kwa ushindani wa kisayansi na teknolojia katika ulimwengu huu.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na shirika la *USAID* na kampuni binafsi za za kimataifa, Wizara inaendelea kufanya juhudi za makusudi kuhimiza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano.
Mhe. Spika, Kwa mwaka huu wa fedha 2010/11, wizara inakusudia kutoa mafunzo kwa walimu wa vyuo vya Qur-an ili kuwapatia mbinu bora za kufundishia.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatoa shukurani kwa Wizara kwa kuipatia idara ya ukaguzi wa elimu basi jipya lililowawezesha kutekeleza kazi za ukaguzi katika skuli 166 kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Spika, Sheria ya Elimu Nam.6 ya mwaka 1982 imefanyiwa marekebisho na hadi sasa marekebisho hayo yamepelekwa kwa mwanasheria mkuu. Rasimu ya sheria hiyo itawasilishwa katika kipindi cha 2010/2011.

Aidha, mamlaka ya mafuzo ya amali na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia zimeanzishwa chini ya bodi ambazo zimeundwa kisheria.

Mhe. Spika, baada ya Maoni hayo ya Kamati, nawaomba wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya shilingi za Kitanzania 47,093,000,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 42,618,000,000/= ni kwa kazi za kawaida na shilingi 4,475,000,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, kabla sijawasilisha naomba kutoa maoni yangu kidogo tu Mheshimiwa kama dakika 2 tu, najua muda wenyewe hakuna.

Mhe. Spika, mimi kama mzazi lakini tunaamini katika nchi yetu mwanafunzi bado anahitaji elimu na elimu bora zaidi. Lakini pia Katika tunakotembelea katika sehemu mbali mbali huwa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii, tunapata maelezo mengi ya maendeleo ya elimu lakini kuna hii Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.

Mhe. Spika, elimu hii hivi sasa hivi tukifanya ukaguzi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu hasa vijijini kuna baadhi ya wazee wengi hawajui kusoma na wala hawajui kuandika. Tukiangalia wakati huu ni wakati muhimu sana kwa elimu yoyote japo mtu ajue kusoma ile a, e, I, o, u. Namuomba sana Mhe. Waziri afanye ziara za makusudi kwa baadhi ya maeneo katika vijiji vyetu mbali mbali vya Unguja na Pemba atembele na afanye kama upekuzi yaani uchanganuo ili aone kwamba kweli hili suala lipo au halipo.

Mhe. Spika, mimi hupenda sana kudadisi mambo ya magazeti na mambo mengine, unaweza kumpa mtu gazeti ukamwambia nisomee akakwambia sijui. Kwa hivyo inaonesha dhahiri kwamba bado watu wetu wako nyuma kutokana na shughuli hiyo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati yangu ya Maendeleao ya Wanawake na Ustwi wa Jamii na kwaniba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani walionichagua kuja katika Baraza hili naiyunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri au bajeti yake hii kwa asilimia mia moja na naomba wajumbe wenzangu waichangie ili wamsaidie Mhe. Waziri. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mhe. Moh'd Ali Salim: (Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali) Mhe. Spika**,** nakushukuru kwa ninipa nafasi hii wakati huu wa jioni wakati nyoyo zimetulia na sote tuko tayari kuichangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, ninamshukuru Allah kwa neema yake aliyotukirimu ya kuweza leo hii kuwapo hapa tukiwa wazima na tukiwa na uwezo wa kufanya shughuli hii muhimu kwa maendesho ya nchi yetu.

Baada ya kumshukuru Allah Mhe. Spika, natoa shukrani kwako kwa kuweza kufuata Kanuni ya Baraza hili ipasavyo ukaniruhusu kutoa maoni haya ya Kambi ya Upinzani juu ya Hotuba ya Waziri wa ELimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2010/2011. naomba Mhe. Spika, wewe na wajumbe wako wote watukufu wa Baraza hili mnivumilie mpaka nimalize kazi hii niliyokwishaianza.

Shukrani nyingine naomba zende kwa Kiongozi wangu wa Kambi ya Upinzani Mhe. Abubakar Khamis Bakary Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni kwa kutuongoza vizuri katika Kambi yetu ya Upinzani na kutupatia ushauri mwema ulioniwezesha leo hii kuwasilisha maelezo haya muhimu.

Mhe. Spika, sasa naomba niungane na wenzangu wengi waliotangulia kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mawazo yake mwanana na vitendo vyake vya kiungwana vilivyopelekea leo hii wajumbe wa Baraza lako hili tukawa ndugu wa toka nitoke. Na katika shukrani hizi naomba pia zimfikie Kiongozi mwadilifu na jasiri Katibu Mkuu wa CUF na Waziri Kiongozi Mstaafu Maalim Seif Sharif Hamad kwa kushirikiana na Mhe. Rais katika kuleta mwanga mpya wa matumaini ya kuishi kwa usalama na amani katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba na kuwanusuru wanawake na watoto kufikwa na matatizo na idhilali isiyo ya lazima.

Mhe. Spika**,** nikiingia sasa katika lile la maudhui ya Hotuba ya Mhe. Waziri napenda tu kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa kama kawaida yangu sitamfuata Mhe. Waziri kwenda Idara baada ya Idara hasa kwa kuwa muda wako ni mdogo sana. Hivyo basi nitaeleza yale ambayo Kambi ya Upinzani inayoyaona yana umuhimu zaidi kuliko mengine.

Mhe. Spika**,** naomba nianze maelezo haya kwa kuangalia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza naishukuru serikali kwa kuamua kwa makusudi kuwekeza katika elimu na hivyo wizara hii kutengewa asilimia angalau iliyononooka. Hata hivyo namuomba Mhe. Waziri atutegulie kitandawili kidogo tu. Katika hotuba yake ukurasa wa 67 kifungu cha 211

katueleza anaomba aidhinishiwe Tshs. 4,475,000,000/- kwa ajili ya miradi ya maendeleo na akaeleza uchambuzi wake uko katika Jadweli Nam. 47 .

Lakini katika jadweli hiyo iliyopo ukurasa wa 211 jumla ya fedha za miradi ya maendeleo ni 50,850,089,000/- . inaonekana anataka aidhinishiwe mchango wa Serikali tu jee ruzuku na mikopo haihitaji idhini? Au hizi hazimo katika Bajeti ya Serikali?.

Mhe. Spika, ni jambo la kupongezwa sana utekelezaji wa miradi ya Wizara, kwani hatua kubwa imepigwa. Lakini Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi kidogo katika utekelezaji huo wa miradi.

1. Mradi wa ukamilishaji wa Ujenzi wa Makao Makuu ya WEMA 2009/2010 ulitengewa Tshs. 150,000,000/- na kwa bahati njema zote zilipatikana. Hivyo tegemeo letu kuwa tayari ujenzi huo umekamilika. Lakushangaza na mwaka wa 2010/2011 mradi huu bado upo. Kambi ya Upinzani inauliza ukamilishaji huu huwa mara ngapi?

2. Mhe. Waziri kalifanya Baraza lako lisiweze kutathmini utekelezaji wa miradi kwa kukosa ufafanuzi wa kila kipengele cha mradi kwa mfano: mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima uliotengewa Tshs. 900,000,000/- za SMZ na Tshs. 31,510,000,000/- kutoka Benki ya Dunia na BADEA una miradi saba (7) ndani yake lakini kila mradi mmoja mdogo haukuainishiwa fedha zake ni kiasi gani ili katika kutathmini ikaonekana kama kweli kila mradi umetumia kiasi kilichopangwa. Hili lilielekezwa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza hili lakini bahati mbaya limepuuzwa. Jambo hili linaweza kusababisha Mhe. Waziri na watendaji wake wakagawa fedha hiyo watakavyo na Baraza likashindwa kuhoji chochote. Tunahitaji taarifa hiyo iliyokamili.

3. Katika miradi ya mwaka unaomalizika Mhe. Waziri katueleza asilimia ya fedha iliyotolewa na SMZ lakini ile ya wahisani hakuiwekea asilimia yake, jee kuna nini? Jee asilimia yake ni kubwa sana au ni ndogo sana.

Mhe. Spika**,** jambo lolote lile ikiwa linataka kutekelezwa lazima kwanza lipangwe ili utekelezaji uwe mzuri. Utoaji wa Elimu kwa wanafunzi nao unahitaji mipango inayoeleweka na inayotekelezeka.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri anajitahidi sana kwenda huku na kule kutafuta misaada ya kuendeleza Elimu nchini mwetu, kwa hili anastahili pongezi sana. Hata hivyo pamoja na juhudi yote anayochukua bado mambo hayajapata mwendo unaotarajiwa. Inaonekana matayarisho ni madogo kuliko mahitaji halisi.

Mhe. Spika, katika utoaji wa Elimu kuna mambo mengi yanayohitaji kupangwa kabla ya kuanza kutoa elimu stahili. Kwa mfano kunahitajika miundombinu, nguvu kazi iliyobobea na mazingira shawishi ya elimu. Hayo yote yanahitaji yapangwe wala yasiwe ya kushitukizia. Mambo yafuatayo ni baadhi ya yale yanayohitaji matayarisho ya mapema ili elimu ipatikane ipasavyo:-

Majengo

Mhe. Spika, majengo yanajumuisha madarasa ya kusomea, ofisi ya mwalimu Mkuu, ofisi ya/za walimu, jengo la Maabara, jengo la Maktaba, ghala na vyoo vya wanafunzi (wanawake na wanaume) na vya walimu halkadhalika. Mhe. Waziri kakiri kuwa madarasa yaliyoko hayatoshi na wanawaomba wananchi waendelee kujenga mengine. Sidhani kama kuna haja ya kuwaomba wananchi waendelee kujenga madarasa mengine wakati hivi sasa kuna madarasa takriban 500 yanayohitaji nguvu za serikali baada ya wananchi kukamilisha sehemu yao.

Lakini katika Bajeti ya 2010 /2011 kuna lengo la kukamilisha madarasa 180 tu kati ya hayo 500 yaliyopo. Kwa mwendo huu madarasa 500 yatahitaji miaka mitatu kukamilika. Katika kipindi hicho cha miaka mitatu cha kumaliza madarasa yaliyotayari hivi sasa wananchi wanaweza kujenga hata madarasa 1000 ambapo serikali itashindwa kuyamaliza na wananchi watahisi nguvu zao zimepotea bure na watavunjika moyo. Kama ingewezekana kuyakamilisha madarasa yote 500 yaliyotayari hivi sasa na yale ambayo ndani ya mwaka 2010/2011 yatakuwa tayari hapo pangekuwa na haja ya kuwaomba wananchi waendelee. Kambi ya Upinzani inaiomba serikali ifanye kila juhudi iwezavyo lakini yende sambamba na nguvu za wananchi katika ujenzi wa madarasa. Aidha wakati wananchi wakijenga madarasa na ofisi za walimu wakuu basi Serikali ilipaswa ijitutumue ijenge majengo mengine kama vile maabara na maktaba.

Mhe. Spika, ni jambo la kutia moyo sana kuwa wanafunzi wote walioandikishwa 2010/2011 wa darasa la kwanza wamepatiwa nafasi skuli. Nchi nyingi zinazotoa elimu kwa kupanga mwanzo hazijafikia hatua hii. Hata hivyo tunaomba Mhe, Waziri atujulishe wanafunzi hawa kawapatia nafasi katika madarasa yenye vikalio au kawapatia nafasi za kukaa darasani wakipinda vibyongo na kuchafua sare zao kila siku? Hilo ni moja lakini jengine

katika wanafunzi wote hao kuwapatia nafasi kila darasa lina wanafunzi wangapi? Jee hawamo katika yale madarasa yanayoitwa *"Giant Class*" ambayo hufundishwa na walimu watatu mpaka wanne wakati mmoja? Kama ni hivyo basi bado hawajapatiwa nafasi ila wamekwekwenezwa madarasani ili wapate nafasi. Elimu ina taratibu zake na zinapokiukwa athari ya elimu haipatikani ipasavyo na huambukia na wanafunzi wengi kuwa hawapati elimu stahiki na wengine hata kuichukia wakahiari kupara samaki kuliko kukaa darasani.

Vikalio

Mhe. Spika**,** vikalio ni miongoni mwa mambo muhimu yanayohitajika katika elimu. Hivi sasa skuli nyingi za serikali ama zina upungufu wa vikalio au hazina kabisa. Na katika miradi iliyoorodheshwa na wizara hakuna mradi wa vikalio. Jambo ambalo limetupa wasiwasi mkubwa. Kambi ya Upinzani inaona kuna haja ya kuwa na makisio ya vikalio vinavyohitajika hivi sasa na miaka mitano ijayo. Kisha kukawa na mradi maalum wa kuondoa tatizo hilo. Ikiwa wizara imejiandaa kwa hilo basi tunaomba ilijulishe Baraza hili ni mwaka gani taasisi zote za elimu zitakuwa na vikalio vya kutosha.

Vifaa vya Kufundushia na Kusome

Mhe. Spika, nyenzo nyengine muhimu ya kutolea elimu ni vifaa. Vifaa vinajumuisha :- mihutasari, vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, vitabu vya rejea na vielelezo vingine. Mhe. Spika, naipongeza wizara kwa matayarisho na ugawaji wa vitabu vya kiada vya sekondari na vya msingi. Hata hivyo kwa vile vya msingi itabidi vitayarishwe vipya ili vikidhi mahitaji ya Sera ya Elimu inayotumika sasa ya 2,6,4,2, badala ya ile ya 3,7,2,2,2, ambayo ikitumika zamani. Kwa upande wa vitabu vya Sekondari hofu kubwa ni ubadilishaji wa mihutasari unaofanywa huko Tanzania Bara bila ya mashauri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jambo hili litasababisha kubadilisha vitabu kila mihutasari inapobadilishwa. Hiyo ni hasara ambayo inahitaji kutafutiwa dawa.

Maktaba za Skuli

Mhe. Spika**,** tumeshaona yanayohusu vitabu vya kiada. Sasa kuna haja ya kuangalia vitabu vya ziada na vile vya rejea. Hivi sasa skuli nyingi hazina maktaba na kwa hivyo wanafunzi na walimu wanakosa vitabu vya ziada na vya rejea. Kuna wakati "*British council"* ilianzisha maktaba za skuli na kuzipatia vitabu vya Kiingereza kwa ajili ya kuendeleza lugha yao. Lakini baada ya wao kuondoka ni chache kati ya maktaba hizo zilizobaki. Na hatuoni juhudi za makusudi zinazofanywa katika jambo hili. Serikali imeshindwa kuweka maktaba kila skuli kwa sababu walifungua madarasa bila ya kupanga kunahitajika nini na nini. Kwa kuwa kinga haikuwezekana basi sasa itabidi

tutibu. Kuna haja ya Serikali kuandaa mpango wa makusudi wa kuwa na maktaba kila skuli tena zilizo na vitabu vinavyostahiki.

MAABARA

Mhe. Spika**,** kipindi kirefu sasa tuna malalamiko ya wanafunzi kukataa kusoma masomo ya sayansi na wengi wao kukimbilia masomo ya sanaa. Sidhani kama Wizara imefanya utafiti wakutosha na kugundua ni jambo gani linalofanya wanafunzi wachukie masomo hayo. Wanafunzi wengi wanadai kuwa masomo ya sayansi ni magumu. Lakini sababu kubwa inayowafanya wayaone magumu ni jinsi yanavyosomeshwa. Sayansi katika skuli nyingi inasomeshwa kama masomo ya sanaa kwa nadharia tu bila ya vitendo. Vitendo vya sayansi vilianzishwa katika juhudi za kupata ufumbuzi wa mambo mengi ambayo yakielezwa kwa nadharia na ukweli wake ulikuwa na mashaka. Hivyo basi sayansi ni lazima isomeshwe kwa vitendo ili ipendwe. Mwanafunzi anastarehe na anavutiwa sana na anafahamu kwa muda mrefu bila kusahau anapofanya jaribio la sayansi mwenyewe na akapata matokeo yake. Lakini hili katika skuli za serikali halipatikani kwa sababu hakuna Maabara au kama iko hapana vifaa vya maabara au hapana mwalimu anayeweza kuzitumia. Hivyo kuna haja yakuwa na Maabara zenye vifaa stahiki na walimu wanojua kuitumia.

Naomba hapa nimuulize Mhe. Waziri ni wafanyakazi wa Maabara wangapi walioajiriwa katika kipindi hiki cha miaka 5 iliyopita? Kama wapo wamepelekwa skuli gani? Hawa nao ni wafanyakazi muhimu kwani ndio wasaidizi wa walimu wa sayansi.

WALIMU

Mhe. Spika, baada ya kupata vitu vyote vilivyotangulia kuvitaja lazima wapatikane walimu ili elimu iweze kuhamishwa kutoka vitabuni na kupelekwa kwa wanafunzi. Walimu wanaohitajika ni walio na uwezo wa kuyajua masomo wanayofundisha na kujua jinsi ya kuyafundisha. Kutokana na Sera mpya ya Elimu somo la Kiingereza linatarajiwa kutumiwa kama lugha ya kufundishia kwa baadhi ya madarasa ya msingi ili watakapofika Sekondari wanafunzi waweze kuyaelewa masomo yao vizuri.

Hili ni jambo la kupongezwa sana. Wasiwasi uliopo katika utekelezaji huo ni jee hao walimu wa skuli za msingi wanao uwezo wa wao wenyewe kwanza kusema Kiingereza sahihi? Kwani kama uwezo huo hawana mpango mzima utafeli. Kutokana na uzoefu wangu ninajua kuwa walimu wengi hawawezi kuzungumza Kiingereza hata wao wenyewe licha yakuwa na uwezo wa kuwafundisha wengine kwa kutumia lugha hiyo. Wizara ina mpango gani wa

kuwawezesha walimu wote husika katika uwanja huo, hali tuukijua kuwa walimu hao ni wengi sana.

Mhe. Spika**,** hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa walimu katika skuli za Serikali. Kutokana na hali hiyo usomeshaji unakuwa mgumu, ingawaje kuna baadhi ya skuli walimu wanapigana vikumbo kwa wingi. Hali hii inaleta tafauti katika usomeshaji. Skuli nyingine zina tahafifu na nyingine zina mbano mkubwa. Ni jambo la busara kwa Wizara kufanya uchunguzi yakinifu wa kujua ugavi wa walimu ulivyo na isawazishe ili skuli ziwiane katika kubeba mzigo wa kufundisha. Uwiano huo usiwe wa idadi tu ya walimu bali hata uwezo wa kufundisha masomo wanayopangiwa.

Mhe. Spika, jambo jengine la kuzingatiwa ni maslahi ya walimu. Hivi karibuni Serikali imeanza kuwalipa walimu kwa kutumia muundo mpya (*scheme of Service).* Hili ni jambo la kupongezwa. Lakini shughuli nzima hii ya mishahara ya walimu imegubikwa na matatizo kadhaa. Inavyoelekea Wizara haina taarifa zakutosha kuhusu walimu wake. Kwani matatizo mengi yaliyojitokeza ni walimu kupunjwa kutokana na utangulizi kazini (*Seniority*) kama kungekuwa na taarifa za kutosha matatizo hayo yasingetokea yangeweza kuepukwa. Lakini pia bado kuna haja ya kuangalia zaidi. Walimu.

Mhe. Spika**,** kama nilivyotangulia kusema katika shughuli za elimu kunahitaji mipango ya kufaa. Kuwe na mipango ya muda mfupi na yale ya muda mrefu. Wizara ilikuwa ipange mahitaji ya walimu kwa angalau miaka mitano. Kutokana na mipango hiyo Wizara ingeelewa kila mwaka inahitaji kuajiri walimu wangapi wenye sifa gani na watapatikana wapi ili mpango huo ukaeleweka na Utumishi na Wizara ya Fedha kwa utekelezaji wa kila mwaka. Mpango huo ungeondoa usumbufu wa wahitimu wa ualimu kukaa nje ya kazi kwa muda mrefu bila kuajiriwa, hali ambayo huwapunguzia ari ya kazi na hata masomo waliyoyasoma. Hapa naomba Mhe. Waziri atuarifu walimu waliobaki ambao hawajaajiriwa atawaajiri lini ili apunguze upungufu na awaondolee na wao usumbufu.

Mhe. Spika, bado kiwango cha elimu yetu ni kidogo ukilinganisha na skuli nyingine huko Tanzania Bara. Kutokana na jinsi wanafunzi wetu wanavyopasi mitihani inaonesha wazi kuwa bado tuko nyuma. Mhe. Waziri katika kitabu chake katuonesha jinsi wanafunzi wa kidato cha 4 walivyofanikiwa tangu 2005 mpaka 2009, akabagua wasichana na wavulana (Jadweli Nam. 6 (b)(i) na 6 (b) (ii). Ukiangalia mwaka wa mwisho yaani 2009 tumeambiwa waliofaulu wote wavulana ni 80.7% na wasichana 81.3%. kwa kuchukulia kuwa kila aliyepata cheti amefaulu ni matokeo mazuri ya kujivunia. Lakini ukiangalia wangapi wenye uwezo wa kuendelea kidato cha 5 tutaona kuwa bado hali sio nzuri, kwani wavulana ni asilimia 18.17 (D1 – III) na Wasichana ni 14.146%.

matokeo haya yanafanya wastani wa asilimia 16.14 kwa wavulana na wasichana pamoja. Hii bado haijawa hali nzuri. Kwa kuzidi kuthibitisha ubaya wa matokeo yetu ni kuwa 2009 skuli 5 za mwisho ni kutoka Zanzibar na 2010 katika skuli 10 za mwisho 4 ni kutoka Zanzibar.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa sasa umefika wakati wa Elimu ya juu isiwe ni jambo la Muungano kwani sasa tayari tunavyo vyuo vikuu vyetu wenyewe. Lakini zaidi hata Baraza la Mitihani tuwe na letu wenyewe tusitegemee tena kufanya mitihani ya Tanzania Bara, uwezo tunao bado nia na utekelezaji tu.

Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ianzishe vyombo hivyo ili tujitegemee. Inawezekana tutimize wajibu wetu.

Mhe. Spika, mwaka jana nilizungumzia swali zima la michango ya skuli. Nilipendekeza mambo mawili ya msingi lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Naomba na leo nikumbushe mambo hayo. Moja ni kuwa michango ingetozwa kwa mujibu wa uwezo wa mzee na isiwe watu wote sawa. Lakini lapili ni kuwa kwa kuwa makusanyo ni makubwa kuna haja ya Wizara kuelewa makusanyo yote ni kiasi gani na ikaliarifu Baraza lako tukufu. Hivyo kama Mhe. Waziri anaijua ya mwaka huu tunaomba atuarifu.

Mhe. Spika, tumefurahishwa sana na ujenzi unaoendelea wa majengo ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) huko Tunguu. Tunaomba ujenzi huo wende salama na usisuesue kama ilivyokuwa huko mwanzo. Kwani ujenzi huo ukikamilika utafanya ungalau chuo hicho kianze kuwa na sura ya chuo halisi. Hata hivyo tunaomba ruzuku ya Bajeti ya Chuo iongezwe ili chuo kiweze kufanya shughuli zake ipasavyo.

Mhe. Spika**,** sasa niruhusu nikushukuru tena kwa kunivumilia nikaweza kumaliza hotuba hii ya maoni ya Kambi ya Upinzani. Ni mategemeo yetu kuwa kuna mambo mengi ya kufanyiwa kazi kwa maendeleo ya elimu na nchi kwa jumla. Aidha napenda nichukuwe nafasi hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkoani kwa mashirikiano makubwa waliyonipa kwa muda wote tangu wanichague mpaka hivi sasa. Naomba niwaombe radhi sana tena kwa kutokuchukua fomu ya kugombea mara hii. Hata hivyo, ninawaahidi nitakuwa nao bega kwa bega muda wote wa uhai wangu na nitatumia ujuzi nilionao kuwaelimisha wengine kila itakapohitajika.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema kuwa sasa hivi tuko wazima tunatekeleza majukumu yetu kama tulivyojipangia.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia jioni hii bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, pia nimshukuru Mhe. Waziri na nimpongeze kwa kuwasilisha kwa uzuri bajeti yake kwa mwanana na murua.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu nitaanza kuchangia katika ukurasa wa 30. Mhe. Spika, naanza katika elimu ya madarasa na vyuo vya qur-ani, katika hotuba yake Mhe. Waziri ameeleza kwamba vyuo vya qur-ani vimetembelewa na katika kutembelewa ilifanywa ziara ya kukutana na walimu na walimu hao walishajihishwa jinsi ya kutafuta njia mbadala ya kuwapatia adhabu nyengine ili kuondolewa ile adhabu ya bakora.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba bakora ndizo zinazochangia utoro wa vyuoni. Mimi naweza niko kinyume na suala hili, naweza kusema bakora si kweli hazichangii utoro. Nadhani kama hizi ziara zilizofanywa na wakakutana na walimu wakatoa maoni yao, mimi sifikiri kwamba maoni mengi yatatoka kuwa bakora ndizo zinazokimbiza utoro.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi tu yanayowafanya wanafunzi wakimbie vyuoni, ni mambo ambayo mengine yanachangiwa na wazee. Haya yanaweza kuwa ni maoni ya wazee kwa sababu mzee siku zote mtoto wake agombe mwenyewe, mtoto siku zote apigwe na mzee wake mwenyewe ukimpiga wewe ni kosa. Kwa hivyo, kuna mambo mengi yanayosababishwa na utoro vyuoni.

Mhe. Spika, jambo la kwanza unajua chuoni ni pahala pakufunzwa maadili mazuri na utoro unaanza wakati mtoto anapofikia umri wa kubaleghe pale ndio unaposhamiri utoro. Mhe. Spika, mtoto utamlea chuoni vizuri lakini akishakufika baleghe au akishakuwa mwanamwari pale ndio utoro unaanza kushamiri kwani huwa anaanza kuwekwa kitako na kufundishwa maadili mazuri. Anaanza kufundishwa heshima ya kivazi, pengine ameshashonewa nguo ambayo haitambulikani na mzazi wake, leo pale anakwenda kufundishwa jinsi ya mavazi yanayotakiwa, hapo mtoto anaona pale kila siku ni kuadhibiwa basi ndio anaanza kukimbia. Kwa hivyo, hapo ndio mtoto kama huyo ndio anaanza kutoroka chuoni.

Mhe. Spika, jambo la pili linalowafanya watoto watoroke chuoni ni tamaa. Kwa mfano kenda pahala kafanya biashara amepata shilingi mia tano, leo kapata shilingi elfu moja hizo ndio naweza kusema ni ajira za utotoni. Mhe. Spika, ajira za utotoni pia zinamfanya mwanafunzi akimbie chuoni.

Mhe. Spika, jengine linalosababisha mwanafunzi kukimbia chuoni ni suala la ada. Mhe. Spika, unajua skuli mara nyingi watoto wanatoleshwa ada, lakini mzazi yuko tayari auze kuku wake, ng'ombe wake lakini mtoto wake amlipie skuli. Mhe. Spika, kuhusu chuoni pengine kwa mwezi ni ada ya shilingi mia tano tu, basi ile mia tano kupeleka chuoni basi mzazi atamwambia mtoto wake mimi sina kaa kitako hapo. Hiyo shilingi mia tano naweza kusema labda vyuo vya mjini lakini kwa vyuo vyetu vya shamba mtoto kwa kila siku ya Alhamisi anapeleka shilingi 20 tu.

Mhe. Spika, pesa hiyo inatiwa kwenye kibubu inakuja kusaidia mfunguo sita kwenye maulidi, ikifika mfungo sita mwezi unaotolewa pesa ni huo kwa mtoto mdogo ni shilingi 1000 ili wafanye maulidi yao. Kwa hivyo, ni masuala ambayo yanachangia watoto kukimbia chuoni hasa ni hayo, na yako mambo mengine mengi yanayosababisha kukimbia chuoni.

Mhe. Spika, pia jambo jengine ni kwamba pengine mzazi anamuamsha mtoto wake asubuhi na mapema awahi skuli lakini mtoto huyo akisharudi skuli saa tisa anatakiwa aende chuoni basi atacheza huko nje, mzazi wake atamuuliza leo huendi chuoni, mtoto atajibu nakwenda hapo ndio imekwisha hiyo hakuna lile sisitizo kama la skuli.

Kwa hivyo, na hilo linachangiwa na wazee, lakini suala la bakora mimi siamini kwamba mtoto anakimbia kwa bakora kwa sababu hiyo bakora imo kwenye dini na imetajwa. Mhe. Spika, sisi tumesoma kwa bakora, mimi chuoni kwangu nilikuwa na mwalimu anaitwa Mwalimu Othmani maarufu tukimwitwa Jini maarufu, Mwenyezi Mungu amrahamu. Mhe. Spika, mwalimu huyo anakuja chuoni anakwambia leo Mtumwa simama nataka unisomee yasini yote, ukiikosa unachezea bakora na tumesoma hivyo hivyo. Mimi miaka kumi na mbili nimeshahitimu zamani akanikabidhi darsa hilo ulisomeshe.

Mhe. Spika, mimi nina imani sasa hivi tunataka tuwafanye watoto Mhe. Waziri wasisome kabisa. Kwa hivyo, mimi ningeliomba Mhe. Waziri ukae na wizara iwakusanye walimu hasa wa vyuoni ili waweze kutoa maoni yao kwa hili. Mhe. Spika, huo mswada unaotaka kuletwa wa bakora kwamba iondoshwe bakora mimi ndiye mmoja nitakayekimbia kwa sababu bakora ndio malezi.

Mhe. Spika, nikiendelea anasema kwamba kuna manung'uniko ya walimu wa vyuoni kuwa muda mwingi watoto hushughulikia mambo ya skuli, hili ni kweli. Mhe. Spika, manung'uniko haya yapo zamani nadhani hapa Baraza hili tuliwahi kuyasema kwamba muda mwingi wanafunzi wanachukuliwa na walimu wa skuli. Hivi sasa kuna skuli inaitwa Al-Haramayn, skuli hii iko Mombasa, skuli hii imewachukua watoto wengi imewakusanya watoto kila mwalimu anapita akauliza je, hujakumbwa na Al-Haramayn wewe.

Mhe. Spika, unakuta kuna gurupu kubwa la vyuoni watoto wamechukuliwa katika skuli hiyo kuanzia asubuhi mpaka saa kumi. Mhe. Spika, saa kumi mtoto akirudi skuli anakwenda chuoni saa ngapi, huyo kweli ndio anasoma chuoni. Kwa hivyo, sasa hivi vyuo vingi vimeteteruka watoto wengi wamechukuliwa na skuli hiyo. Mhe. Spika, isitoshe hizi skuli zetu palikuwa pana migogoro hapa siku nyingi, kwamba walimu siku ya Jumamosi na Jumapili ni siku ambayo mwanafunzi unahakikisha mwanafunzi huyu tayari nimpate mimi mwalimu wa chuoni kuanzia asubuhi mpaka muda wangu ninaomsomesha.

Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo Mhe. Waziri wakati hii wizara yako ni ya elimu na haishughulikii elimu moja, ilipotajwa Wizara ya Elimu ni kwamba haikubaguliwa ni elimu gani, ni elimu zote Mhe. Spika. Kwa hivyo, hata Mtume alisema kwamba tafuteni elimu mpaka Uchina, hapa haikutajwa elimu gani hapa. Kwa hivyo, elimu zote elimu ya dini na elimu ya dunia. Mhe. Spika, hii wizara ina jukumu ya kushughulikia elimu zote.

Mhe. Spika, huko kwa wenzetu Sudan wana siku maalum wameweka miezi mitatu wenyewe wanaita siku za Halwa. Siku hizo zinafungwa skuli wanachukuliwa watoto, walimu wa vyuoni wanawaweka watoto wao wanakwenda kuwanywesha qur-ani. Hata wakimaliza miezi mitatu wanaambiwa haya nyinyi kazi yenu kudurusu tu hiyo qur-ani. Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo Mhe. Spika, na elimu ya dini ipo haja ya kuishughulikia.

Mhe. Spika, nikiacha hapo nije katika mafao ya walimu. Suala la mafao ya walimu nalo ipo haja kutizamwa lizidi kuangaliwa, lizidi kutizamwa kwani siku zote mimi husema kwamba mwalimu na daktari ikiwa hukumtukuza basi hanasihiki. Kwa hivyo, mimi ningeliomba kwa kazi kubwa wanayoipata walimu hivyo tuzidi kuwashughulikia mafao yao. Kwa kweli ipo haja ya kuyashughulikia mafao yao ili wale walimu ambao wanaotoroka hapa wakenda kutafuta maslahi sehemu nyengine basi wabakie hapa watusomeshee watoto wetu. Mhe. Spika, kuna hatari kubwa za wizara zetu mbili hizi kama Wizara ya Afya wanavyotutoroka wataalamu na Wizara ya Elimu wanatukimbia walimu.

Mhe. Spika, kuna suala zima la *bus fare* kuna walimu wanaosemesha sehemu za mbali muda mwingi utawakuta wanaranda mabarabarani. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hiki kinachotolewa kwa kweli hakidhi haja wala hakiwatoshi kusema ukweli, na ikiwa watakipata hakitoshi au pengine hawapati kabisa. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri suala hili la walimu aliangalie vizuri.

Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri angalau angewatizama walimu katika sehemu za warsha, semina na wao wapatiwe nafasi hizi ili wajione kama na wao ni sehemu ya wafanyakazi kama wafanyakazi wengine.

Mhe. Spika, pia kuna suala zima la Bodi ya Mikopo. Mhe. Spika, kuna malalamiko ya bodi hii kwamba hiki kinachotolewa hakikidhi haja. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri hili alifuatilie na afanye utafiti iende na wakati leo mtu unamtoa hapa anakwenda kusoma Mzumbe anakaa huko na wala anachokipata hakikidhi haja. Hata hivyo, kinapotolewa huwa kinatolewa kwa muda mrefu, pengine huko nyuma ameshakopa hata anapokipata anakwenda kulipa tu. Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Waziri hili alishughulikie.

Mhe. Spika, jengine nije katika sehemu ya magofu, kuna suala moja ningelimuomba Mhe. Waziri gofu la kwa Bihole kamati yetu mwaka jana tuliwahi kwenda kutembelea. Mhe. Spika, huko kuna tuhuma kwamba kuna sehemu ya gofu la Bihole limeuzwa. Kwa hivyo, ningeliomba suala hili lifuatiliwe kwa makini na tulipokwenda hii kamati inayoshughulikia ni kamati yenye utatanishi Mhe. Ame Mati ilipokuwa inatajwa alishtuka akasema mbona hii kamati iko katika familia moja.

Kwa hivyo, hatima yake ni kwamba kuna tuhuma imekatwa sehemu imeuzwa na baadhi ya wenye kamati wanalalamika sana kwani hivi sasa kumekuwa kuna zogo sana. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri suala hili liende likafanyiwe utafiti ili lishughulikiwe kama kuna hatua zichukuliwe.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru na namuombea Mhe. Waziri wakati ametangaza nia ya kugombea Urais na wale wote waliotangaza basi Mwenyezi Mungu awarejeshe. Ahsante nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo kuwa mtu wa pili kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hii ni moja katika barka ambayo kama tunavyojua huu ni wakati wa waheshimiwa wetu kuchukua fomu za kugombea Urais. Mhe. Spika, nashukuru na mimi nimekuwa mtu wa pili katika bajeti yake kumchangia.

Mhe. Spika, hivi sasa dunia nzima ina mageuzi ya mambo mengi tu, moja ikiwemo masuala ya uchumi, mambo ya elimu na mambo mengine. Lakini tusishangae katika nchi yetu ya Zanzibar nayo ikaingia katika duru hilo la kugeuka. Mhe. Spika, hakuna anayejua Marekani kama kutakuwa na Rais wa Kiafrika, lakini na sisi Zanzibar Mwenyezi Mungu akitujaalia Mhe. Waziri wa Elimu ampe lile jambo ambalo analiomba kwa njia ya kheri kwa kutaka kutuongoza sisi waja wake katika mambo ya kutuletea maendeleo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu wake, Naibu Katibu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wake wote nao nawapongeza sana kutokana na jitihada zao za kusimamia fedha za miradi hakuna ile hali ya ubadhirifu. Hii

ni sifa moja kubwa sana kwa hiyo tunawapelekea pongezi hizo kwa sababu duniani sasa hivi utasikia leo kuna ubadhirifu wa pesa, lakini katika wizara hii mpaka hivi sasa tunaingia kwenye bajeti ya mwisho bado hatujasikia ubadhirifu wa fedha za miradi.

Mhe. Spika, kutokana na kitabu hiki kina mambo mengi haya yote amesimamia Mhe. Waziri mwenyewe na amehangaika huko nje kutafuta fedha za wahisani na kwa bahati nzuri amekwenda nchi mbali mbali kwenda kutafuta misaada. Mhe. Spika, sasa hivi Vyuo Vikuu hapa kwetu vinajengwa kama uyoga, hii ni moja katika ishara kubwa sana ya Mhe. Waziri tunavyoziona jitihada zake na kuitakia Zanzibar kupata elimu ya vyuo vikuu.

Mhe. Spika, ukweli haufichiki kila jambo linajionesha, tumeanzia kwenye vitabu na sasa tunakwenda kwenye majengo, ukizunguka unaambiwa Mhe. Waziri vitu vyake hivi ameviweka. Mhe. Spika, kwa kweli anayesifiwa hupewa tunza kwa hiyo kutokana na jitihada zake Mhe. Waziri ni lazima na yeye tumtunze. Kwanza tuikubali hotuba yake mia kwa mia na pili Mwenyezi Mungu atambariki.

Mhe. Spika, kuhusu hali ya maendeleo ndio kama nilivyosema kuwa simsifu mtu burebure namsifu kwa vitendo. Mhe. Spika, hapa hali inatuonesha kwamba hali ya maendeleo ya elimu kwa kipindi cha miaka hii ameonesha hali nzuri sana. Ni kweli hili tukubaliane nalo kwa sababu ameyafanya mambo kwa kipindi kifupi sana alichokuwepo yeye. Mhe. Spika, huko nyuma tulikuwa na historia walikuwepo na wengine na wao wamefanya kiasi cha kufanya lakini hata hivyo haikufikia *level* kubwa kuliko mwenyewe Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Sera na Mipango hapa kidogo namuomba Mhe. Waziri aje kunipa maelekezo kwa sababu kuna kipindi fulani kulikuwa na ile miradi ya Skuli za Wilaya za Sekondari. Lakini kwa bahati nzuri sisi Wilaya ya Kaskazini ‘B’ tuliambiwa Kinduni na wao tutapata lakini kwa bahati mbaya au sijui ni bahati nzuri tunasikia kuwa lengo lile limepotea kabisa limeelekea katika eneo jengine. Kwa hivyo, hapa ningemuomba Mhe. Waziri aje kunipa maneno mazuri sana ili na mimi anifurahishe kama ninavyompigia debe.

Mhe. Spika, sasa nije katika ujenzi wa maskuli, hapa kuna kijifungu kidogo katika huu mradi wa uimarishaji wa elimu ya maandalizi. Kidogo naomba anisaidie hapa labda masuala ya komputa kama tunavyosema siku zote zinapata *virus* na zikarusha baadhi ya mambo. Hapa kuna ujenzi wa skuli mbili mpya za maandalizi unaendelea huko Potoa na Wilaya ya Kaskazini ‘B’. Mhe. Spika, huwa najiuliza Kaskazini ‘B’ ni sehemu gani. Ndio hiyo Kinduni au ni sehemu gani hapa kidogo inanichanganya.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hapa aje kunifahamishe kwani kwenye redio huwa tunasikia kwamba hili suala limeshaondoshwa katika kijiji cha Kinduni imepelekwa sehemu za Donge. Hapa kidogo naona hili sijalifahamu vizuri Mhe. Waziri hapa aje kunifafanulia vizuri kipengele hiki amekusudia vipi ili na mimi niweze kuchangia vizuri.

Mhe. Spika, sasa niingie katika ukurasa wa 17 kuhusu mambo ya kale. Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Kitope kuna sehemu nyingi za magofu, lakini nimeangalia katika kitabu hiki hakuna masuala hayo. Kwa mfano, kuna magofu sehemu ya Kiombamvua ndani kuna kijisehemu kama kisiwa huko kuna magofu ya kale tena ni mazuri. Lakini nikiangalia katika mpangilio mzuri wa Mhe. Waziri amenisahau. Kwa hivyo, namkumbusha binadamu pengine hajalisikia na wala hajalionapo. Mimi kwa kuwa eneo lile nalijua ndio namwambia kwamba kuna kisiwa kizuri na kuna gofu zuri sana tena ni la historia.

Mhe. Spika, pia isitoshe kuna mapango mazuri tu katika Jimbo la Kitope tena ya historia, kuna pango kubwa sana ambalo lina maajabu kabisa, nalo hilo liko mkabala na Skuli ya Upenja pale. Pale lipo bango lakini sidhani kama bango lile Mhe. Waziri ni katika mpangilio wewe. Kwa hivyo, ninakuomba Mhe. Waziri ili uweze kwenda kuniingiza kwenye mipango hiyo na kuweza kujijua wananchi wa Upenja kwamba na wao wamepata mradi wa mambo ya kale.

Mhe. Spika, pengine hapo pana mambo mengi wanafaidika, pengine pale panaweza pakatokeza ajira, vijana watapata kusomeshwa historia ya pango lile ili waweze kujua limekuja vipi. Kwa hivyo, hapo mambo mengi wanaweza wakayapata vijana hivyo namuomba Mhe. Waziri hili nalo alitafutie njia ya kuweza kuliingiza humo katika miradi yako ili kupata kunufaika wananchi wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea kuchangia bajeti hii nije kwenye uimarishaji wa skuli za msingi. Mhe. Spika, katika Jimbo la Kitope tuna skuli nyingi sana za maandalizi, nazo hizi kuna nyengine nafikiria Mhe. Waziri hazijapata kusajiliwa. Kwa hivyo, ninakuomba Mhe. Waziri skuli hizi zifanyiwe *registration* halafu na hao walimu wapate taaluma ili wapate kuwaelimisha watoto vizuri. Mhe. Spika, hizo ni jitihada zao wenyewe kutaka watoto wao waendelee basi wazazi wanajielimisha wao wenyewe.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri kwa makusudi kabisa hawa walimu ambao waliojitolea katika Skuli ya Jimbo la Kitope wachukuliwe na wao waelimishwe. Mhe. Spika, sisemi kwamba wapate ajira ghafla kwa sababu pengine taaluma hawana, lakini utakapowasomesha na wakapata elimu nzuri

basi naamini na wewe utaweza kuwaajiri ili wapate kuwaelimisha watoto wetu vizuri.

Mhe. Spika, mimi nikushukuru sana kutokana na ajira ya walimu, Wilaya ya Kaskazini tumepata ajira lakini bado nataka nikwambie ajira hiyo haijatutosheleza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwa kweli amejitahidi sana tunakushukuru sana watu wa Kaskazini, lakini bado hususan katika Jimbo la Kitope kwa sababu umetuelimisha jinsi ya kujenga skuli. Mhe. Spika, nimesema kuwa namsifu mtu kutokana na utendaji wake na umahiri wake na ujasiri wake. Skuli ya Kitope Mhe. Waziri ametusaidia sana hususan katika majengo.

Kwanza yale majengo yako katika hali nzuri na pili sasa hivi tumepata hamasa nzuri anasema kuwa anzeni mimi nitamaliza, hiyo ndio sera ambayo tumeikamata. Sasa hivi kuna skuli nyingi Kitope tumejenga na ametusaidia baadhi ya mabanda lakini kuna banda sasa hivi halijatiwa paa hivyo tunakuomba Mhe. Waziri utusaidie.

Mhe. Spika, nikwambie Mhe. Naibu wake ameshikwa alipokuja siku ya sherehe zetu za kutoa misaada alisomewa risala pale yeye mwenyewe alisisimkwa na mwili kutokana na ile hamasa ya kuwa tunajitahidi na alitamka wazi wazi kwamba tutasaidia. Mimi nimefurahi sana kauli ile lakini najua kauli ile imetokana na wewe Mhe. Waziri amejinasibu kwa sababu anajua wazi mnafanya kazi kwa pamoja. Sasa nina imani hiyo kubwa kuwa Mhe. Waziri utatusaidia kutokana na kauli ya Mhe. Naibu Waziri wako ili sipotee tukaona labda yuyle ametuhadithia tu hivi hivi bila ya mafanikio yoyote. Lakini Mhe. Waziri hilo ndio suala tunalokwambia.

Tunakwambia Mhe. Waziri bado walimu skuli zetu za majimboni hazijatosheleza. Tunakuomba tena uendelee kuwasaidia walimu kutufanyia ajira ili kuweza kupata na wao ndugu zetu kuweza kusomesha vizuri kwa wakati. Kwa sababu kuna wengine wanakaa mjini, lakini wakifika kule kipindi cha kwanza hawakipati, lakini tunataka sasa hivi ajiri walimu wetu wawe karibu na lile eneo lenyewe. Hilo ndilo tunalolipigia kelele sana utusaidie.

Halafu Mheshimiwa mwenzangu alisema suala la mishahara. Mhe. Waziri mimi ninavyokujua wewe hodari, utalisaidia sana suala hili la mishahara kwa sababu kuna walimu wengi na walimu ndio wana-*mass*, walimu wanaweza kuzungumza. Kwa sababu unapomsaidia mwalimu anapoona jinsi gani mshahara wake unavyotekelezwa kwa wakati, wanapata pesa zao za nauli kwa wakati na wale waliokuwa hawajapata kipindi cha nyuma warekebishiwe waweze kupata Basi mimi sidhani kama wewe watakuangusha, hawakuangushi

hata siku moja Watakuwa ni vielelezo vya skuli. Baada ya kumaliza skuli watazungumza na wewe kwa nia nzuri.

Sasa hilo nalo nione kuwa marekebisho ya mishahara Mhe. Waziri uyape kipaumbele ili na wao wakuombee dua. Kuna wengine masharifu, wengine Mwenyezi Mungu kawajaalia midogo yao mizuri kawabariki, Mwenyezi Mungu atakujalia manufaa.

Mhe. Spika, katika ukingo wangu wa kumalizia nimwambie Mhe. Waziri kwamba kweli umesema masuala ya upigaji katika madrasa kwa wanafunzi. Mimi nakubaliana na wewe kuondoshwa kupigwa. Kwa sababu kuna walimu wengine wanafanya chusha kwa makusudi, nalo tulitizame hili, wanapigwa vibaya vibaya na tunasema jambo kwa kumbukumbu.

Kuna mwanangu mimi ameshapigwa amewiva na kupasuka. Lakini nilipofika sikumkemea mwalimu wana sikwenda kumshitaki, nimenyamaza kimya, walioona vijana 'nimeminya tu', lakini naugulia ndani ya roho kumuona mwanangu kawiva kabisa. Sasa upigaji mwengine unakuwa *too much* jamani. Hili suala tukubaliane nalo, kupiga si kulea hili mimi nasema. Kwa sababu tumelelewa sana na wazee wetu sisi.

Mzee wangu mimi alinipiga hatimaye namuonesha ununda usione leo nimetulia. Ndio ilivyo tuseme ukweli, mwisho anakutizama tu. Lakini Mwenyezi Mungu humuongoa yule mja iko siku akaa akatulia akasema ah! kumbe mimi nilikuwa najipigisha bure kwa mzazi wangu kumbe nikitulia nitakuwa mtu bora? Nayo imo kwa sababu mtoto naye kila siku umpige Mhe. Spika, hayo yatakuwa si masomo si kweli bwana, anakimbia anakuwa nunda yule mtoto. Lakini ukiwa na maelezo mazuri ya faraja kabisa mwanafunzi atatulia bila ya kutumia bakora.

Mhe. Spika, hili mimi nakubaliana nalo mia kwa mia, kuwa liondoke naunga mkono. Kwa sababu hili linatayarisha watoto kuwa sugu maana yake unampiga wee, kupasuka kwake anaingia usugu, sasa ndio yale yale akija pale mwalimu wewe unampiga anakucheka, atakucheka tu. Mimi nilikuwa nikiwacheka walimu, wananipiga na huvaa nguo tano tano bila ya kunijua. Wananipiga mimi najidai kukenya tu, najifanya naumia kumbe ndani nina suruali tano nikisha namcheka. Sasa imesaidia nini? Sio lengo, lakini hilo ni suala ambalo nakubaliana na Mhe. Waziri liondoke mia kwa mia.

Mhe. Spika, kuna madrasa zetu hizi, kwa mfano tuna madrasa nzuri ya Fujoni tena nzuri sana. Juzi nilikwenda nikaizindua imetimiza muda wa mwaka mmoja. Lakini imeelimisha vizuri sana, ina matatizo kidogo tu pale, tayari tumeshasaidia *foundation* hivyo, ninakuomba Mhe. Waziri na hili

tunakukabidhi utusaidie kutununulia. Iko nzuri sana pale Fujoni Nyumba ya Ndege, inaelimisha vizuri sana.

Mhe. Spika, baada ya hayo yote la kwanza kama ulivyosema nafasi yangu iliyobakia, basi namtakia heri na baraka *Inshaallah*. Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa lile analolitaka Mwenyezi Mungu ampe lenye kheri na yeye. Kwa kumalizia watu wa Jimbo la Kitope tutamshangilia na mimi akiniita siku ya kurudisha fomu nitakuwanaye pamoja bega kwa bega. Kwa hayo machache Mhe. Spika, Jimbo la Kitope tunaunga mkono hotuba kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kwa jioni hii ya leo kuzungumza machache kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza namshukuru Allah kwa kutuweka hai na uzima na tukapata taufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, tuko karibu na ukingo wa kumaliza Baraza, kwanza napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wetu wawili wakuu katika sehemu hii ya Zanzibar, Mhe. Rais wa Zanzibar (Dr. Amani Abeid Karume) na Maalim Seif Sharif Hamad kwa makusudi kuibadilisha taswira ya Zanzibar kutokana na hali ya mivutano, migongano na kuileta katika hali ya maelewano na maridhiano.

Nawaomba wagombea wote ambao karibuni wamejitangaza nia yao akiwemo Mheshimiwa wetu huyu kama alivyotaja katika hotuba yake, basi aiendeleze hii hali na ashawishi wengine kuiendeleza hii hali ili Zanzibar ijikwamue kutokana na pale ilipo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi nilifikiria kwamba, moja katika sababu kubwa ambayo Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amechukua nafasi hii ni kuona kwamba mambo yamekwama. Kwa hivyo, aweze kupata fursa hii ili kutukwamua. Naomba niseme kwamba, namtakia heri katika safari yake na pamoja na vikwazo vyote ambavyo vipo.

Mhe. Spika, mimi nilizungumza katika Bajeti Kuu ya Serikali kwamba fedha zinazotengewa mawizara hata ukazikokotoa kwa asilimia haileti maana. Kwa sababu fedha zenyewe ni ndogo sana kulingana na hali halisi ya wizara. Kwa hivyo, sioni haja kubwa ya kusema kwamba Wizara ya Elimu kutokana na umuhimu wake imepewa fungu kubwa.

Lakini naamini kwamba fungu hili bado ni dogo sana kutokana na mahitaji halisi ya wizara ilivyo sasa hivi. Tunachangamoto nyingi ambazo tungeliweza

kuzikabili katika kipindi kijacho katika wizara hii pamoja na bajeti ndogo ambayo inatolewa.

Pamoja na kwamba ni kubwa yao katika mawizara, lakini tatizo liliopo sasa hivi Wizara ya Elimu ni kwamba tumechukua na elimu ya vyuo vikuu. Hii ni elimu ambayo inavuta pesa nyingi sana, tusipojiangalia tunaweza kuua huku kwenye msingi na tukashughulikia vyuo vikuu. Lakini ukishughulikia vyuo vikuu ukaacha msingi ni sawa sawa na mti mzuri uliochanua na majani mazuri, matawi yanapepea halafu ukaanza kuutoa magome huku chini. Kwa muda mdogo utaona yale matawi yanapepea lakini kwa muda mti ule utanyauka na halafu matawi yataanguka.

Kwa hivyo, mimi nasema kwamba, pamoja na kuwa tumeingia katika elimu za vyuo vikuu, lakini kuna haja ya makusudi ya kuona kwamba elimu ya msingi inatizamwa kwa uangalifu sana. Kwa sababu hii ndio inayozalisha hivyo vyuo vikuu vya baadaye. Lakini kama tutaangalia vyuo vikuu na *focus* yake, kwa sababu vyuo vikuu vinatumia fedha nyingi sana katika fedha za Wizara ya Elimu. Ni dhahiri kwa sababu walimu wake pamoja na kuwa wachache lakini wanapewa fedha nyingi na wanahitaji mambo mengi na ni mazito sana. Kwa hivyo, tuangalie kwa kina kabisa. Vile vile tuitake serikali itafute vyanzo vyengine vya mbadala vya mapato ili tuweze kuweka mkazo mkubwa sasa hivi katika elimu.

Mhe. Spika, kitu kidogo ambacho Mhe. Waziri anatukosesha uhondo katika bajeti yake ni kwamba hatufafanulii ule mgao anaoupeleka vipi katika elimu tafauti. Kwa hivyo, nashindwa kuweza kujua kwamba mwaka huu ni wapi palipoongezwa au wapi palipopunguzwa. Sasa labda inafanyika kutupunguzia huu uwezo wa kujadili bajeti yake, lakini pamoja na uwezo wa kutoa mawazo.

Kwa mfano, Mhe. Spika, sasa hivi kuna mwelekeo katika ulimwengu wa kuona kwamba hizi wizara za kutoa huduma kama Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wanaangalia *per capital post* ya mtu ambaye wanamhudumia. Ukiangalia hivyo au *unit cost* unaweza ukajua kwamba kutokana na matatizo yaliyojitokeza, kwa mfano wanafunzi wengi wamefeli katika elimu ya sekondari mwaka huu.

Kwa hivyo, tungeweza kuangalia je, fedha haikuwa na athari yoyote katika *failure* ile iliyotokezea. Tunaomba sana Mhe. Waziri ikiwa utapata fursa katika nafasi yako hii ya kuja kutoa mchanganuo angalau utupe kwa *brief* kabisa elimu ya msingi imepewa ngapi na elimu ya sekondari imepewa ngapi. Lakini kwa waziri wako atakayefuata ukiwa wewe ni Rais, waelezwe basi kwamba waheshimiwa wanataka hivi katika Baraza lijalo.

Mhe. Spika, bajeti inatakiwa ielezee zile changamoto ambazo zipo na wanahitaji kitu gani katika kupambana na changamoto hizo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, moja katika mambo ambayo mimi nimeyakusanya kama matano hapa yanayokabili Wizara ya Elimu sasa hivi, ambayo ni changamoto kubwa. Kwanza ni maslahi ya walimu. Zanzibar yenyewe inasifikana kuwa mishahara midogo, kwa hivyo, mishahara hii midogo imeenea katika kila wizara. Sasa hivi ni tatizo kubwa kwa sababu kuna soko huria la Tanzania au soko huria tunaingia la Afrika Mashariki, hili litakuwa ni tatizo kubwa hasa kwa wataalamu wetu ambao wanamaliza katika vyuo vikuu mbali mbali na hasa wale wanaochukua pengine masomo mpaka ya *post graduate* na kuendelea. Kwa hivyo, tungeliangalia suala hili katika kina chake.

Lakini pia tuangalie katika ngazi mbali mbali namna gani walimu wanapandishwa daraja. Hili suala la *promotion* katika walimu ni suala muhimu sana. kwa sababu utakuja baada ya miaka kumi utamuhesabu mwalimu kwamba ile miaka yake tu, sasa hakuna *grade* fulani ya walimu ambao kutokana na kazi zao huyu kapanda *grade*, huyu kapanda *grade* hii, sasa hili lingesaidia hata wakati wa kubadilisha mafao ya walimu hakuna tena haja ya kumtafuta kafika miaka mingapi, katumia miaka mingapi, anajulikana tu, yeye ni mwalimu *grade* gani basi anajulikana mafao yake.

Halafu Mhe. Spika, changamoto nyengine iliyopo ni upatikanaji wa vikalio katika skuli zetu. Kwa kweli hili ni changamoto kubwa, kwa sababu moja katika sera ya Wizara ya Elimu ile mpya ni kutoa mazingira mazuri ya *learning situation* au usomaji. Mwanzo ni wale walimu, tukisema *learning situation* ina maana ni wale walimu halafu huku unakuja kwa wanafunzi, wanakaa pahala pazuri, masafa yao wanayokwenda, fursa wanazozipata ni sawa sawa na hivyo. Kwa hiyo, suala la vikalio kwa kweli lisitazamwe katika *angle* moja tu.

Jambo la kusikitisha ni kwamba unapopeleka vikalio kidogo na kwa muda mrefu inakuwa huwezi kufikia lengo. Kwa sababu vile kidogo ulivyopeleka na kwa muda mrefu vyengine havijafika ukienda ukipeleka tena vile vimeshavunjwa unaanza pale pale. Sasa ni muhimu kuiandaa hiyo *situation*.

Sisi hapa hupewa ripoti kwamba kuna Mifuko ya serikali ya dharura, sijamsikia Mhe. Waziri hata siku moja kuomba Mfuko ule akasema wanafunzi wetu wanakaa katika hali ngumu kwa hivyo tunaomba ule Mfuko wa serikali utusaidie. Lakini pia kuna wafadhili wengi. Siku moja nilimuuliza swali hapa tulimpoteza vipi sisi *OPEC*? Wakati *OPEC* alikuwa tayari anatusaidia? Na mpaka sasa hivi bidhaa iliyuodumu duniani ni mafuta, sasa sisi tulimpoteza vipi yule *OPEC*?

Mhe. Spika, hilo ni changamoto ambayo wizara inayo na ingelikuwa wali-*address* ni mwaka gani, basi kama alivyosema Mhe. Mohamed Ali Salim (Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali) ni mwaka gani ambapo Zanzibar itajikuta wanafunzi wake wanakaa juu ya viti na hawagaragari katika *floor* za madarasa.

Mhe. Spika, hakuna mtu asiyejua kwamba skuli za sekondari zina upungufu mkubwa wa walimu. Na saa nyengine utasema sio upungufu ni ukosefu hasa, hawapo. Sasa Mhe. Waziri hajatueleza katika hotuba yake ni vipi ame-panga kupambana na suala hili. Pamoja na kwamba walimu wanasomeshwa katika vyuo vikuu vyetu. Lakini inaelekea walimu wa sayansi ni haba na maendeleo yao pia yana wasi wasi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ni changamoto kwa Wizara ya Elimu si kujidanganya ni kufanya tathmini ya matokeo ya mitihani yanavyokwenda. Si suala la kukaa kitako ukasema hivi na hivi, shuka, kaa. Mhe. Waziri angekaa na wataalamu wake wakamwambia *a to z* kitu gani kinachosababisha matokeo yetu yawe mabovu kiasi hiki. Kweli Zanzibar hakuna uwezo wa watu kusoma kwa kiwango hiki?

Nakumbuka sisi tulipokuwa tukisoma *Form V* na *VI* tulikuwa na walimu wanne kutoka India. Sasa ikiwa tuna upungufu wa walimu kwa kiwango hicho hasa katika *'A' Level.T*unashindwaje kupata walimu kutoka sehemu nyengine? Au sasa uhusiano ule haupo tena? Mhe. Waziri hapa mgombea mtarajiwa, alitueleza kwamba kasafiri nchi nyingi, basi katika ncho zote hizo alizokwenda hakuwahi ku-*snatch* walimu wawili watatu akawaleta katika skuli zetu na wao wakaweza kusaidia? Kidogo tungelipata ufafanuzi kwamba, hatuna tena uwezo hata wa kupata walimu wakaliokoa hili jahazi?

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu Elimu ya Ufundi. Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nikichangia kuhusu Idara ya Utumishi Serikalini niliwaeleza kwamba, kitabu chao walichokujanacho wanafunzi wote walioko nje waliowaandika mule kwa fani zao, hakuna anayesoma elimu ya ufundi. Lakini kilikuwa na kasoro kwa sababu hawakutueleza ndani humu, najua Zanzibar hakuna chuo kikuu kinachosomeshwa ufundi, vyuo vyote sasa hivi ni *science*, *art* na mambo ya *bussiness administration* na mengineyo.

Kwa kweli Chuo Kikuu cha Mbweni bado hakijawa. Hebu tueleze Mhe. Waziri, kuna mpango gani na mkakati wa makusudi wa Zanzibar kutilia mkazo elimu ya ufundi? Mimi naona kwa Zanzibar kwa sababu ni nchi ndogo na kwa sababu vijana wetu wanao uwezo. Elimu inayoweza kutusaidia sisi ni elimu ya ufundi kabisa kabisa. Ukienda ulimwengu wote uliza, lakini kwa Zanzibar elimu inayoweza kutusaidia ni elimu ya ufundi.

Pia tulikuwa na mchepuo wa uvuvi. Je, Wizara ya Elimu imechukua jukumu gani la kuona kwamba baadhi ya vijana wanaomaliza *Form VI* wanakuwa *channeled* kwenda kusoma mambo ya *fisheries*.

Kwa sababu sasa hivi tuna suala zima la uvuvi wa bahari kuu, hatuna wataalamu. Sasa tukisema tusome *bussiness administration*, tusome *laws*, kuna muda tuta *saturate* soko upesi sana kiasi cha kwamba hatutakuwa na uwezo wa kuwaajiri. Lakini tukisomesha katika fani za ufundi uajiri utakuwa ni rahisi na wataweza kuleta *income* katika nchi. Kwa sababu tukiwa na ma *engineer* tutawatoa *expert* hapa.

Kwa hivyo, mimi naomba kwamba, pamoja na mambo yote yaliyoko katika Wizara ya Elimu, lakini elimu ya ufundi inastahiki kupewa nafasi inayofaa.

Mwisho Mhe. Spika, kwa sababu ya muda wako nizungumzie kuhusu suala la majenzi ya skuli. Kwa kweli kuna haja ya ku *rehabilitate*Wizara ya Elimu, kwamba iwe kweli sasa ina kitengo cha ujenzi kilichokuwa kinashughulikia kweli majenzi, lakini sio kilivyo sasa hivi. Haiwezekani, namna wanavyoachiwa walimu kujenga majengo hayajulikani yatachukua muda gani. Kwa hivyo, haiwezekani namna hiyo, lazima kifanye ukarabati mkubwa wa hicho kitengo cha shughuli za ujenzi, wao ndio waweze kuishauri wizara namna gani ya kushughulikia badili ya wizara ipate maombi wao ndio waseme wenye wizara.

Mhe. Spika, Ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Haji Mkema Haji: *Bismillahi Rahmani Rahiim.* Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuunga mkono hoja. Kwa sababu mimi nimekuja kuunga mkono tu hii hoja. Kwa hivyo, hii hotuba aliyoisoma Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani mimi naikubali.

La pili naridhika na kazi walizozifanya ambazo nazijua mimi na walizoziandika humu. Hizi ni kazi sahihi walizozitekeleza na mimi nakiri zimefanywa kwa uhakika. Namshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa ufupi na watendaji wote wa Wizara ya Elimu.

Mhe. Spika, nawapongeza watendaji hawa kwa sababu wamefanya kazi kilillahi katika mazingira magumu. Lakini lengo la wizara na serikali limepatikana, sasa kipimo kila mtu ana chake, lakini mimi nasema mafanikio makubwa tumeyapata katika Wizara ya Elimu. Lazima tujisifu, kwanza kiwango cha elimu kimekua. Mwanafunzi anayemaliza *Form VI* hapa Zanzibar au *degree* ya kwanza atapokwenda chuo chengine chochote ulimwenguni

atakuwa ni bora zaidi kuliko mwengine yoyote. Nasema hayo kwa ushahidi Mhe. Spika.

Mimi nimemaliza darasa la kumi na mbili lakini nikapata masomo ya Chuo cha Uchumi ya mwaka mmoja halafu nikenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna chuo cha Afrika Mashariki kusomea takwimu na baadaye Marekani. Nilipofika kule nilikuwa bingwa, nikarudi hapa nikapata masomo tena Uingereza *Schoo of Tropical Medicine* miezi sita. Wazungu barua nimeisahau walitaka kuniajiri na kupewa uraia. Kwanza nilikuwa nikafanye *research* ya *PNG* ambayo ilikuwa inachukua miaka miwili na nusu baadaye watanipa mafunzo ya miezi sita halafu nifanye kazi kwa mkataba wa mshahara mzuri wa miaka mitatu mitatu.

Mimi mwenyewe nimejiona sina elimu, lakini wataalamu wa *university* kwa sababu *university* zote nilizosoma sio za masihara. Nimesoma *North Caroline*, *School of Tropical Medicine of Liverpool* safi kabisa na wao waliniona kumbe ni mtaalam bora na niliwashinda madaktari kutoka Ufaransa, Denmark mpaka India. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kigezo hicho mimi nawasifu wenzetu kwa sababu mimi nimesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi nasema kiwango chetu ni kikubwa lakini wenyewe hatuwezi kukiona.

Mwanafunzi anayetoka Zanzibar akienda vyuo vyengine vyovyote nakwambia anafanya vizuri na anakuwa na sifa mbele ya wanafunzi wa nchi nyengine zote. Utaona wanafunzi wetu hawafeli wakienda huko kutokana na ubora wa elimu wanayopata. Kwanza niwapongeze wataalamu wetu.

Walimu wana haki zote za kusifiwa hasa wale wanaosomesha vyuo vikuu sasa hivi kwa kubakia. Hapa ubavuni ninaye rafiki yangu *Prof.* Mshimba mtaalamu wa hesabati mzuri. Wazungu wanamtaka kasoma chuo kikuu akaenda Ujerumani wakamwambia abakie akasema ata, akarudi kwao kwa sababu hapa tulikuwa hatuna chuo kikuu akawa kwa ndugu zetu Bara kwa uzalendo wake. Baada ya sisi kuanzisha Chuo Kiku hapa akasema nitakuja kwetu kwa sababu yeye ni mtu wa Paje huyu kaona lazima asomeshe hapa hapa. Mimi nampongeza sana.

Ubavuni pangu hapa pana Dr. Ismail Kanduru, na yeye kwa uzalendo wake amebakia. Hivi sasa taaluma yoyote ya biashara bidhaa inayotakiwa vyuo vikuu hivi sasa vimekuwa kama utitiri lakini nyenzo yake wataalam. Wenzetu hawa wamebakia hapa lazima tuwapongeze sana ni huo uzalendo. Huko kuna mapesa chungu nzima, mafursa chungu nzima lakini wamebakia hapa. Mhe. Spika, mimi nawapongeza sana sina cha kuwalipa. Lakini Mwenyezi Mungu kwa uzalendo wao atawapa kheri na mafanikio yao kwa kuwatumikia ndugu zao.

Mhe. Spika, isitoshe napenda Mhe. Waziri awawekee mazingira mazuri. Maana yake hawa ni binadamu, hawa wawili nimewaeleza kwa sababu ya uzalendo, tutakapopata na wengine zaidi ya hawa watakuwa hawana uzalendo huo lakini angalau kuwe na kitu cha kuwavutia. Mhe. Spika, mishahara yao tuipandisheni, kama njia ya kupandisha mishahara nafasi hatuna basi kuwe na posho maalum angalau shilingi laki tano mpaka milioni kwa mtaalam pale, akipumzika basi mbali ya mshahara wake. Hata kigari cha *second hand* ukiwatafutia ni moja ya motisha.

Lakini na makaazi Mhe. Spika, amezungumza Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba walimu hawana nyumba za kuweza kuwa ni kivutio. Amerudi chuo kikuu anataka kusomesha hapa bado akakae Kwamtipura kwenye kibanda uchochoroni. Anatakiwa kwenda chuo kikuu kama kesho kutwa tuna majengo mazuri pale Tunguu lakini nyumba za kukaa bado hazipo, itabidi asomeshe kule arudi tena Jang'ombe haifai. Kwa hivyo, haya nasema yafikiriwe nayo, wataalam wetu tuwawekee mazingira ili tubakie nao tuweze kuchota elimu wapatiwe vijana wetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika ujenzi wa madarasa. Nawapongeza wananchi wote, maana yake sasa hivi Kaskazini, Kusini Unguja na Pemba wamehamasika kujenga madarasa kuisaidia serikali yao. Kwa kweli kasi yao sasa hivi imezidi nguvu za serikali. Kwa hivyo, napenda wasaidiwe ili wasivunjike moyo kwa sababu kasi hii tuliwapa sisi wenyewe na wamekubali. Hivi sasa madarasa mengi yako mabanda bado hayajaezekwa.

Mojawapo Mhe. Spika, pale Jumbi mji mpya, Mhe. Waziri miaka minne zaidi alikuja na wageni wa Kimarekani pale huko tunakopata misaada ya vitabu akasema hapa mkija mwakani kusherehekea Mapinduzi mtayakuta tayari, mpaka leo. Mhe. Spika, nataka akigombania urais akaifungue yeye mwakani ile katika sherehe za Mapinduzi. Kwanza namuombea kheri ashinde na sherehe za Mapinduzi za mwaka 2011 awe ndio mgeni rasmi pale aifungue badala ya kuja wale Wamarekani. Kwa hivyo, nafikiri namtia ari. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, pia mengine yapo, ninalo Tunguu, Machui na kwengineko. Kwa hivyo, jitihada kama hizi zipo kwa wananchi na lazima tuziunge mkono kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, jengine uhifadhi wa magofu na mambo ya kale. Jitihada kubwa zimechukuliwa za kuhifadhi magofu chini ya wizara hii. Kwa bahati nzuri mimi kipindi cha miaka mitano iliyopita nilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, nilikuwa na wizara hii kwa muda mwingi nimeona jitihada zilizochukuliwa. Tumbe kule, Chwaka, hata msikiti ule wa

Shumba Mjini, tumeuona msikiti wa Kizimkazi, tumekwenda Mkumbuu na kwengineko. Jitihada za kuhifadhi hazina hii zinachukuliwa tunawapongeza.

Lakini sasa hivi nina maswali mawili nimuulize yanayohusiana hasa na jimbo langu la Koani. Kwanza mji wa kale Unguja Ukuu zile harakati za kuhifadhi mji huu zimefikia wapi. Maana yake walikuja wataalam wa *research* hapa wakachimba wakapata pesa ukaonekana ni mji wa kwanza Afrika ya Mashariki ambao umeanzishwa tangu karne ya 4 AD. Lakini bado harakati zile zimezima kimya. Wafadhili mbali mbali wa *UNDP* walisaidia pale lakini sasa hakuna kinachoendelea. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kuna nini.

Lakini la pili kuna gofu la Bihole chini ya mradi wa jamii wa *TASAF* wananchi wa pale wamepata fedha kuliendeleza gofu lile ili baadaye na wao pembezoni mle waweze kufanya vibanda vya biashara. Watalii wasome historia ya Bihole lakini wakati huo huo waweze kupata *juice*, matunda, embe nzuri za pale Bungi na samaki au pweza.

Mhe. Spika, juzi umenijia ujumbe wa wanachama wale nyumbani wakanambia kwamba wakati wa kupimwa eneo lile lilipatiwa hatimiliki, sehemu nzima imemegwa na imeuzwa kwa thamani ya kiasi ya shilingi milioni nane kwa kampuni ya simu kwa ajili ya kujengwa mnara sijui. Sasa Mhe. Waziri anajua hili, kama hajui afanye utafiti. Mhe. Spika, kesho hakuna Baraza, afanye kazi hiyo mpaka Jumatatu wakati wa majumuisho nafikiri atakuwa kapata jawabu. Jambo hili kama kweli limefanyika basi aliyehusika kumega ardhi ya eneo la hifadhi ya Bihole afikishwe mbele ya vyombo vya sheria.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu utaratibu wa huduma za wanafunzi. Bado mji wetu unakua, skuli bado zinatawanyika sehemu mbali mbali, harakati za ndani ya mji za magari, mapikipiki, gari za ng'ombe zimekuwa kubwa. Kwa hivyo, watoto kwenda skuli kwa miguu imekuwa ni hatari. Usalama wao hivi sasa lazima wapelekwe skuli kwa magari. Gari tunazozitumia sasa hivi ni madaladala bado zina upungufu hazitoshi kwa sababu daladala hizo hizo zipakie wafanyakazi kufika makazini mwao na watoto wanataka kwenda skuli.

Sasa juzi nilimsikia Mhe. Rashid Seif Suleiman akichangia kwenye bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Fedha na Uchumi kama sikosei. Basi hawa wenzetu taasisi ziliopo Mhe. Waziri hashirikiani nazo angalau akatupa tukaweza kupata mabasi yakawa maalum kwa watoto wa skuli kwa sababu wenzetu ndio wanavyofanya ili wasipate kufinywa finywa. Joto lile ndani ya gari hata mtoto akifika skuli hawezi kusoma kutokana na kufinywa kwenye gari. Maana wengine kwa sababu anatoa shilingi mia hapewi hata kibao anaambiwa akae chini akifika skuli sare yake yote imechafuka. Kwa kweli watoto wetu wanakwenda skuli katika hali ya mazingira magumu.

Mhe. Spika, kuna na hizi skuli za binafsi wao wana magari maalum lakini watoto wanawachukua wengi na magari yao yanatishia usalama. Kama skuli ya *Highview* wana magari mawili tunayaita nyambizi watoto wanatiwa zaidi ya mia moja katika gari hilo hawana hata nafasi, wengine utafikiri watoto wa bandia.

Kwa hivyo, wale waangalizi wetu wa elimu nafikiri mkono wao unafika katika skuli za binafsi, waone hali hii wawape maelekezo. Uwezo wa gari kuchukua watoto arubaini, basi anaweza kuongeza angalau watano au kumi kwa idadi ya hamsini, lakini watoto wadogo kuwatia wengi ndani ya gari ikitokezea ajali tutakuwa na maafa makubwa. Mhe. Spika, naomba utaratibu uwepo maalum wa wanafunzi wa kupata usafiri wa uhakika na usalama wa kuweza kufika maskulini mwao.

Mhe. Spika, niipongeze Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa utaratibu wao wa kuwarekebishia mishahara walimu. Najua binadamu hatosheki atataka moja apewe mbili, akipata mbili atataka tatu. Lakini serikali imejitahidi na hii ni kutokana na juhudi za mwenyewe Mhe. Waziri kwa sababu na yeye alikuwa mwalimu ana uchungu wa kazi hiyo. Fedha walizopewa nawaomba wenzetu walimu wazikubali na sisi ndio mnatuona tunakupigieni debe, kikiingizwa tu isitosheleze tukaambiwa walimu tumeshawaongeza mwaka jana aaa. Kama karafuu zitapatikana nyingi, watalii wamekuja wengi tusione tabu na mwakani kuwaongezea tena.

Mhe. Spika, hili naomba kwa serikali, Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi namwambia pesa zikiwepo nyengine tumezipata ampe Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali awaongezee walimu. Kwa sababu nchi hii bila ya elimu haipatikani na walimu bila ya kupewa motisha hawawezi kupatikana. Kwa hivyo, ili ng'ombe huyu aweze kutoa maziwa mengi basi tumpe majani mengi na maji mengi ili tuweze kukamua maziwa ya kutosha tunyonye na tupate vitamin ya kutosha.

Mhe. Spika, mimi kidogo wakati wa upandishwaji wa mshahara huu kulitoka kauli kwa Chama cha Walimu sikuipenda na naweza kusema ilikuwa ni ya uchochezi. Vyombo hivi tumekubali viundwe kwa maslahi ya kusaidiana, kiwe ni chombo cha kurekebisha mafanikio, yakipatiwa serikali ya muajiri pamoja na muajiriwa. Kama kulikuwa na kasoro basi vikao vya ndani vifanyike lakini si kutoa kauli ya *public* kama walivyotoa Chama cha Walimu baada ya Mhe. Waziri kuweka nyongeza katika mishahara ile. Kwa kweli mimi ilinisikitisha kwa sababu kazi hiyo tunaifanya kubwa hapa lakini hakukuwa na shukrani hiyo hata Mwenyezi Mungu anakataa. *Wa inshakkatu la zidat, wa inkafartu inna adhabi la shadid.*

Kwa hivyo, kama walimu hamridhiki na hichi Mwenyezi Mungu hayupo pamoja na nyinyi jamani. Tafadhalini pokeeni kidogo na Mwenyezi Mungu atatupa kingi.

Mhe. Spika: Hayo maneno niambie mimi huku yatafika huko. *(Kicheko)*

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nawausia walimu wangu kidogo tulichoongezwa tukipokee na tukikinai hicho kidogo kingi kitakuja. Bado serikali hii ina imani sana tupate elimu na walimu tunawajua kazi yao ngumu. Mimi siiwezi kazi ya ualimu kwa sababu nilipopewa hiyo barua ya kwenda Ulaya nimekataa. Kwa hivyo, hao waliokubali najua ni majasiri na Mwenyezi Mungu atawasaidia.

Mhe. Spika, naishukuru wizara hii kwa kutumia fedha vizuri kwenye miradi yote ya maendeleo. Nafikiri mafanikio haya yamepatikana kutokana na viongozi hasa kinamama. Maana yake idara ile Katibu Mkuu ni Bi Mwanaidi Saleh Abdulla namuombea dua. Lakini pia mkurugenzi anayeshughulika na fedha Bi Khadija Moh'd Ali ni mwanamke. Mhe. Spika, hawa ni watu waaminifu na tupendelee kuwapa nafasi kinamama na wao wanaweza. Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kupanga timu ya udhibiti wa fedha kwa kinamama na kwa hivyo naiunga mkono hoja ya Mhe. Waziri mia juu ya mia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kutekeleza wajibu wetu kwa mashirikiano makubwa.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 28/6/2010 saa 3:00 asubuhi)